Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILINAO YA BUNGE

## MKUTANO KUMI NA TATU

**Kikao cha Nne – Tarehe 31 Oktoba, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 40

**Makumbusho ya Taifa ya Mwalimu J. K. Nyerere**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI (K.n.y. MHE. NIMROD E. MKONO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Makumbusho ya Kitaifa ya Mwalimu J. K. Nyrerere yaliyoko kwenye kijiji cha butiama yalifunguliwa na Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Fredrick T. Sumaye hapo tarehe 2 Julai, 1999 kwa lengo la kutafiti, kuhifadhi, kutoa elimu kwa Umma na kutunza Kmbukumbu za ki-historia za Baba wa Taifa na za Taifa kwa ujumla; na kwa kuwa Makumbusho hayo yamekuwa kichocheo cha Utalii wa ndani ambao unachangia paoto la ndani la Serikali lakini yako katika hali mbaya ya ukosefu wa fedha, watumishi wachache n a uhaba wa nyumba za kuishi watumishi:-

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyaboresha Makumbusho hayo ili yawe ya kisasa kwa kuongeza na kuanisha maeneo ya Kumbukukmbu za kihistoria za Baba wa Taifa, kuboresha mazingira yake, kujenga nyumba za watumishi wake na kuweka urafiki kwa ajili ya watalii?

(b)Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu Makumbusho hayo yakawekwa chini ya Serikali kuu ili itengwe fungu maalum la Bajeti ya Serikali na kuondoa ile dhana ya kueleweka kuwa Makumbusho hayo ni Shirika la Umma na pia iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi mkubwa kwani shughuli zake zinafanana na zile za Makumbusho yote hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mbunge wa Musoma vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Shirika la Makumbusho ya Taifa, linaendelea na mchakato wa kuongeza na kuanisha maeneo ya kumbukumbu za historia ya Baba wa Taifa kama moja ya majukumu yake. Katika kuboresha mazingira yake, kiasi cha shilingi milioni sitini (60,000,000/=) kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari jipya ili kurahisisha utendaji wa kazi katika makumbukusho hiyo. Aidha bajeti kwa ajili ya makumbusho ya Mwalimu J. K. Nyerere imeongezeka katika kipindi cha miaka minne (4) kutoka Tsh. 14,561,580 mwaka 20005/2006 hadi Tsh. 123,624,202.40 mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha kiasi cha shilingi milioni thelathini na moja (31,000,000,000/=) kimetengwa kwa ajili ya kununua na kutengeneza mitambo ya kudhibiti wizi. Hili ni katika kuthamini umuhimu wa mikusanyo hiyo ambayo ni adimu na ni urithi muhimu kwa Taifa letu. Serikali itaendelea kuyaboresha makumbusho haya ili kufanya yawe ya kisasa zaidi na kuboresha makazi na mazingira ya kazi ya watumishi kupitia bajeti zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia katika bajeti ijayo (2009/2010), Serikali imekusudia kutenga fedha kwa ajili ya nyumba za watumishi. Ili kuweka urafiki kwa ajili ya watalii, njia pekee ni kutangaza makumbusho hayo ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza hilo, mabango ya kutangaza makumbusho hayo yamewekwa katika barabara kuu ya Mwanza kwenda Musoma. Aidha makumbusho hayo yanatangazwa kupitia tovuti za nyumba ya sanaa *(www.housefculture.or.tz)* na makumbusho (www.musemu.or.tz) Aidha mipango inafanywa ili kuiunganisha tovuti ya makumbusho na tovuti ya Bodi ya Utalii ambayo ina jukumu la kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Makumbusho ya Mwalimu J. K. Nyerere yaliyoko Butiama ni sehemu ya Shirika la Makumbusho ya Taifa ambalo lipo chini ya Serikali Kuu na Wizara imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya makumbusho hayo kama ilivyoainishwa katika sehemu (a) hapo juu na itaendelea kuyaboresha kadri bajeti itakavyoruhusu.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu kama Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na eneo maalum kwa ajili ya ukumbusho wa viongozi wa kitaifa kwa sababu sisi kama nchi hatuna eneo maalum *(Heroes Acer)* ambayo viongozi mbalimbali wa kitaifa wanapokufa au kunapotokea mambo ya kitaifa tuliyokuwa tunasema ambayo wananchi kwa urahisi zaidi wanaweza kupafikia na kuweza kupajulisha kwamba makumbuhso ya kitaifa. Je, Serikali ina mpango wowote ule wa kuanzisha eneo maalum kama makumbusho kwa ajili ya viongozi wetu wakuu wa kitaifa?

**NAIBU SPIKA:** Lakini tuna sheria tumepitisha hapa sehemu ya kuzika viongozi.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema sheria zinazotawala uhifadhi wa kumbukumbu za mali na rasilimali za taifa ziko katika makundi mawili. Kuna zile ambazo zinahusu viongozi ambao tulipitisha mwaka 2004 Sheria ya kuwaenzi waasisi wa Taifa na ile sheria ambayo ni ya mwaka 1972 ambayo ndiyo inayotawala makumbusho ya sasa hivi.

Sasa katika sheria hii ya kuenzi waasisi wa Taifa, sheria hii imeainisha namna ya kuenzi na namna ya kutunza Kumbukumbu zao. Katika sheria ya Makumbusho ambayo tunayo kwa sasa hivi nayo inaainisha kwamba mali za Taifa zinahusu au zinahifadhiwa kwa kushirikiana na wadau wengine kwa sababu hawa viongozi pia wana familia zao. Kwa hiyo, baadhi ya vitu vyao ambavyo wanavihitaji au wamekuwa wakivitumia yaani *personal properties* ya familia hizo tunaviweka kwenye Makumbusho kama tulivyoweka Makumbusho ya Butiama na ile tutakayoweka hapa Dodoma kwa kushirikiana na familia zenyewe. Kwa hiyo, mpango uliopo ni kutumia hizi sheria mbili kwa kushirikisha familia za wahusika.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa swali la msingi linazungumzia juu ya makumbusho ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na kwa kuwa makumbusho ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere yako mengi sana na kumbukumbu mojawapo ambayo ilikuwa inatakiwa kutunzwa ni ile ambapo siku alipofariki pale uwanja wa taifa kilijengwa kibanda ambacho kilitumia fedha nyingi sana na kile kibanda tukaambiwa kwamba kitahifadhiwa kwa ajili ya kumbukumbu yake ili kwamba vizazi vijavyo kuja kukiona na kushuhudia kwamba baba kwamba alizikwa kupitia kibanda kile. Sasa je, kile kibanda kiko wapi na kama kipo kinatunzwa kwa ajili ya maonyesho?

**NAIBU SPIKA:** Sina hakika anaweza kujibu kile kibanda unakijua kiko wapi? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema sheria ya Makumbusho ya taifa ina mapungufu na sasa hivi tumeshakamilisha kutengeneza sera ambayo itapelekea kuundwa kwa sheria mpya. Mapungufu yaliyopo kwenye sheria ile ni kwamba kumbukumbu ambazo zinahifadhiwa kwa mujibu wa sheria ni zile ambazo ni viu visivyohamishika vilivyotengenezwa zaidi ya mwaka 1863. Kwa hiyo, kuna vitu vingi sana ambavyo ni vizuri na vinafaa lakini haviko *covered* na sheria hiyo. Kwa sera ambayo tumetengeneza sasa hivi tunavi- *cover* vitu hivyo. Lakini ndani ya sheria hiyo inamruhusu Waziri wa Maliasili na utalii kutangaza kitu fulani kwamba na chenyewe kihifadhiwe na moja ya vitu ambavyo vinakuwa *covered* na tangazo na tamko la Mheshimiwa Waziri ni pamoja na vitu kama hivyo ambavyo vinahusu kumbukumbu za karibuni sana zinazohusu watu maarufu kama hicho kibanda. Kwa sasa hivi kibanda hicho kimehifadhiwa vizuri lakini hakijaanza kutumika kwa ajili ya maonyesho. Kimehifadhiwa vizuri hapa nchini. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 41

**Wilaya ya Serengeti Kunufaika na Uwekezaji wa Mahoteli ya Kitalii**

**MHE. ROSEMARY S. KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Serengeti ina vivutio vikubwa vya Utalii kutokana na kuwepo kwa mbunge ya wanyama ya Serengeti na kwambakuna hoteli nyingi za kitalii kwenye maeneo ya uwindaji katika mbuga hiyo:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuongeza viwango vya mapato yatokanayo na vitanda *(% bed fee)* ili Halmashauri ifaidike na uwekezaji huo?

(b)Je, kwa nini Serikali imempatia mwekezaji huyo sehemu yote ya uwindaji hata yale maeneo ya wazi ambapo wananchi wa mkoa wa mara hawaruhusiwi kuwinda sehemu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Usimamizi wa shughuli za matumizi ya wanyamapori yasiyo ya uvunaji *(Non-consumptive wildlife use)* katika maeneo yenye wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Mamalaka ya Hifadhi eneo la Ngorongoro ulikuwa unafanyika kwa kuzingatia Kanuni za Usimamizi wa matumizi ya Wanyamapori yasiyo ya uvunaji ambazo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali Namba. 196 la tarehe 14 Septemba, 2007. Kanuni hizo zilionekana kuwa na upungufu katika mgawanyo wa mapato kwa Halmashauri za Wilaya na vijiji.

Serikali imefanya mapitio ya Kanuni hizo, na kuandaa kanuni mpya zitakazoanza kutumika hivi karibuni. Kanuni hizi mpya zimeanisha viwango vya mapato ambapo mgawanyo utakuwa asilimia 80 kwa Halmashauri na jumuiya za wananchi (Halmashauri 15% na 65% Jumuiya za wananchi na asilimia 20 tu ndiyo itakayokwenda Serikali kuu. Asilimia hizo ni kwa mapato yote ya makusanyo ya ada ikiwa ni pamoja na *bed night fee.* Hivyo kanuni mpya zitaongeza mapato kwa wananchi na Halmashauri ikiwa ni pamoja na Serengeti.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni za uwindaji wa kitalii zinatakiwa kuchangia shughuli za miradi ya maendeleo ya wananchi, uzuiaji ujangili na maendeleo ya vitalu, kulingana na kanuni za uwindaji wa kitaliii za mwaka 2000 na marekebisho yake. Katika utaratibu huo, baadhi ya kampuni hutoa michango ya fedha, vifaa mafuta ya magari na watumishi kwa ajili ya doria. Katika kutekeleza wajibu huo, kampuni ya *Grumeti Reserves* hutoa watumishi ambao hushirikiana na watumishi wa Idara ya Wanyamapori katika kufanya doria za pamoja chini ya uongozi wa watumishi wa Idara ya Wanyamapori. Katika mantiki hiyo, kampuni ya *Grumeti Reserves* haina Jeshi bali

linachangia watumishi wake ambayo Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia idara yake ya wanyamapori imekuwa ikifanya doria kwa kushirikiana nao.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Grumeti Reserves* iligawiwa maeneo (vitalu) matatu kwa ajili ya shughuli za uwindaji wa kitalii. Vitalu hivyo ni mapori ya akiba ya Grumeti na Ikorongo vilivyogawiwa mwaka 1994 pamoja na eneo la wazi la *Fort Ikoma* lililogawiwa mwaka 1997. Vitalu hivyo viligawiwa kwa kuzingatia taratibu na kanuni za uwindaji wa kitalii za mwaka 2000 na marekebisho yake. Umiliki wa vitalu hivyo utamalizika mwezi Desemba, 2009 baada ya kipindi cha uwindaji *(Hunting term)* cha sasa kumalizika. Katika misingi hiyo, kampuni ya *Grumeti Reserves* haijagawiwa maeneo mengine zaidi ya hayo ndani ya utaratibu ambao uko ndani ya kanuni za mwaka 2000.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kwa mara nyingine, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla kwa jitihada nzuri wanazozifanya. Lakini bado ninayo maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a)Kwa kuwa katika Wilaya ya Serengeti Mbunge ile ya Serengeti sisi kwetu ndiyo kama mgodi na kwa kuwa katika Wilaya ile kuna mahoteli makubwa ya kitalii ambapo hutoza mpaka dola 1500 kwa kichwa lakini hoteli hizi hazichangii kitu chochote kwa maana ya kwamba ushuru wa vitanda kwa Halmashauri yetu na hivyo kupelekea Halmashauri yetu kuwa na kiwango kidogo cha mapato hata kama tuna hoteli hizo katika Wilaya yetu. Je, Wizara haioni sasa ni wakati muafaka kwa mahoteli makubwa kama *VIP*, Solonela na mengine yote kuanza kuchangia ushuru wa vitanda kwenye Halmashauri yetu?

(b) Kutokana na kutokuwindwa kwa mapori ambapo kwa sasa yamepewa kwa mmiliki wa Grumeti hii imesababisha wanyama kuongezeka na hasa wanyama kama tembo ambao wamekuwa wakitoka kwenye maeneo na kuwaingilia mpaka majumbani wananchi na kula mazao yao, kula mifugo yao na hata akiba yao ya chakula. Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wa kuwapunguza wanyama hao kwa kuwaruhusu wananchi wa Serengeti waweze kuwinda kwenye maeneo haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali kule nyuma ilikuwa haitozi hizi *bed fees* na kuzitoa kama fedha kwa Halmashauri. Kwenye hizi kanuni ambazo nimesema kwamba za mwaka 2007 tangazo namba 196 ndiyo tulipoweka utaratibu huo wa ku-*charge* hizo *fees* lakini zililalamikiwa sana na wadau wakiwemo wananchi wa maeneo hayo ndiyo sasa tumetengeneza kanuni zingine tena ambazo ziko kwenye hatua ya mwisho kabisa ya kusainiwa ambazo zinaweka katika kifungu namba 15 za kanuni hicho zitakapokuwa zimekamilika zinaonyesha kwamba kutakuwepo na mgawanyo wa mapato na mapato yatakayogawanywa ni mapato yote *including* hizo *bed night fees*.

Tumesema kwamba Halmashauri pamoja na jamii jirani itakuwa inapata jumla ya asilimia 80 na Serikali Kuu itachukua asilimia 20 tu. Kwa hakika kanuni hizi zitakapokuwa zimekamilika na kuanza kutumika, mapato yatakayopatikana kwenye

Halmashauri hizo yatakuwa ni makubwa sana hakika kuzidi hata maeneo ambayo yana migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la kuongezeka kwa wanyama na kusababisha uharibifu wa mali na maisha ya binadamu hili tatizo haliko Serengeti peke yake liko karibia maeneo mengi ya nchi hii.

Lakini majadiliano yamekuwa yakiendelea kama Mheshimiwa Naibu Spika unavyofahamu na pamoja na Wabunge wengine kwamba sasa hivi tunatengeneza sheria nyingine ambayo hakika mwezi Januari itakuwa hapa Bungeni ambayo baadhi ya mambo inayojaribu ku-*address* ni pamoja na namna yaku-*deal* na uharibifu wa mali za binadamu zinazosababishwa na wanyama kutoka kwenye hifadhi zetu.

Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa mchakato unaendelea acha ukamilike tutaweka utaratibu mzuri zaidi.

Lakini pia niseme kwamba kuhusu namna gani wanyama hawa watapunguzwa au watafanywaje kwamba wameongezeka sana kuna mchakato unaoendelea TAWIRI ambayo ni taasisi ya utafiti wa wanyamapori, wanafanya sensa ya wanyama na hili tumekuwa tumekuwa tukilisema hapa Bungeni tokea kipindi cha bajeti cha mwaka huu kwamba wanafanya sensa ya wanyama kujua *total population* yao na kujua mtawanyo wao kwenye hifadhi zetu mbalimbali ili kujua nini kifanyike baada ya utafiti huo. Kwa hiyo, hizi shughuli mbili zikikamilika matatizo yatakwisha.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu kuna semina ya wanyamapori, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 42

**Hifadhi ya Ngorongoro – Kuwaendeleza Wananchi Wenyeji**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya majukumu ya kisheria iliyopewa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ni pamoja na kuwaendeleza wenyeji (Wamasai) hususan katika sekta ya mifugo, elimu, ajira na utalii:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani wananchi wa Ngorongoro wameendelezwa na Hifadhi hiyo katika sekta hizo hadi sasa?

(b) Je, ni kwanini wenyeji hawaruhusiwi au wanawekewa masharti magumu yanayofanana na wale wawekezaji wa nje wanapoanzisha *campsite*?

(c) Je, ni nini mchango wa Shirika hilo la Umma katika ajira ya Watanzania wakiwemo wenyeji wa Ngorongoro?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Telele (Ngorongoro) lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Eneo la hifadhi ya Ngorongoro imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo ya kijamii kama moja ya majukumu yake makuu tangu ilipoanzishwa mwaka 1959.

Katika miaka 6 iliyopita Shirika limetekeleza miradi ya elimu, afya, mifugo, chakula, maji na barabara katika tarafa ya Ngorongoro kupitia Baraza la wafugaji na jumla ya shilingi bilioni 2,931 kama ifuatavyo:- 2002/2003 shilingi milioni 552.7, 2003/2004 shilingi milioni 551.1, 2004/2005 shilingi milioni 524.1, 2005/2006 shilingi milioni 600, 2006/2007 shilingi milioni 703.3.

Aidha Shirika limetekeleza na limepanga kutekeleza miradi mbalimbali kwenye Tarafa zingine nje na ile tarafa ya Ngorongoro na jumla shilingi bilioni 2,291 zitakuwa zimetumika ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Miradi hiyo ni mingi, mingine imeshakamilika mingine bado inaendelea lakini nimeweka figure hizi kwa pamoja tu, miradi hiyo ni pamoja na Tiba ya mifugo na maji; ambayo kuna jumla shilingi milioni 350 kuna miradi elimu inayohusu ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, nyumba za walimu shilingi milioni 792 zimetuka, ada za wanafunzi kuna jumla ya wanafunzi 570 wanaosomeshwa kwa ufadhili wa shirika la Ngorongoro na jumla shilingi milioni 390, zimetuka. Tuliwahi kununua katika kipindi cha mwaka jana Chakula/ Mahindi ya bei nafuu kwa ajili ya kuyauza kwa wananchi katika kipindi hicho na shilingi milioni 50 zilitumika, ukarabati wa Hospitali ya Endulen shilingi milioni 10, Hosteli za Baraza la Wafugaji shilingi milioni 100, Miradi ya vijiji shilingi milioni 160, Kuwezesha vikundi vya kina mama shilingi milioni 10 mradi wa uji mashuleni shilingi milioni 75 na mradi wa barabara kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya shilingi milioni 362. Kwa mwaka huu wa fedha shirika limetenga shilingi bilioni 1.25 kwa ajili ya miradi katika Tarafa ya Ngorongoro kupitiai Baraza la wafugaji.

(b) Wenyeji waishio kwenye Hifadhi wamekuwa wakipewa haki sawa na wawekezaji wengine katika sula zima la kujenga makambi ya kulala wageni ili kutoa huduma bora kwa watalii. Utaratibu ulioo wa kuanzisha makmbai mapya unazingatia kutoa matangazo ili watu mbalimbali wenye sifa wakiwemo wenyeji waweze kuomba. Aidha, mwombaji hutakiwa kufanya tathimini ya athari za kimazingira ili kuona kama kutakuwepo na athari yoyote kimazingira kwenye maeneo yaliyokusudiwa kujengwa mradi. Hivi sasa wenyeji wana makambi 12 ya kupumzika watalii na watembeao kwa miguu na maboma ya kitamaduni 10.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kama yalivyo Mashirika mengine ya umma, ajira zake zote zinazingatia mahitaji katika idara

mbalimbali na sifa za kitaaluma zinazotakiwa. Shirika limeajiri wafanyakazi wenyeji 70 kati ya wafanyakazi wake 420 kutoka eneo la Ngorongoro.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Ukiangalia takwimu hizi utadhani kama ingekuwa inatekelezwa vizuri Ngorongoro ingekuwa mbinguni kwa kweli lakini nataka niseme kwa sababu umesema kwamba hii sheria ya wanyamapori tutaijadili Jumapili na kwa kuwa nilikuwa nimeomba pia Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira watembee Ngorongoro na wazungumze na Baraza la Wafugaji basi labda haya tutachambua mbele ya safari kama ni kweli au si kweli. Kwa hiyo, sina la kuuliza sasa hivi tutajaribu kucheki haya mambo mbele ya safari. Maana mengi si kweli. Nakushukuru.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sheria ya kuanzishwa kwa mamlaka ya Ngorongoro inaweka ukomo wa idadi ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Ngorongoro kati 6 na 11 na kwa kuwa Waziri aliyekuwa na dhamana aliteua wajumbe wapatao 15 katika bodi hiyo kitendo ambacho kinaongeza gharama kwa bodi na kwa mamlaka ya Ngorongoro na kupunguza wa kusaidia miradi hii ya wenyewe na miradi mbalimbali.

Je, Serikali haioni kwamba imefika wakati wa kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi hiyo ili kupunguza matumizi makubwa ambayo yako huko na kuelekeza kuwasaidia wananchi wa Ngorongoro ambao wana shida ya shule na Hospitali katika maeneo hayo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida ni kwamba wajumbe wa bodi yoyote ile wa Wizara yangu wanaweka kufuatana na sifa mbalimbali.

Sifa ya kwanza tunaweka wale ambao tunajua kwa mujibu wa kazi zao wanaweza wakaingia kwenye bodi ili kuweza kutoa mchango na kutoa ushauri mzuri.

Sifa ya pili tunaongeza wananchi ambao tunajua kwamba kwa njia moja au nyingine masuala ya kule yanawahusu au pia na wenyewe wanaweza wakawa na mchanga.

Sasa nimepokea alichoongea na pia tutazingatia kwa kuangalia kwamba wakati mwingine tunapochagua bodi tutaangalia zaidi na kuona kwamba mchango ukoje.

Lakini hata hivyo pia nataka nimfahamishe Mheshimiwa kwamba fedha inayotumika katika shughuli za bodi haina uhusiano na fedha ambayo tunatoa/tunachangia kwa ajili ya Maendeleo ya sehemu yoyote inayohusiana na shughuli za uhifadhi.

Na. 43

**Mafunzo kwa Vikundi vya Ujasiriamali**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali ni moja ya mikakati ya Serikali ya kukuza biashara ya ndani na nje; na kwa kuwa, wakulima wajasiriamali wa vijijini hususan katika jimbo la Peramiho wameanzisha vikundi vya wakulima vya usindikaji na kwamba wengi wao hawajapatiwa mafunzo kutokana na ufinyu wa bajeti ya Halmashauri.

Je, Serikali kuu kupitia vyanzo vyote mbalimbali, iko tayari kusaidia vikundi hivyo vya wajasiriamali kufanikisha malengo yao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha vikundi vya wajasiriamali vinawezeshwa kufanikisha malengo yao kwa kupatiwa mafunzo kulingana na shughuli zao wanazofanya. Kwa kuzingatia hilo, juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanywa kuhakikisha wakulima na wazalishaji wadogo wanapatiwa mafunzo ya kutosha kuimarisha nafasi ya katika ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka 2006/2007 kupitia *SIDO* jumla ya wajasiriamali 66 walipewa mafunzo ya aina mbalimbali na Wizara yangu katika Mkoa wa Ruvuma wakiwemo wajasiriamali 41 wa usindikaji wa vyakula katika jimbo la Peramiho.

Katika programu ya mafunzo ya *SIDO* Mkoani Ruvuma, kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha vikundi vilivyopo Jimbo la Peramiho vitapatiwa mafunzo ya ujasiriamali na usindikaji vyakula mwezi Februari, 2009. Hata hivyo walengwa wanahamasishwa kuchangia kiasi kidogo cha gharama ili kupatiwa huduma husika kulingana na mahitaji.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa sekta kipaumbele katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara ni pamoja na kukuza sekta ya viwanda vidogo kwa wakulima vijiji ili kuwafanya uzalishaji wao uwe wenye tija. Je, Wizara sasa iko tayari kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwanza kukuza kilimi cha miwa kwa wajasiriamali ambao wako katika jimbo la Peramiho hatimaye kuwapa mafunzo na kuwasaidia kupata viwanda vidogo vidogo hivyo vya kusindika na miwa kati jimbo hilo la Peramiho?

Mheshimiwa Naibu Spika, na pili wakulima hao na wajasiriamali hao wadogo wadogo kupitia jimbo la Peramiho wamefanya kazi kubwa sana ya kujichangia wenyewe na hatimaye kufanikiwakupata mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo yao, je, Wizara sasa iko tayari kuja kufanya kazi na vikundi hivyo ambavyo vimekwisha kupata mafunzo kuwasaidia kufungua viwanda vidogo vidogo kulingana na ujasiriamali waliojifunza kama usindikaji wa uyoga, matunda na mazao mengine ambayo wameshayafanyia kazi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukubaliana naye kabisa kwamba mkakati wa Wizara yangu ni kuimarisha viwanda ambavyo vinachangia kuimarisha kilimo kwa maana ya kwamba vile viwanda ambavyo vinaongeza thamani ya mazao kwa kweli tunavipa vipaumbele. Na napenda kumhakikishia kwamba pendekezo lake tumelipokea tutawasiliana na Wizara ya Kilimo na tunaomba ushirikiano wake yeye mwenyewe ili kama kuna hao wakulima wa miwa ambao wanahitaji kusaidiwa kuanzisha viwanda vidogo tuweze kuwashauri nini cha kufanya.

Swali la pili la kuhusu wajasiriamali ambao wamefanya kazi kubwa kwanza napenda kwa niaba ya Wizara kuwapongeza wakulima hao, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jenista anavyoshirikiana na kuhusu hili suala la Wizara yangu kwenda kufungua viwanda napenda nirudi tena swali langu la msingi kwamba Serikali yetu haiwezi kufungua viwanda isipokuwa itaweka mazingira mazuri ya sekta binafsi kwa ajili ya kufungua viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuongeza thamani katika mazao hayo yanayozalishwa katika jimbo la Peramiho.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa *SIDO* wanafanya kazi nzuri sana ya kukopesha wajasiriamali na hivi karibuni wamekopesha wajasiriamali zaidi ya 300 wilayani Mpwapwa. Je, Serikali ina mpango kuwaongezea uwezo fedha *SIDO* ili waweze kukopesha wajasiriamali wengi zaidi katika nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubalina naye kwamba taasisi ya SIDO inafanya kazi kubwa

sana katika nchi yetu kutoa mikopo na napenda kumhakikishia kwamba tutaendelea kuhamasisha na kuwaelekeza SIDO waendelee kufanya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la bajeti kubwa kwa upande wa *SIDO* suala hili limetokea tena wakati wa bajeti ya Wizara yangu na tulisema kwamba tumejitahidi kadri ya uwezo wetu angalau mwaka huu wa fedha kuwaongezea *SIDO* mpaka shilingi bilioni 7 kwa ajili ya kufanya hilo tunakiri Wizara kwamba fedha hiyo haitoshi lakini kadri bajeti ya Serikali itakapokuwa inaongezeka tutakuwa tunaomba *SIDO* waongezewe fedha ili waweze kutoa mikopo kwa wajasiriamali wengi zaidi katika jimbo lake na katika majimbo yote Tanzania.

Na. 44

**Soko kwa Ajili ya Matunda**

**MHE. MOHAMED ALI SAIDI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakulima wengi wanalima matunda ya aina mbalimbali kwa ajili ya biashara kwa lengo la kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini lakini hawana soko kwa ajili ya matunda hayo na matokeo yanaharibika ovyo na kuwapatia wakulima hasara kubwa na kuendelea kubaki kwenye umaskini.

Je, kwa nini Serikali isijenge viwanda vya kutengeneza juisi kwenye kila wilaya Tanzania ili kuondoa kabisa tatizo la soko kwa matunda?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Saidi, Mbunge wa Mgogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa maendeleo endelevu katika uzalishaji wa matunda yanahitaji uongezaji wa thamani ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda vya Usindikaji Wizara yangu imetoa kipaumbele katika suala la usindikaji kama inavyoainishwa katika mikakati ya uendelezaji viwanda na kukuza mauzo nje. Aidha, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mkakati Unganishi wa Biashara wa Tanzania (Tanzania *Trade Integrated Strategy*) ambapo usindikaji na ubora vimepewa kipaumbele na maabara kadhaa zitajengwa katika viango vya kimataifa ili kuwawezesha wazalishaji wa vyakula mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wasindikaji wa matunda, kuzalisha na kusindika kulingana na viwango vya ubora katika soko la ndani na nje. Hii itawezesha wazalishaji wengi zaidi kuwekeza katika viwanda vya kusindika matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi na uendelezaji wa viwanda, kama unavyofahamu, Serikali imejiondoa katika jukumu hilo na kuiachia sekta binafsi. Kazi ya Serikali ni kuweka mazingira bora ya kuvutia sekta binafsi kuweza kuwekeza katika uanzishaji wa viwanda hivyo. Kwa mfno, kutokana na juhudi za Serikali za kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya kusindika matunda, baadhi ya viwanda vifuatavyo vimeanzishwa.

1. Unnat *Fruit Processing* cha Morogoro;
2. Fruit *Kin-Concentrate Ltd* cha Kibaha;
3. Catewako *Ltd* cha Dodoma; na
4. Dawshi *Industries Ltd* cha Arusha.

Nawahamasisha wananchi wakishirikiana na Halmashauri za Wilaya na kwa kushirikiana na Mabaraza ya Uwekezaji ya Mikoa kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo, ikiwemo miradi ya ujenzi wa viwanda vya kutengeneza juisi, ili viwanda hivyo view ni soko la matunda mbalimbali yanayozalishwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuisaidia Serikali katika zoezi hili la uhamasishaji katika majimbo na mikoa yao.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa niulieze swali moja la nyongeza kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga soko la kimataifa pale Segera na mipango yote ilikwisha kamilika na hadi sasa imeshachukua muda mrefu hatimaye mpango huo hauonekani kama kuna maendeleo. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuharakisha na kuhakikisha soko hilo linafanya kazi na hatimaye matunda yaliyokuwepo katika maeneo yale yaweze kuwa *processed* kama ulivyojibu katika swali la msingi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba soko la kimataifa la Segera limekuwa tatizo la muda na kumekuwepo na jitihada mbalimbali za miaka mingi kujaribu kulijenga hili na katika majibu tuliyotoa ya bajeti ya Wizara yangu mwaka huu wa fedha tulisema kabisa kwamba tutalifuatilia napenda nimhakikishie nimuombe Mheshimiwa Rished Abdallah kwa kweli tushirikiane sote kuanzisha soko la kimataifa sio kitud ambacho kinaweza kikasemwa leo kesho kikaanzishwa lakini napenda nimhakikishie kwamba nia iko pale pale na mchakatao unaendelea namuomba kabisa kwamba hata tukitoka hapa leo tuweze kuonana niweze kumueleza hatua moja baada ya nyingine ambayo tumeweza kufanya. Sasa hivi sina majibu ya kina ya kumpa hapa lakini nia ya Serikali iko pale pale naomba ushirikiano wake.

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuwa mbali na viwanda vya kusindika haya mazao ziko njia zingine za kuweza kuhifadhi mazao ambayo yakachukua muda mrefu yakatumika wakati ambao sio wa

msimu. Je Wizara yako imechukua juhudi gani za kuwafundisha wananchi au wakulima njia hizo na ili mazao yasiharibike na yaweze kutumika wakati ambao sio wa msimu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubalina naye kabisa kwamba upo umuhimu wa kuweza kuhifadhi mazao ili yaweze kukaa muda mrefu yasiharibike na hili kumuongezea mwananchi faida anapouza yale mazao. Na nimwambie tu kwamba mafunzo yaliyokuwa yanatolewa siku zote na *SIDO* wako jamaa zetu Acamatec ambao wako chini ya Wizara yangu ambao wanatoa mafunzo mbalimbali katika mikoa na wilaya mbalimbali.

Mimi ninachomwomba ni kwamba endapo anaona kwamba anahitaji mafunzo yafanyike katika eneo ambalo analiona kwamba wananchi hawana ufahamu huo awasiliane na sisi tunakiri kwamba hatuna uwezo wa kuwafunza Tanzania nzima wakafahamu kwa kipindi kifupi lakini jitihada zinaendelea na napenda kukiri kwamba pale ambapo tunakuwa na nyezo za kufanya hivyo tutaendelea kufanya hivyo na tunaomba ushirikiano kama nilivyosema kwenye swali langu la mwanzo.

Na. 45

**Tanzania na Medali za Michezo ya *Olympic* Mwaka 2008**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni tumeshuhudia mashindano ya *Olympic* yaliyofanyika huko China na nchi yetu pia ilishiriki katika baadhi ya michezo kwenye mashindano hayo.

Je, nchi yetu ilifanikiwa kupata medali ngapi kwenye mashindano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, hivi karibuni nchi yetu ilishiriki katika mashindano ya *Olympic* ya Dunia yaliyofanyika Beijing, China ambapo jumla ya nchi 205 zilishiriki.

Nchi yetu ilishiriki katika michezo ya riadha na kuogelea. Riadha walishiriki wachezji 10 na mchezo wa kuogelea walishiriki wachezji wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya nchi 205 zilizoshiriki mashindano hayo ni nchi 88 tu zilizopata medali mbalimbali, wakati jumla y a nchi 117, Tanzania ikiwa miongoni mwaka nchi hizo hazikupata medali hata moja.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza Mheshimiwa Waziri anaweza kueleza Bunge hili mmejifunza nini na mmejiandaa vipi kwa mashindano yajayo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kule kushirikiana kwenyewe kwenye mashindano ya *Olympic* tumejifunza, wachezaji wetu waliokwenda wakapata uzoefu na nchi nao imepata uzoefu wa namna mashindano mbalimbali wenzetu wanavyojiandaa.

Lakini lingine ambalo tumejifunza ni kwamba mashindano haya ya *Olympic* tumegundua hizi nchi 205 ambazo zimekwenda kushiriki kule washiriki waliokwenda wanatakiwa washiriki wa michezo mingi, sisi tulipeleka michezo miwili tu riadha na kuogelea, lakini wenzetu wengine wengi wamepeleka zaidi ya michezo 20 kubeba vyuma, kutupa mishale na michezo mingine. Hivyo tumejifunza kwamba lazima tujifunze na michezo ili tuweze kupata medali nyingi zaidi. Lakini kubwa ambalo tumejifunza ni kwamba tuwe na msingi imara wa kuwekeza kwenye michezo. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuwekeze kwenye michezo mtupatie bajeti angalau nono kidogo ili tuweze kupata vipaji na kuviendeleza vipaji vyetu, ili tuweze kupata walimu wa kutosha na kuwa na academia za kutosha na wataalam katika kufunza wachezaji wetu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, katika michezo ya *Olympic* ya hivi karibuni ambayo wana michezo wetu walishiriki, baadhi ya wanamichezo hodari walipoteza medali zao baada ya kugudulika kwamba walitumia madawa ya kuongeza nguvu.

Hivi karibuni hapa nchini baadhi ya viongozi wa michezo walisikika wakisema kwamba kabla ya mechi ya watani wawili wa jadi hapa nchini Simba na Yanga ni lazima wana michezo wapimwe kujua kwamba…

**NAIBU SPIKA:** Usiende nje ya swali hii ni michezo ya kule, sasa ya hapa tena yameingiaje hebu uliza, China tunazungumzia Beijing ya hapa sio yenyewe uliza ya huko Beijing ndiyo swali la msingi uliza basi tukusikilize lakini uwe *relevant.*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika nilitaka kujua kwamba je, suala hili la matumizi ya madawa ya kuongeza nguvu kama ilivyotokea kule katika michezo ya Beijing hapa Tanzania na kama lipo Serikali inalichukulia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, alichozungumza ni kwamba ni kweli katika mashindano ya kimataifa kuna antoping kampeni ambayo inafanyika dunia nzima kwamba wachezaji wasitumie madawa ya kulevya na hilo linafanyika katika mashindano lazima kabla ya kucheza wachezaji wanapimwa na sisi Tanzania pia tuna Kamati maalum inayoshughulika na hayo na semina mbalimbali zinafanywa na tunao wataalam lakini katika ligi zetu hatujaanza kutumia hiyo staili. Pale ambapo tutakapogundua kwa sababu mpaka sasa hivi hatuna ushahidi basi tutafanya hivi.

Na. 46

**Mabadiliko yanayofanywa na TBC Katika Vipindi vyake**

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, *TBC* inafanya kazi nzuri sana ya kuwahabarisha wananchi na kutangaza nchi yetu ndani na nje:-

Je, ni sababu zipi zilifanya *TBC* kufuta kile kianzio cha mpiga mbiu akiwa juu ya mlima Kilimanjaro katika vipindi vya Taarifa za habari *TBC1*?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia utendaji kazi wa chombo hiki cha umma. Aidha, ni kweli kwamba *TBC* imefuta kianzio cha mpiga mbiu akiwa juu ya mlima Kilimanjaro katika vipindi vya Taarifa ya habari za *TBC* 1. Hatua ya kufuta kianzio hicho ni sehemu ya mchakato wa *TBC* wa kuboresha vipindi vyake vinavyorushwa hewani kupitia *TBC* 1 na *TBC* Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa kabla ya mabadiliko hayo ulibaini kuwa baadhi ya vipindi vya *TBC1* na *TBC* Taifa vilikuwa havina mvuto kwa watazamaji na wasikilizaji wake. Baadhi ya vitu ambavyo vilionekana kukosa mvuto ni kianzio cha Taarifa ya Habari ya *TBC1* pamoja na kuwa na maudhui ya kitaifa. Hata hivyo mabadiliko yaliyofanywa yamezingatia uwepo wa msisimko na mwonekano unaowavutia watazamaji na unaostahili kwa taarifa za habari za mtindo wa kisasa wenye ushindani mkubwa wa ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utafiti uliofanywa hivi karibuni na Shirika la Utafiti la *STEADMAN* lenye makao yake makuu nchi Kenya karibu na Shrika la Utafiti la *STEADMAN* lenye makao yake makuu nchini Kenya na kuwa Tawi hapa Tanzania shirika linalofuatilia wasikilizaji na watazamaji yaani wanao *monitor* limeonyesha kuwa,

Taarifa ya habari ya *TBC1* ndiyo inayowavutia watazamaji wengi hapa nchini na katika Afrika Mashariki.

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA:** Nashukuru kwa majibu ambayo nimeyapata pamoja na kwamba imeeleza kwamba kianzio kile hakikuwa na kivutio. Je, Serikali inaona ni sahihi kukwepa ukweli wa mila zetu kwa kuogopa ushindani kwa chombo hiki cha umma ambacho sio cha kibiashara?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Serikali haikwepi sisi kama Serikali na chombo chetu cha umma cha *TBC* kinaushindani katika dunaia hasa katika dunia hii ya utandawazi lazima tukubali kwamba chombo hiki pamoja kwamba ni cha umma lakini pia kinashindana ili kuvutia taarifa ya habari yake iwe nzuri zaidi na ndiyo maana utafiti unaendelea na sisi kama Serikali tumekubali kuendelea kutafiti na Waheshimiwa Wabunge tunawaombeni kama mtu ana mawazo anaushauri bado tunaendelea kuyapokea ili tuweze kuboresha zaidi chombo chetu ili kifanye kazi nzuri kwa faida ya Watanzania wote.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mimi ninakubaliana naye kuwa chombo chetu cha *TBC* kinafanya kazi nzuri sana kwa nchi yetu lakini napenda kumwuliza swali dogo la nyongeza. Je, pamoja na kazi hii nzuri lakini *TBC* inapotokea inaonyesha vitu ambavyo ni kinyume na mila na utamaduni wa nchi yetu kama ilivyoonyeshwa picha ya mwanamke aliyevua nguo pale katika *Sarenda Brigde* wananchi wote wakaona. Je, anasemaje juu ya jambo kama hili?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kimetokea juzi Sarenda Brigde ni tukio, na matukio yoyote yanapotokea vyombo vya habari vya aina yoyote sio lazima iwe *TBC* tu vinaonyesha ili public ili umma ujue kilichotokea na ndiyo ambacho kimetokea kwa chombo chetu. Na hali ile ni kitu ambacho kimetokea kwa dharura na lazima kionyeshwe kwa sababu wananchi wajue hali gani imetokea katika nchi yetu. Yaani ile ni ambayo imejitokeza kwa mpigo kwa wakati ule instant kwa hiyo isingetokea kwamba wasionyeshe kwa sababu ni chombo cha umma, walikuwa wanaonyesha ni chombo cha umma ili wa *public* ijue kwamba hali halisi ya tukio lenyewe ni hili, ingekuwa ni mechi ya mpira ingeonyeshwa watu wamevua nguo ingeonyesha ili hali halisi ijitokeze.

Na. 47

**Kituo cha Polisi Chwaka Kupatiwa Gari**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa ni takribani miaka 22 imepita tangu ilipoelezwa hapa Bungeni jinsi ya ukosefu wa gari katika kituo cha poloisi cha Chwaka; na kwa kuwa, katika jimbo la Chwaka kuna hoteli nyingi za kitalii na ongezeko kubwa la watu na kwamba ujambazi

hutokea katika mahoteli hayo na katika vituo vya mafuta; na kwa kuwa, gari hilo pia litahudumia na maeneo mengine kama kituo cha Dunga, Jimbo la Uzini na Koani:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa gari kwa ajili ya kituo hicho?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutokupatia gari kituo hicho ni sawa na kudumaza uchumi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vyote vya polisi hapa nchini kikiwemo cha Chwaka vinakuwa na vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari, pikipiki, simu za upepo, samani pamoja na majengo mazuri ya ofisi na makazi ya Askari. Hata hivyo nia hiyo nzuri ya Serikali haijaweza kufikiwa kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Chwaka, Dunga, Uzini, Koani, Unguja Ukuu na Fuoni kwa sasa yataendelea kuhudumiwa na gari la *OCD* kati ambapo Makao Makuu yake ni Mwera. Pale kunapotokea hitaji la ziada *OCD* kati huomba gari toka ofisi ya *RPC* Kusini Unguja. Aidha, nimeagiza gari lililopo Kituo cha Polisi Unguja Ukuu lifanyiwa matengenezo haraka ili liweze kutoa huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uhaba huo wa vitendea kazi na kwa kuelewa umuhimu wa maeneo hayo kwa uchumi wa Zanzibar, Jeshi la Polisi linaimarisha mbinu za ulinzi na usalama wa maeneo hayo.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa Jimbo la Chwaka lina nyumba nyingi za utalii na utalii ni moja katika uchumi wa Zanzibar na inawajibika kuwepo doria kwa askari ili kulinda usalama na uchumi ule.

(a) Je, kutokuleta gari kituo cha Chwaka huoni kwamba unadumiza Maendeleo ya Zanzibar ikiwa utalii ni moja katika uchumi wake?

(b) Kwa kuwa hivi sasa ni miaka 22 tunadai gari Kituo cha Chwaka na kuna maeneo ambayo yamepelekewa gari kwa ajili ya ukubwa watu tu. Je, Serikali ina kigugumizi gani kutueleza bayana kwamba haiwezi kuleta gari kituo cha Chwaka ili tusirejee suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimekubaliana na yeye kwamba mahoteli

yaliyokuwepo katika maeneo ya Chwaka ni muhimu katika Uchumi wa Zanzibar hilo halina mjadala.

Pia nimesema kwamba lipo gari ambalo linatumika na lipo gari ambalo ni bovu ambalo tunalifufua sasa liweze kufanyakazi hiyo. Lakini kwa kuzingatia umuhimu huo na kwa kuwa tuko katika polisi jamii na ulinzi shirikishi tumezungumza na watu wa mahoteli wenyewe ili pia waweze kutumia makampuni ya ulinzi binafsi ambayo tunatengeneza sera yake ambao wanafanyakazi ya ulinzi. *(Makofi)*

Lakini isichukuliwe kwamba ni azma ama nia ya Serikali kutojali ama kutolipa umuhimu suala la ulinzi katika maeneo ya Chwaka hasha tunakataa, isipokuwa ni tatizo ambalo lipo katika Tanzania nzima na Serikali inalifahamu hilo lakini kwa uhaba wa bajeti tuliyokuwa nao ndiyo maana tunasema kwamba tutakwenda hatua kwa hatua na hilo ningemwomba Mheshimiwa Mbunge aweze kutuvumilia.

Lakini kuhusu suala lake la pili ni kwamba Serikali haijakataa na haiwezi ikatoa jibu moja kwa moja kwamba haitapeleka gari kule mimi ninasema gari tutapeleka lakini tutapeleka kwa mujibu wa bajeti itavyokuwa inaruhusu kwa hiyo nia iko pale pale na azma iko pale pale. Lakini nilitaka nimwambie Mheshimiwa Yahya kwamba hili tatizo ambalo siyo la Chwaka peke yake ni tatizo la taifa zima. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH A. TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikumbuke kwamba hii ahadi ya kuleta magari mabovu kule Zanzibar imeshakuwa inachosha. Kunako kikao cha tano na cha 6 aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Aboud aliahidi kwamba atapeleka magari haya katika vituo mbalimbali vya polisi. Mheshimiwa Naibu Waziri atakumbuka ahadi moja ilikuwa ni kupeleka gari katika kituo cha Polisi Mazizini ambacho kinahudumia jimbo la Kiembe Samaki na Jimbo la Dimani sehemu ambazo zina madiko mengi ya wavuta bangi, wezi wa ng’ombe na sehemu nyingine kama hizo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ahadi hizi zitatekelezwa lini au bado na huku atatafuta gari bovu atuletee?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hafidh si azma ya Serikali wala siyo nia ya Serikali kuwapelekea wananchi wake magari mabovu. Naona kidogo jinsi ulivyokuwa unauuliza swali lako kuna jazba na kuna hasira. Lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa wewe mwenyewe unafahamu bajeti tunaitengeneza hapa uwezo wa taifa unajua na hakuna nia kusema kwamba Serikali inafanya kwa makusudi. Isipokuwa tunakwenda kwa hali ilivyo na hali tuliyokuwa nayo. Ndiyo maana ninasema kwamba Mheshimiwa Hafidh tuvumilie bajeti kweli ya mwaka huu tayari tumeanza kutumia lakini jinsi inavyokuja ndivyo tutakavyokuwa tunafanya mpangilio wa magari.

Kwa hiyo, ahadi ambayo Serikali imejiweka itatimiza na pale ambapo amekawia kutimiza siyo kwa sababu hakuna nia ya kutimiza isipokuwa ni kwa sababu ya uwezo tulionao kibajeti. (*Makofi*)

Na. 48

## Wafungwa Waliohukumiwa Kunyongwa

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, wapo wafungwa waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa bado wanasubiri adhabu hiyo na hata wengine kubembeleza wanyongwe baada ya kukaa muda mrefu:-

(a) Je, ni wafungwa wangapi mpaka sasa bado wanasubiri kunyongwa?

(b) Je, wafungwa wa aina hiyo waliokaa kwa muda mrefu sana gerezani wamekaa miaka mingapi?

(c) Kwa mara ya mwisho hukumu ya kifo imetolewa lini na mtu wa mwisho kunyongwa alinyongwa mwaka gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napeda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 1 Oktoba, 2008 idadi ya wafungwa waliohukumiwa hukumu ya kifo ambao bado wanashikiliwa katika Magereza mbalimbali nchini ni 286. Kati ya hao, idadi ya wafungwa wanaume ni 277 na wafungwa wanawake ni 9.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mfungwa wa kunyongwa aliyekaa gerezani kwa muda mrefu ni miaka 22 (tangu 1986).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, amri ya kutekeleza adhabu ya kifo kwa mara ya mwisho ilitolewa mwaka, 1994.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika ninashukuru kwa majibu, kwanza mazuri na mafupi.

(a) Je, fedha zinazotumika katika kuwatunza hawa waliohukumiwa kifo zinatoka wapi wakati hawastahili kuendelea kuishi.

Je, si ubadhilifu? Hilo la kwanza. (*Makofi*)

(b)Kwa kuwa wanapokuwa wamehukumiwa kunyongwa hiyo huwa ni haki yao kisheria hapa Duniani na hata mbinguni na kwa kuwa kitendo cha Mheshimiwa Rais kutokusaini mapema ili kusudi waweze kunyongwa huwa ni kuwanyima haki yao ya msingi maana wanakaa gerezani kwa mateso, mashaka na hofu na kila siku wanateseka kisaikolojia.

Je, Mheshimiwa Rais hawezi akaona huruma hata kidogo akahakikisha anasaini mapema ili kusudi wanyongwe na wafe? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama anavyofahamu suala la kunyonga Duniani wala siyo Tanzania peka yake ni suala tete na nchi nyingi wanazo sheria za kunyonga lakini utaratibu wenyewe ulivyo maana yake baada ya mahakama kusema kwamba huyu mtu kufuatana na sheria hii kwa kosa alilofanya basi uamuzi ni kunyongwa, lakini pote unakuta kwamba lazima iende kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siwezi kumjibia Mheshimiwa Rais, hiyo ni moja, lakini kama anavyojua Mheshimiwa Ponsiano Nyami upo mjadala mpana sasa hivi kuhusu hili suala la kunyongwa maana ziko nchi ambazo wameondokana na sheria hii, ziko nchi ambazo bado wanazo sheria hii na mjadala hata hapa Tanzania wanaharakati wapo ni wengi wanalizungumzia, watu wanyongwe au wasinyongwe.

Sasa mimi niseme tu kwamba sheria tuliyonayo bado ipo lakini suala la kumtoa roho sidhani kwamba ni suala la ubadhilifu katika pesa za Taifa maana yake huwezi kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaomba tu kwamba inapokuja katika kumtoa mtu roho kwa kweli si jambo jepesi na ninadhani hata Mheshimiwa Rais anaona uzito katika hilo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kama siyo jambo jepesi tunaendelea na maswali mengine. (*Makofi*)

Na. 49

**Gharama za Kuunganisha Umeme**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, uhaba wa nishati ya umeme vijijini ni tatizo moja kubwa lakini tatizo la gharama ya zaidi ya shilingi milioni moja ya kuunganishiwa umeme kwenye nyumba ni tatizo jingine.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuangalia upya gharama hizo za *TANESCO* ili wananchi wengi wamudu kuunganishiwa umeme vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uhaba wa nishati ya umeme vijijini imekuwa ni tatizo kubwa hasa katika maeneo yanayokua kwa haraka kiuchumi na yale yanayohitaji nishati hiyo kuchochea maendeleo ya maeneo hayo. Serikali kwa kuzingatia hayo imeanzisha Wakala wa Nishati vijijini yenye lengo la kupeleka umeme vijiji waliko asilimia kubwa ya Watanzania, na kwa mwaka huu wa fedha wa 2008/2009 tayari Serikali imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli pia kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi sehemu mbalimbali za nchi kuhusiana na gharama kubwa ya kuunganishiwa nishati hiyo ya umeme. Aidha, katika utekelezaji wa majukumu yetu na haswa kwenye kukagua miradi ya umeme vijijini, tumeshuhudia jinsi huduma ya umeme ikiwafikia wananchi na wanapokuwa tayari kuitumia kwa kubuni miradi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa shughuli zao za kila siku jinsi maisha yao yanavyobadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanda kwa gharama za kuunganisha umeme kunatokana na kupanda kwa gharama za vifaa vya kuunganisha umeme zikiwemo nguzo, nyaya, *transformer*, mita za umeme na vifaa vingine vinavyotumika katika kuunganisha umeme. Kupanda kwa vifaa hivi kunatokana na kupanda kwa kiwango kikubwa kwa malighafi muhimu zinazotumika kwenye kiwango kikubwa kwa malighafi muhimu zinazotumika kwenye vifaa hivyo, k.m. shaba. Hata hivyo, Serikali imeyaona matatizo hayo na tayari imeanza kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikail kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* imechukua hatua zifuatazo kupunguza tatizo la gharama kubwa ya kuunganishia wateja wa *TANESCO* umeme:-

1.Kuhakikisha kuwa ujenzi wa miundombinu ya umeme inasogezwa karibu na nyumba za wateja ili kuwapunguzia gharama za uunganishwaji.

2.Kulipa kwa awamu: Serikali kupitia *TANESCO* imetoa kibali kwa kila mteja anayehitaji kulipia gharama za kuunganishiwa umeme kwa awamu, kuingia mkataba wa kulipia gharama hizo kwa awamu tatu ndani ya miezi mitatu. Mteja atajengea *service line* baada ya kulipa gharama zote.

3.Ili kumuondolea mteja gharama za wiring na gharama hizo kutumika katika kuunganishiwa umeme, Serikali imeanzisha matumizi ya chombo kiitwacho *Ready*

*Board*, ambapo kifaa hicho kinafungwa kwenye nyumba ambayo haijafanyiwa wiring *TANESCO* huweza kuunganisha umeme kwenye nyumba hiyo kupitia kifaa hicho. Nyumba iliyofungwa kifaa hicho haihitaji kufungiwa *main switch* wala *circuit breaker* na kinatimiza masharti yote ya usalama. *Ready board* inafaa katika kuunganisha umeme nyumba aina zote zikiwemo za nyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya Wizara yangu kwamba Sheria mpya ya umeme iliyopitishwa na Bunge lako mapema mwaka huu, italeta hamasa ya uwekezaji wa sekta binafsi kwenye maeneo ya sekta ya umeme yaliyokusudiwa na Sheria hiyo wakati wa kuipitisha. Kwa maana hiyo, ushiriki wa sekta binafsi kwenye masuala ya uzalishaji wa umeme (*generation*) na usambazaji wa umeme (*distribution*) ambao kwa sasa unafanywa na *TANESCO* tu, unaweza kupunguza gharama na kuleta manufaa kwa watumiaji wote, kwa maana ya matokeo ya ushindani.

Wizara yangu inafanya kazi kwa karibu na wadau wote wa sekta ya umeme na hivyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Umbulla na Watanzania kwa ujumla kwamba kwa kufahamu jinsi suala hili lianvyokwaza kukua kwa matumizi ya huduma ya umeme Wizara na *TANESCO* kwa kushirikiana kwa karibu na EWURA inafanya kila linalowezekana ili huduma hii iwafikie wananchi kwa gharama nafuu kadri itakavyowezekana.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nichukue nafasi kwa kweli kumpongeza sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kina. Ni matumaini ya Watanzania wamekuwa na imani na Wizara ya Nishati na Madini na wamesikia maelezo haya. Sasa naomba kuuliza maswali madogo tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kuwa kuwepo umeme kwenye vijiji vyetu ni kigezo cha kuhamasisha maendeleo na kuondoa umaskini kwa jamii zetu na hata biashara zao ndogo ndogo kuweza kushamiri. Je, kwa nini Serikali kwa maana ya *TANESCO* isiandae utaratibu wa kukopesha vijiji hata kama vitaanza na vijiji vichache vichache lakini iweze kuwakopesha vijiji kwa dhamana ya Halmashauri zao kuliko utaratibu aliyopendekeza Naibu Waziri wa kuwakopesha kwa awamu na kuja kulipa mwisho ni ambapo ndio watafikiriwa kupewa *service line*?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kama vijiji vingekuwa vimekopeshwa umeme kwa utaratibu niliopendekeza. Je, Serikali haioni kwamba hii itahamasisha hata wananchi kujenga nyumba bora kuliko ambavyo sasa hivi Wizara imefikiria hata kuweka umeme kwenye nyumba za nyasi? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kukopesha mtu mmoja mmoja na kusema kweli kama ingewezekana hakika Serikali ingependa kufanya hivyo, kama nilivyoeleza sisi tunatambua kwa karibu jinsi ambavyo umeme unapoelekea vijijini mabadiliko yanaonekana moja kwa moja haswa pale ambapo wanakijiji wanapokea kufika kule umeme na wanabuni miradi ambayo inaongeza ufanisi wa maisha yao na kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli hilo jambo tumeliona, lakini kwa sasa ambapo hatujakamilisha kwa ukamilifu haswa kuunganisha miradi haswa malengo haya ya kuweka uzalishaji wetu wa umeme uwe mkubwa zaidi nadhani inakuwa vigumu kuanza kuingia kwenye *stage* ya tatu ya matumizi ya umeme ambayo ni *distribution* hali ya kwamba suala la uzalishaji *generation* bado haijafikiwa kwenye malengo ya Kitaifa yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa kulipa kwa awamu tumeenda huko vijijini tumeenda Ludewa, tumeenda Kanda ya Ziwa na kusema kweli tumeongea na wananchi na wameupokea vizuri na unaonekana unaleta unafuu kidogo kuliko ule wa kuunganisha wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kukopesha vijiji kwa maana hiyo pia ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba ni sehemu ya wakala wa nishati vijijini *REA* kupokea miradi iliyobuniwa na wanavijiji na kuwasaidia kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo kama vijiji vinaweza kubuni matumizi ya miradi ambayo itahitaji umeme au kuzalisha umeme wao wenyewe, nina hakika kwamba *REA* inaweza ikawasaida na kwa maana hiyo umeme utafika kwa wanakijiji kwa namna ambayo ni nafuu zaidi ikiwa imeibuliwa humo humo ndani mwao.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *TANESCO* iliuza kiwanda chake cha kuzalisha nguzo kilichokuwepo Mbeya na badala yake kununua nguzo nje ya nchi na kwa kuwa, *TANESCO* pamoja na *NDC* zimeuza hisa zake za Tanzania *cable* Dar es Salaam na Kiwanda cha *Transformer* Arusha kwa nchi ya Kenya.

Je, Serikali haioni kitendo hiki kimesababisha *TANESCO* kuwa na hali ngumu sana ya kuupeleka umeme vijijini hapa nchini?

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kurejesha …………………

**NAIBU SPIKA:** Swali moja.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** *Ok.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ania Chaurembo, ni swali moja. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu, wengine ni swali moja tu, wa kwanza ndio ana maswali mawili

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *Transformer* na masuala ya kiwanda cha kutengeneza nguzo hizi za umeme, kusema kweli ziliuzwa katika utaratibu wa ubinafsishaji ambao ni utaratibu ambao uchumi wetu umekuwa unaenda kwa pamoja na unaeleweka kwa miaka yote hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sasa hivi naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kuzingatia hali hii ya gharama za kuunganisha umeme ambao umepanda ghafla katika miaka hii miwili iliyopita tunaelekezana sisi Wizara na *TANESCO* na EWURA na wadau wote katika sekta hii ya umeme kuanza kufanya mikakati ya makusudi ya kuangalia namna ambavyo tunaweza tukahakikisha suala la kuunganisha umeme unapungua haswa katika masuala kama haya ya nguzo tunataka *TANESCO* watuambie kama kuna maeneo mengine ambapo nguzo zinaweza zikapatikana kwa bei ya nafuu zaidi. Lakini pamoja na hiyo tunaihimiza sekta binafsi kwa sababau sheria imeruhusu iingie katika biashara ya kuunganisha umeme katika *stage* ya tatu ya *distribution* ili labda ule ushindani utaleta unafuu katika gharama za kuungisha umeme.

Na. 50

**Kuliwezesha Shirika la Mafuta *TPDC***

**MHE. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mfumuko mkubwa wa bei za biashara mbalimbali umesababishwa na ongezeko la bei ya mafuta:-

(a) Je, kwa nini mpaka sasa Shirika la *TPDC* halijawezeshwa ili lishiriki katika kuagiza mafuta kama ilivyoamuliwa na Bunge?
(b) Je, ni lini *TPDC* wataanza kupewa gawio kutokana na biashara ya gesi ili waweze kujiendesha na kufikia malengo yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika mwenendo wa bei ya mafuta humu nchini zinategemea moja kwa moja mwenendo wa bei za mafuta kwenye masoko ya kimataifa. Mara nyingi sisi kama uchumi wa nchi changa, hatuna uwezo wowote na kusababisha bei hizo kushuka au kupanda, na kwa maana hiyo sababu zinazopelekea bei za bidhaa za mafuta kupanda au kushuka ziko nje kabisa ya mikono yetu. Ni kweli pia kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kupanda kwa bei za mafuta kuna athari ya moja kwa moja kwenye bei za bidhaa na huduma mbalimbali zingine.

Hapa nchini, bei za mafuta zimekuwa zikipanda mara kwa mara kama matokeo ya kupanda huko kwa bei katika soko la Dunia, kampunu za mafuta kutumia gharama kubwa kuagiza bidhaa za mafuta kwa sababu ya kuagiza mafuta kidogo kidogo, upungufu na udhaifu wa vyombo vya kupakulia mafuta bandarini na udanganyifu na upangaji wa bei kwa baadhi ya kampunu ya mafuta.

Katika sababu nilizozitaja hapo awali sababu ya kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia ipo nje ya uwezo wa Serikali lakini zipo sababu zingine na Serikali imeshaanza kuzifanyia kazi. Uundwaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*), kupitishwa kwa Sheria mpya ya mafuta (*Petroleum Act, 2008*), uboreshaji wa miundombinu ya kupakuliwa mafuta, uandaaji wa utaratibu wa kuagiza mafuta kwa jumla na uimarishaji wa mamlaka ya kuweka ushindani sahihi kwenye biashara (*Fair Competition Commission (FCC*), zote ni miongoni mwa jitihada za makusudi za kukabiliana na tatizo la bei za mafuta na athari zake kwenye uchumi jumla. Jitihada zingine ni Shirika la Maendeleo ya Mafuta ya Petroli (*TPDC*) kuruhusiwa kuagiza mafuta ili kuleta ushindani katika biashara ya mafuta. Shirika pia limeruhusiwa kuanzisha na kuendesha ghala la mafuta ya akiba ya dharura (*Strategic Stock*).

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo haya yanalenga kuweka bayana kwamba Wizara yetu inatambua kina cha tatizo la bei za mafuta na umuhimu wa ushiriki wa *TPDC* kwenye suala la kuagiza mafuta na limeanza kuweka mazingira haya kama nilivyoeleza yatakayowezesha utekelezaji wenye ufanisi wa ugizwaji wa mafuta kwa pamoja wa jumla wa *TPDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayoiwezesha *TPDC* kushiriki kwenye mafuta imepitishwa na Bunge lako Tukufu, Aprili, 2008 kama nilivyoeleza hapa awali, hivi sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuiwezesha *TPDC* kushiriki katika biashara ya mafuta ikiwamo kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kimsingi imesharidhia kuipatia *TPDC* gawio linalotokana na mapato ya matumizi ya Gesi Asilia. Pendekezo hilo pia limeshawasilishwa humu ndani Bungeni na kuridhiwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu tarehe 8 – 9/07/2008. Wizara imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye mapendekezo ya kiasi cha asilimia ya mapato ya gesi kitakachobaki *TPDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ni vyema nikatumia nafasi hii kueleza kwamba matumizi halisi ya gesi ikilinganishwa na uwezo wa kutumuia (*potential use*) bado ni mdogo sana.

Wizara yangu mara kwa mara inapokea wawekezaji wanaokusudia kuwekeza (*interested investors*) katika shughuli za uzalishaji bidhaa zitokanazo na gesi asilia zikiongezeka, gawio la mapato yatokanayo na gesi asilimia nao litaongezeka maradufu.

Ni matarajio yetu kwamba Sheria ya matumizi ya gesi asilia inayofanyiwa kazi hivi sasa na ambayo inatarajiwa kuwasilishwa humu kwenye mkutano ujao wa Bunge itajielekeza kwenye masuala ya kujenga mazingira yanayovutia uwekezaji wa viwanda vya matumizi ya gesi asilia.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pia nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, ikiwa ni tangu mwezi Aprili tumeweza kupitisha hapa Bungeni kuiwezesha au kuliwezesha Shirika letu la *TPDC* kuweza kuagiza mafuta na mwezi Julai, pia kuliongeza kuliongezea Shirika letu la *TPDC* pesa kutokana na gawio la gasi lakini hadi hivi sasa hilo halijafanyika. Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha ucheleweshaji huo?

La pili, je, Serikali sasa hivi kwa hatua ya dharura na ya haraka na kwa unyeti wa hili suala katika kuinusuru nchi yetu iko tayari basi kuweza kuliwezesha hili Shirika la *TPDC* ili liweze kufanya hizo kazi mbili, kuagiza mafuta na pia katika kupata gawio la pesa inayotokana na gesi ili liweze kujiendeleza na taarifa zilizopo kwamba kuna shughuli zinazofanyika au njama zinazofanyika na makampuni binafsi katika kuchelewesha hii shughuli ili *TPDC* isiweze kufanya hii kazi, lakini pamoja na ile kazi muhimu ya kusambaza gesi au kufanya biashara ya gesi ambayo ilikuwa ya kusambaza magesi majumbani Shirika letu la *TPDC* hadi sasa hivi halijaweza kufanya hivyo. Je, Serikali iko tayari katika kuliwezesha hilo Shirika la *TPDC* katika hali ya dharura kwa hivi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu yawe mafupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Fuya Kimbita, kama ifutavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inayowezesha *TPDC* kupata *retention* na masuala kama alivyoeleza Mbunge, kama nilivyosema tunapitisha Aprili mwaka huu kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina *hansard* ya Mheshimiwa Godwin Kimbita alikuwa ameuliza swali hili hili na Serikali tulimwahidi kwamba tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema waraka wa Baraza la Mawaziri tayari umeandaliwa kwa masuala yote mawili na ninamwomba Mheshimiwa Fuya aelewe tu kwamba kwa sasa hivi masuala haya kwanza tumeandalia waraka wa Baraza la Mawaziri na linashughulikiwa ndani ya Serikali, lakini pia tunawasiliana na Wizara ya Fedha ili kukamilisha hatua hizi kujua ni *retention* ya kiasi gani na kwa kiwango gani itafanyika na kwa muda gani kulingana na uwezo wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la kusambaza gesi pia tumeshalijibu humu ndani kwamba *TPDC* inafanya kazi na inawasiliana na wawekezaji mbalimbali na hata tathmini hiyo ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya matumizi majumbani na kwenye magari na kadhalika kama *liquid natural gas*, tayari imeshafanyiwa tathmini na tuliwahi kusema kwamba mradi huo wote utagharamia kama dola milioni 35 hivi nakumbuka nilisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kusema kweli mradi huo ni mradi unaovutia kwa sababu ya uwezo mkubwa wa matumizi ya gesi Dar es Salaam na kwa maana kwamba wawekezaji wanalifanyia kazi, tunalifanyia kazi pamoja na *TPDC* kukamilisha masuala ya uwekezaji.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, muda hautoshi, si mnasema mnaendelea kulifanyia kazi, naomba muendelee kulifanyia kazi.

Na. 51

**Kuwapatia Huduma ya Maji Wakazi wa Magu**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kero ya maji katika Mji wa Magu imekuwa sugu kwa miaka mingi sasa, kwani kati ya watu 30,000 wanaoishi Magu Mjini ni watu 12,600 (asilimia 42) tu wanapata maji:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuwapatia maji wakazi wa Magu Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji wa Magu. Fedha zitatumika kununua mitambo miwili ya kusukuma maji, mabomba kwa ajili ya kukarabati sehemu ambazo mtandao umechakaa na kununua kufunga dira za maji kwa wateja. Hatua hii itakapokamilika inatarajiwa kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 42 za sasa hadi kufikia asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imepanga kufanya usanifu wa mradi wa maji utakaotosheleza mahitaji ya maji kwa muda mrefu. Usanifu wa mradi utafanyika katika mwaka huu wa fedha 2008/2009. Serikali inaendelea na mchakato wa kupata kampuni ya ushauri itakayofanya uchunguzi, kusanifu na kuandaa zabuni za kutekeleza mradi. Makampuni yanayoweza kufanya kazi hiyo yameorodheshwa baada ya kutathminiwa. Kibali kimeombwa Benki ya Dunia ili kukamilisha zoezi la kumpata Mhandisi Mshauri, chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka ya Mwanza. Kampuni hiyo ya ushauri pia itafanya kazi ya uchunguzi na usanifu wa miradi ya maji katika miji ya Nansio, Sengerema, Geita, Misungwi, Ngudu na Jiji la Mwanza. Ujenzi wa mradi utaanza mara tu baada ya kukamilika kwa usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magu iko katika Mkoa wa Mwanza, nachukua fursa ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Limbu kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mkutano wa Mawaziri wa Maji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) utafanyika Mwanza wiki ijayo tarehe 6 Novemba, 2008, mkutano huo utafunguliwa na Mheshimiwa Dr. Ally Mohamed Shein, Makamu wa Rais ambaye pia atazindua awamu ya kwanza ya ujenzi na ukarabati mkubwa wa mradi wa maji wa Jiji la Mwanza.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya kina na yana muelekeo wa uhakika, lakini pamoja na majibu hayo nina maswali madogo mawili.

La kwanza, Halmashauri nyingi hapa nchini zina tatizo la upungufu wa wataalam katika Idara ya Maji hasa wahandisi wa maji, je, Serikali haina kuna haja ya msingi ya kutupatia watalaam wa kutosha katika Wilaya ya Magu ambao tuna tatizo hilo kwa sasa hivi?

La pili, kwa kuwa Mheshimiwa amesema kwamba anakuja kuna mkutano wa maji katika Jiji la Mwanza na kwa kuwa, kuna maeneo mengi ambayo yako katika Wilaya ya Magu na husasani kama Kata ya Kiloleli, Kata ya Kalemela imekuwa na miradi mingi ya

*water schemes* na miradi hii haifanyi kazi. Sasa Mheshimiwa Waziri anaweza kutenga muda wake akaja akatembelea miradi hii ili atusaidie kupata ufumbuzi wa nini kifanyike ili iweze kutoa huduma kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dr. Chegeni, kama ifuatavyo.

Kwanza, ni kweli Halmashauri karibu zote zina uhaba mkubwa wa wataalam wa maji, tatizo hilo tunalifahamu na tunalifanyia kazi katika mpango wa maendeleo ya sekta ya maji ambao sehemu kubwa ya mpango huo itakuwa vile vile katika kuongezea uwezo wa wataalam wa maji ikiwa ni pamoja na upanuzi mkubwa wa chuo chetu cha maji.

Kuhusu suala la tatizo la Magu lenyewe basi nitakuwa tayari kufanya kazi na Mheshimiwa Mbunge, Dr. Limbu ili tutafute njia ya kupata mtaalam ambaye anaweza kuajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magu ili awasaidie katika masuala la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu miradi mingi katika Wilaya ya Magu ambayo haifanyi kazi, niseme tu Serikali kwa kweli imepeleka fedha nyingi sana katika Wilaya ya Magu.

Naomba zitumike vizuri tu, mwaka 2006/2007 tumepeleka shilingi milioni 211,806,000 kwa ajili ya miradi ya kuleta matokeo haraka, mwaka 2007/2008 tumepeleka shilingi milioni 130,681,000, mwaka 2008/2009 tumetenga kwa ajili ya Wilaya ya Magu shilingi milioni 674,966,000 ni fedha nyingi matumizi yake ndio inabidi yasimamiwe vizuri.

Pamoja na kutatua haya matatizo ambayo ameyazungumza, lakini nadhani tatizo kubwa ni kukosa wataalam na tunafanya kazi na Halmashauri ya Wilaya ya Magu ili kutatua tatizo hili, ili fedha hizi za Serikali na za wananchi zitumike ipasavyo. (*Makofi*)

Na. 52

**Mradi wa Umwagiliaji wa Titye**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, mradi wa Umwagiliaji Kasulu una miaka 28 ukisuasua na kufanya kazi chini ya kiwango; na kwa kuwa ni wazi Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu haiwezi kukamilisha mradi kutokana na ukosefu wa wataalamu wa umwagiliaji:-

(a)Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kukamilisha mradi huo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isipeleke wataalamu wa Umwagiliaji wa "*re-design*" mradi huo ambao unasadikiwa kuwa ulikosewa, ili kuondoa adha ya mafuriko mashambani wakati wa masika?

(c)Je, Serikali inaahidi nini katika kukamilisha mradi huo mapema?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijashindwa kukamilisha ujenzi wa mradi wa Titye.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Wataalamu wa Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Tabora na wale wa Wilaya tayari walifanya upimaji na usanifu wa Bonde lote.

Gharama za ujenzi zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 810. Pamoja na mambo mengine usanifu umezingatia suala la mafuriko wakati wa masika.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi milioni 200 ili kuanza utekelezaji wa skimu hii kwa awamu. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya eneo lililobaki. Halmashauri ya Wilaya inashauriwa kuendelea kuuweka mradi huu katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ili kupata fedha zaidi za utekelezaji.

Wataalamu wa Kanda ya Umwagiliaji Tabora watashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ili kuhakikisha mradi huu unaombewa fedha za ziada kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji wa Wilaya (*District Irrigation Development Fund*).

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mafupi na mazuri. Naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana mkuu wa kanda ya umwagiliaji Tabora.

Baraka kwa kazi nzuri yeye na timu yake wanafanya kazi nzuri, nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa sababu mradi huu ni wa muda mrefu, miaka 28 sasa na ndio maana nasema Serikali pengine ilikuwa haikuweka nguvu yake.

Sasa maadam Mheshimiwa Waziri unasema wataalamu wa kanda ya umwagiliaji watashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, niseme tu kwamba pale Kasulu Ofisi ya Kilimo wameanza mchakato huu, sasa nikuombe wewe sasa kwa sababu hatuna wataalamu wa umwagiliaji uniahidi hapa na uwaahidi watu wa Kasulu kwa upande wako wataalamu hawa wataenda ku-*team up* na wataalam wa Kasulu lini ili mradi huu ambao umekaa miaka 28 uweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, kama ifuatavyo.

Kwanza napongea pongezi kwa niaba ya wataalamu wa kanda ya Tabora ya wataalamu wa umwagiliaji.

La pili, kuhusu ombi alilolitoa Wizara iko tayari kushirikiana na halmashauri pale ambapo halmashauri itakuwa tayari lakini kwa sababu inahitaji msukumo wa haraka naweza kusema hata jumatatu ikibidi wataalamu wetu wanaweza kuwa Kasulu.

Na. 53

**Vituo vya Kutunzia Wazee Nchini**

**MHE. MARIAM REUBEN KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika nchi yetu ipo mikoa yenye vituo vya kutunzia wazee ambao hawana ndugu wa kuwatunza:-

(a) Je, vituo hivyo vipo vingapi na vipo katika mikoa gani?

(b) Je, wazee wangapi wapo katika vituo hivyo kwa mchanganuo wa jinsia zao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napendakujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, swali lenye sehemu a na b kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na takwimu zilizoainishwa katika Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, nchi yetu yenye watu 33,500,000 inao wazee wapatao milioni 1.4 sawa na asilimia 4 ya watu wote.

Ifikapo mwak 2050 idadi hii itaongezeka kufikia milioni 8.3 sawa na asilimi kumi (10) ya watu wote nchini. Hata hivyo, ongezeko hilo ni changamoto kwa Serikali kwa sababu itawajibika kuwa na rasilimali za kutosha katika kuhakikisha wazee hawa wanatunzwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b).

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini kuna vituo 40 vya kutunzia wazee kati ya hivyo 17 vinasimamiwa na Serikali na 23 vinaendeshwa na wakala wa hiari:-

- Arusha (1)
- Dar es Salaam (3)
- Kagera (2)
- Kigoma (1)
- Kilimanjaro (1)
- Lindi (4)
- Mara (2)
- Morogoro (6)
- Mtwara (1)
- Ruvuma (2)
- Mwanza (1)
- Shinyanga (2)
- Singida (1)
- Tabora (5)
- Tanga (4)
- Dodoma (2)
- Pwani (1)
- Rukwa (1)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wazee waliopo katika vituo hivyo ni 2,253 kati yao wanawake ni 1,170 na wanaume ni 1,083. Mchanganuo kwa kila kituo kijinsia nitampatia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu orodha ni ndefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wazee hawatengwi na jamii zao na ili kupunguza hali za upweke, msongo wa mawazo na masononeko yanayotokana na kukaa katika makazi/taasisi *(Institutional care)* Serikali inakusudia kuzijengea uwezo familia na kuhamasisha jamii ili ziweze kuwatunza wazee ikiwa ni pamoja na kuwaandaa vijana kwa maisha ya uzeeni.

Hata hivyo, kama tulivyokuwa tunatoa taarifa katika Bunge lako Tukufu, wajibu wa kuwatunza wazee ni la familia na kuwapeleka kituoni iwe ni suluhisho la mwisho.

**MHE. MARIAM REUBEN KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri Kamati yetu ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilibahatika kutembelea baadhi ya vituo vilivyopo hapa nchini na kujionea hali ngumu sana waliyonayo wazee hawa katika vituo hivi, ikiwemo huduma za afya, chakula kibaya wanachokula pamoja na nyumba mbovu wanazoishi.

Je, Serikali iko tayari kuzungukia vituo hivi vyote kujionea hali halisi iliyopo ili waweze kuandaa utaratibu mzuri utakaowawezesha kukarabati hizi nyumba na kuwapatia huduma bora wazee hawa?

Kwa kuwa bado wazee wengine wako ndani ya vijiji vyetu ambao hawajabahatika kupelekwa katika vituo hivi na wanatunzwa na jamii ndani ya vijiji. Je, Serikali iko tayari kuandaa utaratibu kama ule wa kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili kuwatambua wazee hawa ili kupitia ruzuku za vijiji Serikali iongeze ruzuku waweze kutunzwa ndani ya vijij vyetu wakishirikiana na jamii?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba makambi mengi ya wazee ambao wanatunzwa huko yako katika hali mbaya lakini kama tulivyokuwa tunazungumza ni kwamba Wizara inatembelea na ninataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuzunguka na kuyakagua ili tuweze kuona hali ingawa tumeshaifanya.

Lakini tunasema kwamba tunakarabati makambi machache kwa sababu ya uwezo wa fedha tulizokuwa nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba wako baadhi ya wazee wako katika vijiji. Kama nilivyosema sisi tunavyoona ni kwamba jamii ni lazima ipewe maelekezo na itambue kwamba wajibu wa kuwatunza wazee hawa ambao wamefanya kazi nyingi katika Serikali hii ni wajibu wa jamii na familia zetu. Lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Serikali inakusudia kuwajengea uwezo familia na kuhamasisha jamii ili waweze kuwatunza wazee wakiwepo palepale kwenye maeneo yao kule vijijini. Suala la kuwapeleka katika vituo kwanza linawafanya wawe wanyonge, wanaona kama vile wametupwa. Kwa hiyo, mimi bado nasisitiza kwamba wakati tunaangalia ni jinsi gani tutawasaidia katika vijiji lakini bado ni wajibu wa kila familia kuona kwamba unawatunza wazee mpaka pale watakapomaliza maisha yao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha lakini leo nimejifunza kwamba maswali mengine yalikuwa marefu na majibu yake yakawa marefu hasa yale ya mwanzoni. Nadhani tuendelee na tabia yetu ya kuuliza maswali mafupi na kujibu kifupi kusudi tuwe *comfortable* kuwapa maswali ya nyongeza Wabunge wengi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni wa Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Naibu Waziri wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni Bwana Abdul Said Haji kutoka Zanzibar. Huyu alikuwa Mwakilishi wa Chake, nadhani kutoka mwaka 1980 – 1990. Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, Mbunge wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Naibu Waziri Wizara ya Maji na Ujenzi, Habari na Michezo. Karibu sana na tunakukukumbuka sana na ni ndugu yetu maarufu sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu ambao ni Bwana Hamad Abila Mkopa, Katibu wake Jimboni, Ndugu Seleman Chitanda ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Mkowe na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Ruangwa. Karibuni sana.

Yuko pia Mheshimiwa Ibrahim Issa Ndoro ambayo ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Ruangwa na Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya. Yuko Mama Adella Mbonye Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Ruangwa, pia yuko Mama Ruzuna Mkunga Katibu wa UWT Wilaya ya Ruangwa, pia Bwana Seleman Kaondo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana Wilaya ya Ruangwa. Yuko Ndugu Mohamed Ali Hassan, Katibu wa Vijana Wilaya ya Ruangwa. Naona Jeshi lote linalofaa wakati fulani fulani liko hapa, karibuni sana na tunaomba tu mumuenzi Mbunge wenu. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Eliatta Namdumpe Switi ambao ni Ndugu Aziz Amir, Ndugu Frank Ndanguzi na Ndugu Marcus Exaut naye ni Bwana Mdogo. Karibuni sana.

Wako wageni wa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi ambao ni Mheshimiwa Edwin Mgaya, Diwani wa Kata ya Mavanga, huyu tunapakana na mimi kule Tabora. Yuko na Mheshimiwa Diwani Lucy Haule, yeye ni Viti Maalum. Karibuni sana.

Pia tuna Washauri 35 wa wanafunzi kutoka vyuo vikuu wanaohudhuria mkutano wa *Dean of Students* hapa Dodoma wamefika kujionea na kujifunza uendeshaji wa shughuli za Bunge. Wanaongozwa na Mchungaji Ndelwa kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini. Naomba pale walipo wasimame. Ahsante sana Viongozi wa kesho tunafurahi kama mnapata nafasi ya kuja kutuona tunavyoendesha shughuli za Bunge. Ahsante sana. (*Makofi*)

Shughuli za kazi kwa siku ya leo yaani kazi za Kamati. Kwanza nina Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati tatu za Miundombinu, Fedha na Uchumi na Kamati ya Nishati na Madini kwamba jumapili tarehe 2 Novemba, 2008 saa saba mchana kutafanyika kikao cha pamoja katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kwa kukutana na wadau wa usafirishaji wa mafuta ya magari na sheheza za mizigo nje ya nchi wakiongozwa na *Tanzania Truck Owners Association.* Kwa hiyo, ziko Kamati tatu nadhani makatibu na Wenyeviti wenu mnafahamu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 31/10/2008 kutakuwa na Kikao cha Kamati saa 4.30 asubuhi katika ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuwa leo tarehe 31/10/2008 kutakuwa na Kikao cha Kamati hii saa 5.00 asubuhi katika chumba Namba 231. Nafikiri Makamu wake ataendesha kwa sababu Mheshimiwa Jenista Mhagama, atakuja kukaa hapa mezani.

Ile Kamati ya Huduma za Jamii Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', sasa nadhani hili ndiyo litasahihisha lile tangazo la kwanza.

Katibu wa Bunge anawatangazia kwamba kutakuwa na semina zifuatazo siku ya tarehe 1 Novemba, 2008 maana yake kesho. Semina hiyo itahusu ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzia saa 3.00 asubuhi nadhani ni *Msekwa Hall* lakini hawajasema.

Lakini Jumapili sasa tarehe 2 Novemba kutakuwa na semina kuhusu Muswada wa Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2008 kutakuwa na semina katika ukumbi wa Pius Msekwa saa 4.30. Nadhani hii ndiyo imesababisha tofauti hapa. Hii semina ya wanyamapori ni Wabunge wote. Kwa hiyo, Kamati na Wizara wamefikiria kwamba ni vizuri Wabunge nanyi mkafanya semina na mkaweza kutoa maoni yenu katika mfumo wa Semina siku ya Jumapili katika Ukumbi wa Msekwa Saa 4.30 wamechukulia muda huu kwa sababu wengine wanakwenda kwenye ibada kwa hiyo saa 4.30 ni muda mzuri.

Itakapokwisha hiyo semina ndiyo maana ile ya Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga itafanyika baadaye yaani baada ya hiyo, hii ya Alhaj Mohamed Hamisi Missanga itahusisha Kamati tatu yaani Kamati ya Miundombinu, Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Nishati na Madini na ninafikiri ukumbi ni huohuo. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti kwa sababu tulikosa muda mwingine ndiyo maana ikaahidi tuji-*organise* namna hii.

Mtakumbuka kwamba pia tulitangaza kwamba kutakuwa na semina ya Wizara ya Afya. Sasa sisi tuliwatangazia kwamba tutakuwa Wabunge wote.

Lakini ikaonekana kwamba watoa huduma uwezo wao kwa kuhudumia sisi Wabunge wote hautoshi na wakataka Wabunge 100 tukasema kwamba wangoje mpaka wakati mwingine, ndiyo maana tumebadilisha na hii sasa. Iko pia ya *East Africa* siku ya Jumapili halafu ya Wanyamapori pia na itafuatiwa na ile ya Kamati tatu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti nadhani imekaa vizuri. Katibu endelea na *Order Paper!*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi wa Mwaka 2008 *(The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Ngozi yaani *The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008* pamoja na jedwali la marekebisho yaani *The Schedule of Amendment.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha Muswada wangu ninapenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Mwera Mbunge wa Tarime kwa kuchaguliwa lakin ipia napenda pia nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mheshimiwa Gideon A. Cheyo na wadau wote waliochangia na kuboresha Muswada huu wa Sheria ambao napenda kuuwasilisha kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Ngozi *The Hides, Skin and Leather Trade Bill, 2008* wanakusudia kuweka utaratibu wa kisheria unaolenga kusimamia uzalishaji, usindikaji na hatimaye biashara ya ngozi kwa kuzingatia hali halisi ya biashara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngozi ni zao muhimu la mifugo ambalo limekuwa likiingizia nchi yetu fedha za kigeni kwa muda mrefu kutokana na mauzo nje ya nchi. Aidha, zao la ngozi limeendelea kutoa ajira na kuboresha kipato cha wafugaji, wafanyabiashara na wadau wengine katika sekta ndogo ya ngozi na hivyo kuchangia katika jitihada za Serikali za kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Biashara ya Ngozi yaani *The Hides and Skin Trade Act number 68, 1963* na marekebisho yake namba 30 ya mwaka 1965 inayopendekezwa kufutwa inainasimamia uzalishaji, ukusanyaji wa bidhaa ya ngozi. Sheria inayopendekezwa kutungwa siyo tu kuwa itasimamia uzalishaji na ukusanyaji wa biashara ya zao la ngozi bali itakusudia pia kusimamia usindikaji wa ngozi kwa lengo la kuboresha zao hilo ili liweze kuendana na matakwa ya biashara hiyo kwa sasa na hatimaye kukuza pato la wafugaji, wasindikaji, wafanyabishara wa ngozi na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya ngozi za ng’ombe, mbuzi na kondoo zinazokusanywa na kuuzwa nje ya nchi imekuwa na mwelekeo wa kuongezeka katika kipindi cha kati ya mwaka 2000/2001 hadi 2006/2007 na 2007/2008. Katika kipindi hicho kumekuwepo na ongezeko la 130% ya ngozi zilizouzwa nje ya nchi. Aidha, mapato yatokanayo na mauzo ya ngozi nje ya nchi yameongezeka kwa 135%, kiasi kidogo cha ngozi ghafi zinazokusanywa takribani 20% hutumika kama malighafi katika viwanda vyetu vinavyosindika ngozi ambazo hatimaye huuzwa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *trend* hiyo utaona kwamba katika mauzo na makusanyo yaliyofanyika katika mwaka 2000/2001 makusanyo kwa ngozi za ng’ombe zilikuwa 1,400,000 wakati ngozi za Mbuzi zilikuwa 750,000 na ngozi za Kondoo zilikuwa 400,000 na hivyo kuwa na jumla ya ngozi 2,550,000 zilizokuwa na thamani ya shilingi bilioni 4.65.

Lakini katika mauzo ya nje ngozi za Ng’ombe zilikuwa ni 1,320,000, ngozi za Mbuzi zilikuwa 597,000 wakati ngozi za Kondoo zilikuwa 208,000 na kuwa na jumla na ngozi zilizouzwa nje 2,125,000 ambazo ziliingizia taifa bilioni 4,383,045,000/=.

Kama nilivyoeleza mlolongo huo umezidi kuongezeka na katika mwaka 2007/2008 makusanyo katika ngozi za Ng’ombe zilikuwa milioni 2500,000 wakati za Mbuzi zilikuwa 1,900,000, za kondoo zilikuwa milioni 1,500,000 na hivyo kuwa na jumla ya ngozi milioni 5.9 zilizokuwa na thamani ya bilioni 13,500,000,000. Lakini katika mauzo ya nje kulingana na ngozi hizo ambapo ngozi za Ng’ombe ziliuzwa milioni 2.3, ngozi za Mbuzi zilikuwa milioni 1.6 na ngozi za Kondoo zilikuwa milioni 1.1 na hivyo kuwa na jumla ya ngozi zilizouzwa nje kuwa ngozi milioni 5 zilizokuwa na thamani ya bilioni 21,500,000,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya ngozi inakabiliwa na tatizo la ubora hafifu wa ngozi unaosababishwa na upungufu uliopo katika sheria ya sasa inayosimamia ubora wa ngozi.

Matatizo ya mengine ni pamoja na lishe duni ya mifugo, umri mkubwa wa mifugo inayochinjwa, chapa za moto, upigaji hovyo wa viboko na mikwaruzo itokanayo na miiba au vitu vyenye ncha kali aidha hali mbaya ya miundombinu ya machinjio, makaro, mabanda ya kukaushia na stoo za kuhifadhia ngozi vinachangia zaidi katika kupunguza ubora na thamani ya ngozi zetu.

Takribani 80% ya ngozi zote zinazozalishwa hapa nchini huuzwa nje zikiwa ghafi kutokana na viwanda vingi vya ngozi kutofanya kazi au kufanya kazi chini ya uwezo wake. Kati ya viwanda 7 vya ngozi vilivyopo hapa nchini ni 6 tu vinavyofanya kazi kwa sasa navyo ni kwa kiwango cha kati ya 30% hadi 50% cha uwezo wake. Hii si kwamba imesababisha kupungua tu kwa mapato bali pia imepunguza nafasi za ajira kutokana na kiwango kidogo cha usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ngozi iliyopo imekuwa haitekelezeki ipasavyo kutokana na mabadiliko mengi ya kiuchumi hivyo kusababisha ugumu katika kusimamia na kudhibiti uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na ubora wa ngozi zenyewe.

Ni mategemeo yangu kuwa Sheria mpya itawezesha kutekelezwa kwa ufanisi majukumu ya kuendeleza sekta ndogo ya ngozi ambayo ni muhimu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko halisi la Muswada huu ni kwamba tangu Sheria ya Ngozi ya *The Hides and Skin Trade Act number 68, 1963* na marekebisho yake ya Sheria namba 30 ya mwaka 1965 ilipotungwa na kuanza kutekelezwa yametokea mabadiliko mengi ya kiuchumi na kijamii hapa nchini na duniani kwa ujumla ambayo kimsingi yamebadilisha sera na mifumo mbalimbali ya kuendeleza na kukuza uchumi wa taifa.

Lakini pia yamekuwepo na sera mpya ya taifa ya mifugo ya mwaka 2006 na kumekuwepo na sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi yaani *Decentralisations by Devolution* yaani D by D ambayo inatoa nafasi kubwa kwa wananchi katika kumiliki na kutekeleza shughuli za uzalishaji, usindikaji na biashara ya mifugo na mazao yake ikiwemo zao la ngozi.

Lakini pia kukidhi mahitaji ya viwango vya ubora kwa zao la ngozi kwa mahitaji ya viwanda vya ndani na nje kwa sababu nimeeleza kwamba karibu 80% ya ngozi zinazouzwa zinauzwa kama ghafi nje ya nchi.

Lakini pia upungufu wa Sheria ambayo kwa kiasi kikubwa umechangia kwa kiasi kikubwa kuifanya Sheria hiyo isiwe na ufanisi kiutekelezaji, mambo haya ni pamoja na:

Sheria kutotamka wazi malengo yaani *objectives* na masuala ya kulinda mazingira. Sheria kutozingatia uendelezaji wa sekta ya ngozi kitaasisi hususani majukumu ya kila mdau. Sheria kutotambua utayarishaji wa ngozi nje ya maeneo ya

machinjio. Sheria kutokuzingatia mfumo wa kupeleka madaraka au maamuzi katika ngazi za wananchi yaani D by D. Sheria kutohusisha shughuli za usindikaji wa ngozi viwandani hasa katika eneo la uchambuzi wa ngozi katika madaraja kwa lengo la kutoa picha halisi ya ubora wa ngozi ili mzalishaji aweze kulipwa bei halisi kulingana na ubora na daraja la ngozi yenyewe. Lakini viwango vya faini na adhabu kwa makosa mbalimbali vimepitwa na wakati lakini sheria haitamki viwango vya ujuzi wanavyotakiwa kuwa navyo wachunaji wa ngozi yaani *Hides Dressers* na wawekaji madaraja ya ngozi yaani *graders* kabla ya kupewa leseni.

Kwa hiyo, upungufu huu wote ndiyo umetuletea kuleta mabadiliko na Muswada mwingine ambao tunaamini unaweza ukaboresha na ukaenda na wakati huu tunaotakiwa kuutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta ufanisi na maendeleo endelevu katika sekta ndogo ya ngozi nchini Muswada huu unazingatia mambo muhimu yafuatayo.

Kwanza, kuundwa kwa Kamati ya Ustawi wa ngozi kuanzia ngazi za Taifa mpaka ngazi ya vijiji. Hii inalenga kupeleka madaraka au maamuzi katika ngazi za wananchi yaani *D by D.*

Pili, Muswada huu utaanzisha utaratibu wa usajili wa maeneo yaani *premises* ya utayarishaji wa ngozi nje ya machinjio ili kudhibiti uharibifu wa ubora wa ngozi na mazingira.

Tatu, kuongeza wigo wa sheria hii ili isimamie pia shughuli za usindikaji wa wa ngozi hasa eneo la ubora wa ngozi zilizosindikwa.

Lakini pia kuboresha utaratibu wa utoaji leseni kwa wachunaji yaani *Hides Dressers* na wachambuzi wa madaraja ya ngozi yaani *Hides Graders,* lengo ni kuanisha aina ya mafunzo na sifa zinazowastahili kuwa nazo wachunaji na wachambuzi wa madaraja kabla ya kupewa leseni.

Mwisho, itasaidia katika kurekebisha viwango vya adhabu na faini vilivyopitwa na wakati ili viendane na hali halisi ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa Sheria mpya ni katika kutekeleza dira ya sekta ya mifugo inayoelekeza yafuatayo na ninapenda ninukuu.

‘Ifikapo mwaka 2025 kuwe na sekta shirikishi ya mifugo inayozingatia ufugaji wa kisasa, endelevu, inayoendeshwa kibiashara, yenye mifugo bora na yenye tija kubwa itakayoinua maisha ya Mtanzania na kutoa ajira, kuzalisha malighafi kwa ajili ya usindikaji na kuongeza pato la taifa na kuhifadhi mazingira”.

Lakini pia dira hii pia inazingatia ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kuhusu kutoa umuhimu katika kuhamasisha wawekezaji katika sekta za kipaumbele yaani sekta ya nguo, ngozi, usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Ni mategemeo yangu kuwa sheria hii mpya itasimamia kwa ufanisi shughuli za uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na ubora wa ngozi na hivyo kurahisisha kufikiwa kwa malengo na matarajio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayopendekezwa kutungwa inatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo.

Kwanza, kuongezeka kwa makusanyo, ubora wa ngozi na mapato yatokanayo na ngozi kwa sababu kwa sasa hivi makusanyo ni karibu bilioni 21.5 kwa hiyo tunaamini kabisa kwamba sheria hii itasaidia kuongeza makusanyo na hivyo kuliongezea taifa fedha.

Pili, kutaongezeka kwa uwekezaji kwenye viwanda vya ngozi ambavyo kwa sasa hivi katika viwanda 7 ni viwanda 6 tu ndivyo vinafanya kazi navyo vinafanya katika kiwango cha 30% hadi 50% ya kiwango chake.

Tatu, kupeleka maamuzi katika ngazi za wananchi kwa kuwepo kwa Kamati za Ushauri kwa zao la ngozi mpaka ngazi za vijiji.

Nne, kutapunguza uchafuzi wa mazingira unaotokana na mabaki yatokanayo katika sehemu za kukaushia ngozi na viwanda vya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 6 zinazopendekeza mambo mbalimbali kuhusu uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na biashara ya ngozi kama ifuatavyo:-

Katika sehemu ya kwanza ambayo ni vifungu namba 1 – 4 sehemu hii inahusu jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, tafsiri ya maneno mbalimbali na misingi muhimu ya sheria hii.

Katika sehemu ya pili ambayo ni kutoka fungu namba 5 – 9 sehemu hii inahusu kuanzishwa kwa Kamati ya Ushauri ya Taifa, Kamati za Ushauri za Wilaya na vijiji na kuhusu uendelezaji wa zao za ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya tatu ambavyo ni vifungu namba 10 – 13 sehemu hii inahusu taratibu za usajili wa sehemu za utayarishaji wa ngozi nje ya

machinjio. Lengo la kusajili maeneo ya utayarishaji wa ngozi nje ya machinji ni kuepuka sehemu hizo kuwa vyanzo vya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ambayo ni kuanzia vifungu namba 14 – 27 sehemu hii inahusu utoaji wa leseni mbalimbali zikiwemo za maeneo ya kukaushia ngozi, biashara ya ngozi, leseni za wachunaji na wachambuzi wa ngozi, muda wa leseni na upatikanaji wa leseni mpya.

Aidha, sehemu hii inaeleza sifa za kupata leseni hizo na adhabu zitakazotolewa endapo masharti ya leseni hizi zitakiukwa. *(Makofi)*

Katika sehemu ya tano ambayo inahusisha vifungu vya namba 28 – 30. Sehemu hii inaelezea taratibu za uteuzi wa wakaguzi wa ngozi na madaraka yao chini ya sheria inayopendekezwa. Aidha, inampa madaraka Mkurugenzi mwenye dhamana ya ngozi kukasimu madaraka kwa Watendaji wengine katika Halmashauri za mitaa.

Katika sehemu ya sita na ya mwisho ambayo ni kuanzia kifungu namba 31 – 35 sehemu hii inahusu masuala ya ujumla, mambo ya msingi katika sehemu hii ni taratibu za kuwasilisha rufaa kama haki haijatendeka katika shughuli za utoaji wa leseni zinazosimamia utoaji, zinazosimamia uzalishaji na ukusanyaji na usindikaji wa ngozi.

Inazungumzia pia aina ya makosa katika uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa ngozi na adhabu zake, Mamlaka ya wahusika mbalimbali na dhamana za uendelezaji wa zao la ngozi katika kuandaa na kurekebisha Kanuni na taratibu mbalimbali juu ya uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa ngozi chini ya sheria hii.

Pia inazungumzia juu ya mapendekezo ya kufuta sheria ya biashara ya ngozi namba 68 ya mwaka 1963 na marekebisho yake namba 30 ya mwaka 1965.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulisomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni na baadaye kukabidhiwa kwenye Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulijadiliwa na Kamati hii pamoja na wadau mbalimbali na kutolewa maoni na ushauri. Maoni na ushauri huu vimezingatiwa na hivyo kuandaliwa jedwali la marekebisho yaani *Schedule of Amendment* ambayo tumeigawa ambayo ninaamini imehusisha michango yote iliyotolew ana wadau pamoja na Waheshimiwa Wabunge na nimeiwasilisha hapa kwa ajili ya kupitiwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kukushukuru na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuweza kupata nafasi ili niweze kusoma Muswada huu na baada ya kusema haya sasa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, hoja hiyo imeungwa mkono. Naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu au mwakilishi wake, Mheshimiwa Keenja nadhani.

**MHE. CHARLES N. KEENJA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi wa Mwaka 2008 (*The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata nafasi ya kujadili Muswada huu katika vikao vitatu, vilivyofanyika kwenye Ofisi ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam na kimoja kilichofanyika Dodoma. Katika kikao cha kwanza kilichofanyika tarehe 13 Oktoba, 2008, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, alitoa maelezo ya jumla juu ya madhumuni ya Muswada na yaliyomo kwenye vipengele vyake. Kikao cha pili kilifanyika tarehe 15 Oktoba, 2008 kiliwashirikisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo. Baadhi ya Wadau walioshiriki ni Wafanyabiashara ya Ngozi, Wafugaji, Wachinjaji, Bodi na Viwanda vya Nyama, Vyombo vya Habari na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati inawashukuru Wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao, ambayo yamezingatiwa katika marekebisho ya Muswada na mengine yatazingatiwa katika Kanuni zitakazotayarishwa chini ya sheria hii itakapokuwa imepita kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri.

Katika kikao cha tatu ambacho kilifanyika tarehe 17 Oktoba, 2008, Kamati ilizingatia michango ya wadau, pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Waziri. Kikao cha nne kilifanyika Dodoma tarehe 28 Oktoba, 2008, kupitia rasimu ya marekebisho ya Muswada yaliyoandaliwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Kamati inaridhika na maudhui na madhumuni ya Muswada. Pamoja na kuunga mkono Muswada, Kamati ilimshauri Waziri, kuzingatia baadhi ya maoni ya wadau na ilipendekeza marekebisho katika baadhi

ya vifungu vya Muswada. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, maoni ya Kamati pamoja na yale ya Wadau, yamezingatiwa katika marekebisho ya Muswada yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake aliyoitoa hivi punde ya kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yanayofuta yatafanana sana na yale aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri na hili linatokana na ukweli kwamba, chanzo chetu cha takwimu kimoja kikatofautiana tu katika matumizi ya takwimu hizo. Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi katika Bara la Afrika. Inakisiwa kwamba, tuna zaidi ya ng'ombe milioni 18.8, mbuzi milioni 13.5 na kondoo milioni 3.6. Kutokana na hali hiyo, nchi yetu huzalisha ngozi nyingi kila mwaka. Kwa mfano, katika mwaka wa 2007/2008, ngozi za ng'ombe vipande milioni 2.5, mbuzi vipande milioni 1.9 na kondoo vipande milioni 1.5 zilizalishwa.

Asilimia 80 ya ngozi zinazozalishwa humu nchini huuzwa nje zikiwa ghafi; ni asilimia 20 tu inayosindikwa kabla ya kuuzwa. Biashara ya ngozi huliingizia Taifa mapato makubwa kila mwaka, kwa mfano, katika mwaka wa 2007/2008, mauzo ya ngozi nje ya nchi yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 21.5. Aidha, biashara ya ngozi huwapatia mapato wafugaji, wasindikaji, wafanyabiashara na Taifa kwa jumla na inawapatia wananchi wengi ajira. Ni dhahiri kwamba, sekta ndogo ya ngozi ina umuhimu mkubwa katika uchumi wa Taifa. Hata hivyo, sekta hiyo inakabiliwa na matatizo mengi ambayo yanaifanya isiweze kutoa mchango wake kikamilifu. Ubora wa ngozi ambao ndio unaifanya iwe na bei kubwa, unatokana na matunzo bora ya mifugo na usindikaji mzuri wa ngozi: Matatizo makubwa yanayoikabili sekta hii ni pamoja na:-

(a) Baadhi ya vitendo vya wafugaji na wachungaji husababisha kuharibika kwa ngozi: vitendo hivyo ni pamoja na lishe duni ya mifugo, kuweka chapa kwa moto, kuwapiga ng'ombe kwa fimbo na mifugo kukwaruzwa na vitu vyenye ncha kali.

(b) Ukosefu wa miundombinu muhimu kama machinjio, mabanda ya kukaushia ngozi na maghala ya kuhifadhia ngozi.

(c) Ubovu na hata ukosefu wa miundombinu ya usafirishaji, hususan barabara na reli, inaathiri usafirishaji wa ngozi na kwa hiyo, biashara ya ngozi.

(d) Wafugaji kutokuthamini ngozi na kwa hiyo, kutomtunza mnyama katika mazingira yatakayodumisha ubora wa ngozi yake.

(e) Ngozi nyingi huharibiwa wakati wa uchunaji kutokana na wachunaji kutokuwa na vifaa sahihi, kutokuwa na ujuzi unaotakiwa na kutokuwepo kwa usimamizi madhubuti katika machinjio. Hali hii inatokana na kutokuwepo kwa mafunzo ya taaluma ya ngozi hapa nchini kwa zaidi ya miaka kumi na mitano.

(f) Sekta ya ngozi imeendelea kudumaa kutokana na kuwepo kwa ulanguzi na magendo ya ngozi yanayofanywa na watu kutoka nje ya nchi ambao wananunua ngozi ghafi kwa bei ndogo na kwenda kuziuza kwa bei kubwa.

(g) Kutokuwepo kwa viwanda vya kutosha vya kusindika ngozi zinazozalishwa humu nchini. Viwanda saba vilivyopo vinafanya kazi kwa viwango vya chini vya kati ya asilimia 30 na 50. Aidha, viwanda vilivyokuwa vya umma na vilivyobinafsishwa vimefungwa tangu vibinafishwe hadi sasa. Kutokusindikwa kwa ngozi kunasababisha mapato yanayotokana na ngozi yawe madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa Sheria hii mpya kunalenga kuondoa changamoto zilizopo, kuweka utaratibu wa kusimamia usindikaji wa ngozi kwa lengo la kuziboresha ili ziendane na matakwa ya soko na hatimaye kukuza mapato ya wafugaji, wafanyabiashara, wasindikaji na Taifa kwa jumla. Ni mategemeo yetu kuwa, sheria mpya itawezesha kutekelezwa kwa ufanisi; majukumu ya kuendeleza sekta ndogo ya ngozi ambayo ni muhimu kwa uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili madhumuni ya Muswada huu yaweze kutimizwa kwa kiwango cha kuridhisha, Kamati inaona ni muhimu kwa Serikali kufanya yafuatayo:-

Kwanza, Serikali iendelee kuboresha huduma kwa wafugaji kwa kuhakikisha kwamba:-

- Wafugaji wanamilikishwa maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo yao vijijini.

- Huduma za ugani, maji na malisho katika maeneo ya Wafugaji ziwe ni za uhakika na zinapatikana nyakati zote.

- Kama ilivyo kwa wakulima, wafugaji nao waendelee kupewa ruzuku kwa pembejeo wanazozihitaji.

- Inakuwepo mipango ya uhakika na endelevu ya masoko ya mifugo na bidhaa zitokanazo na mifugo kama vile Minada, Viwanda, Machinjio ya kisasa na kadhalika.
- Zinakuwepo sheria za kudhibiti ushindani wa haki na kulinda soko la ndani katika Sekta ya Mifugo.

Pili, Serikali iendelee kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara katika Sekta ya Mifugo kwa kuhakikisha kwamba:-

- Taratibu za uuzaji na ununuzi wa mifugo, pamoja na usafirishaji zinakuwa wazi na bila vikwazo. Aidha, utoaji wa leseni, utozaji ushuru na utoaji wa vibali vya kusafirisha mifugo, unakuwa wazi ili kuwezesha kuendeleza biashara ya mifugo.

- Huduma za Minada, Machinjio ya Kisasa na biashara ya nje ziendelee kuboreshwa ili biashara ya mifugo iwe na manufaa makubwa zaidi kwa wadau wote na Taifa kwa ujumla.

- Mipango ya Elimu kwa wadau wa Sekta ya Mifugo; Wafugaji, Wafanyabiashara na Wasindikaji wa ngozi na kadhalika inaendelea kwa lengo la kuboresha sekta ya mifugo na kuifanya ya kisasa zaidi.

- Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha kuwa kiasi kikubwa cha ngozi zinazozalishwa humu nchini kinasindikwa kabla ya kuuzwa nje ya nchi. Nimetangulia kusema kwamba ni asilimia 20 tu inayosindikwa humu nchini. Aidha, ihakikishe kwamba, viwanda vyote vya ngozi vilivyobinafsishwa vinafanya kazi, vinginevyo virejeshwe Serikalini na Serikali iamue itafanya nini.

- Baada ya sheria mpya kupitishwa na kanuni zake kutayarishwa, hatua za haraka zichukuliwe kutafsiri sheria na kanuni hizo kwa Lugha ya Kiswahili ili ziweze kueleweka kwa urahisi zaidi kwa wadau wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inapenda kumshukuru sana Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, pamoja na wataalamu wao, kwa kuwasilisha Muswada huu kwenye Kamati kwa umakini mkubwa sana. Aidha, Kamati inawashukuru Maofisa kutoka kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wote walioitikia wito wa kushiriki katika vikao vya mashauriano na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ambao wametoa maoni katika kuuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama; Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Charles N. Keenja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Frank Mbumi na Ndugu Pamela Pallangyo, kwa huduma zao kwa Kamati na kwa kuhakikisha kwamba, maoni ya Kamati yanaandaliwa na yanakamilika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuupitisha Muswada huu kwa sababu ni muhimu sana kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, naunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Mwadini Jecha.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA (MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai, uwezo na ujasiri wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007, kuhusu Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi ya Mwaka 2008 (*The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008).*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kwamba, hapa nchini tuna idadi kubwa ya mifugo, yaani ng'ombe milioni 19.1, mbuzi milioni 13.6 na kondoo milioni 3.6, lakini inashangaza kuona kwamba, Pato la Taifa litokanalo na biashara ya uzalishaji wa ngozi nchini ni dogo mno ukilinganisha na idadi ya mifugo tuliyonayo. Hii inatokana na sababu kwamba, hakuna juhudi za kutosha zinazowekezwa katika suala zima la usimamizi na uendelezaji wa zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Biashara ya Ngozi nchini inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinashusha ubora wa ngozi. Changamoto hizo ni pamoja lishe duni, maradhi hususan ya ngozi, uwekaji alama kwenye miili ya mifugo kwa kutumia moto na/au vitu vyenye ncha kali, uchinjaji na uchunaji mbaya wa ngozi, taaluma ndogo ya utengenezaji wa ngozi na uchache wa viwanda vya kutengeneza na kusarifu ngozi. Kubwa zaidi ni udhaifu wa sheria iliyopo inayosimamia zao la ngozi. Kambi ya Upinzani inatarajia kwamba, sambamba na madhumuni ya kupitisha Muswada huu, Serikali itasimamia vyema zao la ngozi kwa kuondoa changamoto zinazolikabili zao hili ili hatimaye liweze kumpatia tija mfugaji na ongezeko katika pato la uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato mzima wa kuandaliwa kwa Muswada huu kabla ya kufikishwa Bungeni hii leo, wadau mbalimbali walipata nafasi ya kuujadili na kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa Serikali imeyazingatia na kwa hilo tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hiyo. *(Makofi)*

Kadhalika, Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, nayo imetoa mchango wake mkubwa katika kuuboresha Muswada huu. Niseme kwamba, Kambi ya Upinzani nayo kimsingi haina pingamizi kwa Bunge lako Tukufu kuupitisha Muswada huu na kuwa sheria kamili, hasa tukizingatia madhumuni na sababu ya kuletwa Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kwa kuzingatia hayo na kwa azma ya kuuboresha Muswada huu, tuna maoni machache ambayo tunaiomba Serikali iyazingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya III kifungu cha 10, vifungu vidogo vya (2), (3) na (4) vinavyohusu utaratibu wa kusajili jengo/eneo kwa ajili ya matumizi ya biashara ya ngozi; sisi tunaona kuna jambo la msingi ambalo halikuzingatiwa, nalo ni kuweka sifa za hiyo *Registration Authority*, kama matakwa yanavyoonekana katika kifungu kidogo cha (5) (a) na (b). Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuzingatia na kuweka sifa za hiyo *Registration Authority* wakati inaandaa kanuni zitakazosimamia utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 11, kifungu kidogo cha (3) kinaruhusu *Registration Authority*, kwa kufuata ushauri wa Mkaguzi kubadili vigezo/sifa za mahala au jengo linaloombewa usajili mpya. Hivyo basi, panaonyesha umuhimu wa wazi kutajwa sifa au vigezo vinavyohitajika katika *premises* inayohitajika kwa matumizi ya biashara ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 24 inataja kuwa, kipindi cha kubadilisha cheti cha usajili kuwa ni mwaka mmoja. Kambi ya Upinzani inaona kipindi hicho ni kifupi sana, kwani kinaweza kusababisha usumbufu kwa wafanyabiashara wa ngozi, tunaishauri Serikali kwamba, kipindi hicho kiongezwe kiwe miaka miwili au mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika ibara ya 13, kifungu kidogo cha (1), kinachohusu jinsi wamiliki au watumiaji watakavyoshughulikia *effluents* zinazotoka kwenye viwanda vya ngozi ili kuhifadhi mazingira. Lakini ni dhahiri kwamba, *effluents* sio jambo pekee linaloharibu mazingira kwenye viwanda vya ngozi, bali ni pamoja na *air pollution*, ambalo hili limekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo yanayotengenezwa ngozi. Muswada huu bado haujazamia kwa undani juu ya namna ya kudhibiti harufu mbaya itokanayo na matayarisho au matengenezo ya ngozi viwandani. Tunaiomba Serikali kuliangalia kwa undani suala hili na kulipatia ufumbuzi unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 14 (2), 15 (2) na 33 (1) na (2) vinavyohusu adhabu, vinasema kwamba, mtu atayekwenda kinyume na kwa mujibu wa maelekezo ya vifungu hivyo, atakuwa ametenda kosa na kama akihukumiwa atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kwenda jela kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja. Kambi ya Upinzani, inaona sio busara kwa sheria hii kutaja kiwango cha juu pekee cha adhabu, kwa sababu upo uwezekano wa mfanyabiashara kupima *cost benefit ratio* ya biashara yake na akiona mambo ni mazuri akaamua kutenda kosa kwa mintarafu ya kujiongezea faida. Tunaishauri Serikali itaje katika sheria hii, kiwango tajwa cha adhabu kiwe ndio cha chini *(minimum sentence)* na kiwango cha juu cha adhabu kiachiwe Majaji na Mahakimu, kulingana na mazingira husika ya utendaji wa kosa lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 31(3) inatamka kwamba, katika ukataji wa rufaa, uamuzi unaotolewa na Waziri au Mkuu wa Mkoa ndio wa mwisho na kwa hiyo Mkurugenzi, Mkaguzi na Mamlaka ya utoaji leseni ni lazima kufuata na kutekeleza maamuzi hayo.

Mheshimwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona utaratibu huu unamnyima mrufani haki yake ya msingi ya kwenda Mahakamani pale ambapo hakuridhika na maamuzi ya viongozi tajwa hapo juu. Hii ni kinyume cha Katiba ya Nchi ibara ya 4(2) inayosema kuwa nanukuu; "Vyombo vyenye Mamlaka ya kutekeleza utendaji haki vitakuwa ni Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar." Lazima dhana ya mhimili wa tatu wa Dola, yaani Mahakama kupewa nafasi yake na iheshimiwe na si vinginevyo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, uamuzi wa Waziri au Mkuu wa Mkoa usiwe ni wa mwisho kwa yeyote ambaye ameona hakutendewa haki katika utekelezaji wa sheria hii, bali mkondo wa Mahakama upewe nafasi yake katika kutoa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru kwa mawasilisho yote hayo. Huu Muswada mpaka sasa wachangiaji wamekuwa sijui wachache sana, kwa hiyo, nafasi bado ipo na ni Muswada wa siku nzima. Wafugaji wapo wengi hapa sijui wamebana wapi?

Kwa hiyo, watakaoanza hapa yupo Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kule kwake ng'ombe wenyewe wa kuhesabu. Halafu yupo Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, halafu yuko na Mheshimiwa Martha Umbulla lakini na wengine nafasi bado ipo.

Waheshimiwa Wabunge, nitamwachia nafasi Mheshimiwa Mwenyekiti aendelee na kikao.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Spika, tutaanza kusikiliza mchango kutoka kwa Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, halafu tutaendelea na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

**MHE SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Muswada huu. Nataka kumwambia Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba mimi vile vile ni mfugaji kwa kiasi fulani, kwa hiyo, asishangae kuwa nachangia Muswada wa Ngozi.

Kwanza niseme kwamba, naunga mkono Muswada huu kwa sababu ya malengo yake. Malengo makubwa ya Muswada huu ni kuifuta Sheria ya Ngozi ya Mwaka 1963, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1965. Ni kwamba, sheria hii kwa umri wake haitekelezeki, kwa hiyo, ilikuwa ni lazima kutunga sheria mpya ambayo inaendana na wakati wa sasa. Sheria hii ina miaka karibu 43, kwa hiyo ni dhahiri kwamba, hata baadhi ya Wabunge walikuwa hawajazaliwa. Mambo yaliyomo kwenye sheria hii kwa kweli hayatekelezeki; ni kichekesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia kwenye kifungu kimoja kimoja vya Muswada, nataka kwanza nizungumze mambo ya jumla jumla. Kwanza, nigusie umuhimu wa sekta hii ya ngozi. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba, sekta ya ngozi ni muhimu sana katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kwa sababu mchango wake ni mkubwa zaidi kuliko sekta ya mifugo ya wanyama inayouzwa hai au nyama zao zinauzwa ama ndani au nje ya nchi.

Kwa mfano, katika mwaka uliopita wa 2007/2008, jumla ya ng'ombe hai waliouzwa na nyama zao ni shilingi bilioni 2.3. Ngozi peke yake zilizouzwa ni karibu shilingi bilioni 13.5. Utaona kwamba, mapato kutokana na ngozi peke yake ni karibu mara sita kuliko yale ya wanyama waliouzwa wakiwa hai na baada ya kuchinjwa na kuuzwa nyama zao. Kwa hiyo, inaonyesha umuhimu wa ngozi ni mkubwa sana. Sasa Serikali haina budi kwa hili kuipa umuhimu sekta ya ngozi ili kuongeza pato la ndani na la nje. Hatua ambazo inapaswa kuchukua Serikali ni kuanza kuongeza uzalishaji wa ngozi zenyewe. Pili, kuongeza ukusanyaji wa ngozi kutoka maeneo mbalimbali. Najua kwamba, wanyama wengi wapo vijijini na ng'ombe anachinjwa kule na ngozi zinatupwa tu baadhi ya maeneo. Sasa namna ya kuzikusanya kuzileta katika maeneo ya usindikaji ni kazi kubwa.

Kwa hiyo, baada ya kuzikusanya inabidi kuzitayarisha na matayarisho haya yanahitaji viwanda kama alivyosema Mheshimiwa Waziri hapa na Kambi ya Upinzani kwamba, viwanda vinavyofanya kazi ni vichache mno; si zaidi ya sita na vile vile vinafanya kazi chini ya asilimia 50 ya uwezo wake. Sasa kuna haja Wizara ya Viwanda na Biashara, kujiweka tayari katika hili ili kuhakikisha kwamba, viwanda vya ngozi vinafanya kazi kwa kiwango chake lakini vilevile kuongeza viwanda vingine vya kusindika mazao ya ngozi. Tunahitaji viatu vya ngozi, tunahitaji mikoba ya ngozi, tunahitaji mikanda ya ngozi, lakini tunaagiza kutoka nje; ni jambo la kusikitisha. Tunahitaji vilevile mafunzo ya watu watakaofanya shughuli hizi kule vijijini, wilayani na katika ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote haya yanahitaji fedha. Wizara hii ni moja katika Wizara ambayo katika bajeti iliyopita ilikuwa na ufinyu mkubwa sana wa fedha. Mtakumbuka bajeti ya Wizara hii ilikuwa ni shilingi bilioni 41.8 tu. Katika shilingi bilioni 41.8, shilingi bilioni 20.3 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na katika shilingi 20.3 bilioni 12.6 zinatoka fedha za nje, yaani kwa wafadhili wetu na ni shilingi bilioni 7.7 ndio fedha za ndani. Sasa kwa kuwa fedha za nje zinachelewa kufika, inaweza kuathiri shughuli zetu; fedha za ndani ni kidogo mno. Kwa hiyo, nafikiri mchango wa Serikali katika sekta ya ngozi kifedha bado hautoshi na kwa sababu sekta hii inachangia sana katika Pato la Taifa, nafikiri ipo haja ya kuongeza ili Wizara hii mwakani iweze kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuongeze idadi ya ngozi lazima pia tuiimarishe biashara ya ngozi ndani ya nchi. Kama nilivyosema kwamba, ngozi zipo vijijini kwa wingi na hizo zinakusanywa kuletwa mijini. Lakini kuna matatizo makubwa ambayo yanalalamikiwa na wafanyabiashara kwamba, usafirishaji wa ngozi kutoka vijijini kwenda mijini ni matatizo makubwa. Pamoja na kwamba, wanapewa *movement permits*

au hati za kusafirisha ngozi, lakini kuna vikwazo mbalimbali katika hati kwenye barabara ambavyo wasafirishaji wa ng'ombe kutoka vijijini kuja mijini yanawapata. Kwa mfano, kuna mageti hapa mara wanaambiwa *permit* zenu hazitambuliki, mara wanaambiwa subirini mara wanadaiwa rushwa na kadhalika. Kwa hiyo, biashara ya ng'ombe kutoka vijijini, inakuwa ngumu kwa sababu urasimu unakuwa mkubwa na wafanyabiashara wanalalamika sana kwa sababu wao ndio wanaochukua ng'ombe au ngozi kutoka vijijini na kuleta mijini. Mjini ndio kwenye walaji wakubwa wa nyama. Kwa mfano, Dar es Salaam; hivi sasa wanasema kiasi cha ng'ombe 1,000 wanachinjwa kila siku na hapa Dodoma wanasema kiasi cha ng'ombe 200 na sisi tunakula kila siku. Sasa utakuta mijini ndiko kuna mkusanyiko mkubwa wa ngozi na wa nyama lakini ufikaji wa vitu hivi mijini unakuwa ni vitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la jumla ambalo nataka kulizungumza ni kusaidia Viwanda vya Ngozi. Mimi nilipata bahati kukitembelea Kiwanda kimoja cha Ngozi cha Himo Tanneries kilichopo Moshi. Vijana hawa ambao wapo katika Kiwanda kile wanafanya kazi nzuri sana; wanatayarisha ngozi kwa ajili ya kusafirisha nje lakini vilevile wanatengeneza mikanda na mipira ya kuchezea lakini wana matatizo makubwa sana. Vifaa vyao au mashine zao za viwanda ni za kizamani mno, huwezi kufikiria. Vinapoharibika vifaa vyao huwezi kupata spea sehemu yoyote duniani, wao ni wabunifu wakubwa wanachonga wenyewe kila kitu. Kwa hiyo, wanaendesha kiwanda kile kutokana na ubunifu wao tu, vinginevyo ilikuwa imeshindwa.

Sasa cha kustaajabisha ni kwamba, watu kama hao ambao wamejitolea kufanya kazi hizi wameitikia wito wa Serikali lakini wanakosa uwezo wa kufanya shughuli kwa sababu hawana mtaji wa kutosha. Vijana hao wamehangaika sana kwenda huku na kule kutafuta mikopo, lakini wameangukia patupu. Kwa hiyo, nafikiri ipo haja maeneo kama haya ambayo yanasaidia kuongeza uchumi wa nchi, yakashughulikiwa vilivyo ili wapatiwe mikopo ya kutosha na wazalishe kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye Muswada wenyewe kifungu kwa kifungu; kwanza, nizungumzie sehemu ya 2 ya Muswada vifungu vya 5, 6, 7, 8 na 9 ambavyo vinazungumzia kuhusu Kamati za Ushauri. Kamati hizi zipo za aina tatu; kuna Kamati za Ushauri za Kitaifa, Kamati za Ushauri za Wilaya na Kamati za Ushauri za Vijiji. Kamati za Ushauri za Taifa zina wajumbe 9; maelezo yake ya kazi zake yameelezwa na muundo wa Kamati hizo umeelezwa. Kamati za Ushauri za Wilaya ambazo wajumbe wake ni 7, kazi zake zimeelezwa, lakini muundo wake haukuelezwa. Hali kadhalika, Kamati za Ushauri za Vijiji ambazo zina wajumbe 5 kazi zake zimeelezwa lakini muundo haukuelezwa; sasa nafikiri hili ni tatizo kubwa sana. Kwa sababu unapoacha suala kama hili sifa za wale ambao wanaunda Kamati, unaacha fursa ya kuchaguliwa watu ambao wana sifa na kuchaguliwa watu ambao wapo pale kwa maslahi ya baadhi ya viongozi; nadhani hicho ndicho chanzo kimoja cha kuleta ufisadi katika shughuli zetu.

Kwa hiyo, nafikiri muundo wa Kamati hizi za ushauri za Wilaya na vijiji lazima uainishwe ili kila itakayosajiliwa pale ijulikane uwezo wake wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho nilitaka kukielezea ni cha 12 ambacho kinaeleza kuhusu *Environmentary Impact Assessment,* yaani usajili wa maeneo ya matayarisho ya ngozi lazima uendane na *EIA.* Vilevile kifungu cha 13 cha kwanza ambacho kinaeleza habari ya *Management of Effluent;* yaani ulazima wa kudhibiti uchafu utokanao na viwanda hivi. Mimi nafikiri vifungu hivi ni muhimu sana, kwa sababu vinalinda mazingira na pia vinalinda afya za wafanyakazi na wananchi ambao wanaishi maeneo ya karibu.

Sasa kwa kawaida, viwanda vya ngozi suala hili la *effluent,* yaani maji machafu yanayotakana na viwanda hayadhibitiwi ipasavyo. Sasa inasababisha matatizo makubwa kwa wananchi ambao wanaishi maeneo ya jirani na viwanda hivyo. Kwa hiyo, nafikiri ipo haja sasa hivi ya Sheria hii kuanza kufanya kazi kuona kwamba, viwanda hivi vinatekeleza matakwa ya vifungu hivi viwili; mazingira na vilevile kudhibiti uchafu ambao unatokana na viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 13(2), kinazungumzia juu ya adhabu na hapa adhabu zipo za aina mbili; kuna adhabu ya kifungo na adhabu ya faini. Adhabu ya kifungo inasema si zaidi ya miezi 12 na adhabu ya faini inasema si zaidi ya shilingi milioni moja. Unaposema si zaidi ya miezi 12, unampa nafasi Hakimu kuchagua mwenyewe anavyopenda na inawezekana akamfunga mhusika pengine wiki moja au mwezi mmoja na wewe ulikusudia labda apate adhabu kali kama alivyosema Mheshimiwa Waziri; nadhani hapa sijui kama Sheria itakubali, ingekuwa kama ilivyosema Kambi ya Upinzani; si chini ya miezi ya miezi 12 au si chini ya shilingi milioni moja.

Vilevile kuhusu fedha hizi mimi nafikiri fedha ya Tanzania kama tunavyoona thamani yake inashuka mara kwa mara. Unaweza ukaona shilingi milioni moja leo ni kubwa, lakini baada ya miaka mitatu milioni ikaonekana haina maana sana. Kwa hiyo, nafikiri kama inawezekana labda kuweka fidia hii kwa fedha za kigeni kidogo ambayo ni *stable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya Muswada huu kifungu cha 19 kinahusu mmiliki wa leseni za maeneo ya kutengenezea ngozi. Inasema kwamba, mmiliki ambaye atashindwa kutekeleza biashara yake na ambaye hana sifa ya kuendelea na biashara, itabidi arudishe leseni kwa mamlaka ambayo imempa leseni hiyo. Mimi nafikiri suala si kurudisha leseni, kwa sababu anaweza kurudisha leseni lakini kwa utaalam wa leo anaweza aka-*scan* leseni hiyo na akaendelea kuitumia. Sasa cha msingi hapa ni ufuatiliaji, yule ambaye amaeambiwa asifanye biashara; je, kweli hafanyi biashara? Lakini kurudisha leseni halafu unakaa ukijua kwamba mtu fulani hafanyi biashara, kumbe ana leseni nyingine ambayo ametengeneza kwa utalaam wa kileo na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu wa Sheria ya Ngozi, ulioletwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi na nipende kusema kwamba, nauunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Muswada uliochelewa ni huu. Nadhani wafugaji wakisikia fedha zilizopatikana kwa ajili ya ngozi ambazo Serikali na taifa hili limepata, wataona kwamba kuna fedha nyingi sana zinazopotea kwa ajili ya kupeleka ngozi na kupeleka mifugo nje ya nchi. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na Wizara yake, kwa kuandaa Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni. Pamoja na Kamati iliyojadili Muswada huu, kwa kweli taarifa hiyo ya Kamati imenifurahisha sana kwa sababu imetaja kila mahitaji ya wafugaji na kila kitu kinachohusu mambo ya ngozi.

Nianze na sensa; sensa ya mifugo tunayoambiwa hapa ni sensa iliyopitwa na wakati; na ni sensa ya miaka 20 iliyopita. Ukisema hii sensa ni ya mwaka 1988, ndiyo *data* hizo tunatumia mpaka leo imekuwa ni takwimu za uongo. Tunasema kila mwaka kwamba, sisi ni namba tatu kwa Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, lakini tunatumia sensa ya mwaka 1988. Huu ni uongo, inawezekana sasa tumekuwa namba ya kwanza au ya pili.

Kwa hiyo, ningependa kwa mwaka huu tufanye sensa ya wanyama wote. Kama kila wakati mnafanya sensa ya wananyamapori, hata juzi ndege zilikuwa zinazunguka kuhesabu wanyamapori; hivi kwa nini mnashindwa kuhesabu mifugo kama inawezekana kuhesabu ya wanyamapori waliotawanyika porini ambao hawana wenyewe kuliko mifugo yenye wenyewe? Ukienda kwa kila mfugaji, anakwambia idadi ya mifugo aliyonayo. Mnaona ni rahisi kupata idadi ya wanyamapori kuliko kupata idadi ya mifugo! Hiyo si kwamba inashindikana; ni kwamba Serikali hawataki kuhesabu mifugo na kufanya sensa ya mifugo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mazao yanayotokana na mifugo. Mifugo wana mazao ya aina nyingi; wana nyama ambayo kila siku tunaitumia na kuna ngozi. Kwenye ngozi kuna vifaa vingi; mikanda, mipira hawa wapenzi wa Simba na Yanga au Manchester wanachezea kila siku. Huwezi kucheza mpira bila kuwa na ngozi. Hata ukijaribu kutengeneza mpira nje ya ngozi, huwezi kumaliza dakika tisini. Kwa hiyo, ngozi ndiyo kitu muhimu, hata kwenye makochi tunayokalia ya bei ghali sana ni ya ngozi, inakwenda mpaka shilingi milioni 10 seti moja. Viatu shilingi laki tatu mpaka laki tano kiatu cha ngozi. Kwa hiyo, ngozi ni vifaa vyenye thamani kubwa sana na inatokana na mifugo. Ngozi zitakuwa na ubora zikienda nje zikitengenezwa tunarudishiwa halafu tunanunua vifaa. Ukienda kwenye maduka ya *furniture*, vifaa vyote vinatoka nje, lakini ni ngozi ya mifugo wa Tanzania ndiyo wamekwenda kutengeneza huko nje na kurudisha Tanzania kwa sababu sisi hatuna viwanda. Tatizo letu kubwa sisi hatutaki kufanya biashara, hatutaki kutengeneza vifaa vinavyotokana na mali iliyoko Tanzania mpaka iende nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tupo mpakani; idadi ya mifugo kutokana na *data* zilizotokana na Mheshimiwa Waziri, Kenya wana-*data* za mifugo wanaoingia Kenya

kutoka Tanzania na ni wengi kuliko *data* unazozisema wewe hapa. Kila siku kwenye minada na masoko ya Kenya, ng'ombe wa Tanzania ndiyo wengi zaidi kuliko wa kwao na ndiyo wauzaji wakubwa wa ngozi kuliko sisi, lakini mifugo inatoka Tanzania na hii ni kwa sababu hatuna masoko ya ngozi wenzetu wanayo.

Hatuna viwanda vya nyama wao wanavyo na wanachofanya; mfugaji akiuza ng'ombe kwenye kiwanda mwisho wa mwaka kila mfugaji anapewa fedha za ngozi alizouza kwenye kiwanda kile mwaka mzima. Kwa hiyo, hawawezi kupeleka mifugo sehemu nyingine, wao si kwamba wameuza mnyama, pamoja na kumuuza lakini baadae utarudishiwa fedha za ngozi za ng'ombe wako. Kwa hiyo, hawa wenzetu wanafaidi zaidi kuliko sisi.

Jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni huduma za mifugo. Kamati wameeleza sana huduma ambazo zinastahili mifugo wapate. Wameacha dawa za mifugo, kwa sababu hata kupe wanaharibu ngozi. Kwa hiyo, mifugo inastahili ipate dawa waogoshwe. Wakiogeshwa ngozi itakuwa nzuri na itakuwa na ubora mzuri. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, dawa za mifugo wahakikishe kwamba wanapata. Naishukuru sana Kamati kuzungumzia masuala ya pembejeo na tumezoea watu wanaostahili kupata pembejeo ni wakulima tu. Mheshimiwa Waziri, tulikutegemea sana ulipoletwa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, kwa sababu ulikuwa na historia nzuri sana katika Wizara ulizotoka na bado tunakutegemea, unaweza ukafanya mambo mazuri katika Wizara hii hasa kwa vile na wewe ni mfugaji na mvuvi; kwa hiyo, tunategemea kwamba unaweza ukafanya mambo mazuri hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala zima la elimu kwa wafugaji. Hawa wafugaji wanastahili wapate elimu kubwa sana kutokana na biashara hii ya ngozi. Kwa sababu wanaona kwamba, kuna wafanyabiashara wanaozunguka kununua ngozi kule mpakani, lakini ngozi zote hizo zinakwenda Kenya kwa kuwa hawajui wapeleke wapi; huku Tanzania na nani ananunua. Mabucha yote wanakonunua mifugo na kuchinja, ngozi zote zinapelekwa kwa sababu huku Tanzania hatuna soko.

Sasa tunahitaji elimu kubwa sana ili tujue kwamba, Tanzania kuna viwanda vya kununua ngozi ili na sisi tuachane na mambo ya Kenya tulete biashara huku na Tanzania ifaidi rasilimali iliyopo nchini. Kwa hiyo, napenda kusisitiza hili suala la elimu; wafugaji wapate elimu wajue kwamba, ngozi ni faida kwa sababu sisi tunahesabu kwamba faida ni nyama tu, ngozi tumeisahau kabisa. Sio kwamba tumesahau, lakini hakuna biashara na wala masoko huku Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuishia hapo na nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi kuhusu Muswada huu wa Ngozi.

Naungana na wasemaji wenzangu kusema kwamba, Muswada huu umekuja kwa kuchelewa sana, kama ambavyo wasemaji wenzangu wameusisitiza. Mimi sikutegemea hata siku moja kuwa itafika wakati ngozi nayo itawekewa Muswada. Mimi ninatoka sehemu za wafugaji ambapo ngozi ni nyingi sana, zinatokana na wanyama tunaowafuga miaka nenda rudi, lakini kwa sababu hatukuwa tunaelewa umuhimu wake, wananchi wamekuwa wakiitupa tu bila kuelewa kwamba, tunapoteza rasilimali nzuri sana ambayo Mwenyezi Mungu alikuwa ametuwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, amesoma takwimu ambazo nadhani Watanzania na wafugaji wengi ambao wamesikiliza leo hii wanaweza wakaona na wakakubaliana nami kwamba, kumbe Mwenyezi Mungu, kila jamii katika maeneo yao kama ambavyo tumesikia wenzetu wa maeneo ya machimboni, wamekuwa na rasilimali yao. Kwa hiyo, hatukupaswa kwa namna yoyote ile kusema kwamba, Watanzania ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi tulipokuwa tunachangia Ripoti ya Jaji Bomani ya kuboresha Mikataba ya Madini jinsi ambavyo italeta manufaa kwa Watanzania, hali kadhalika sasa ni wakati muafaka pia tunapotunga Sheria ama tunapoboresha miswada, tuwe makini kuhakikisha kwamba, bila kufanya makosa sasa tuweke sheria ama tuangalie kwa makini kabisa ili isije ikawanufaisha wageni. Kwa mfano, mimi zamani nilikuwa naona malori yalikuwa yanaingia katika maeneo ya wafugaji yanasheheni ngozi, zinapelekwa Kenya na maeneo mengine ya nchi jirani, nilidhani ni njia mojawapo ya kusafisha mazingira. Hatukujua kabisa kwamba, kumbe wenzetu kama ambavyo tumekwishasikia ni kwamba, walikuwa na viwanda kwa hiyo wanakuja Tanzania ambako sisi tulikuwa hatujaamka kujua kwamba ngozi nayo ina manufaa, wanakusanya kwa wingi malori kwa malori wanapeleka kule kwao wanazitengeneza wanaturudishia kutuuzia sisi lakini zaidi sana wanapeleka nchi za nje ili kuongeza pato la nchi yao bila sisi kunufaika na lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa ni wakati muafa kuhakikisha kwamba, Miswada yetu tunayotunga kuwa Sheria kwa ajili ya rasilimali zetu, itunufaishe sisi. Kama ambavyo tumekwishasikia, bahati mbaya wenzangu wameshaongelea na mimi sina sababu ya kurudia sana, lakini niweze kusisitiza tu pia kwamba Muswada huu ni mzuri sana. Tunaishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa kuweza kuleta Muswada huu, lakini tutoe maoni tu kwamba, iweze kuboresha.

Nimeisikiliza taarifa ya Waziri imeeleza vizuri sana, lakini cha kusisitiza tu ni kwamba ni vizuri zaidi kuboresha ngozi. Hata wakati Rais wetu alipoutembelea Mkoa wa Manyara akijua kwamba ni Mkoa wa wafugaji, alisisitiza sana ufugaji bora; alishauri kwamba ngozi iwe pana ili iweze kupata bei nzuri zaidi. Kwa hiyo, nadhani ni wakati muafaka pia Wizara na Serikali kwa ujumla, ikahakikishe inaboresha zaidi ufugaji ili mabilioni ya shilingi tuliyosomewa hapa, yaweze kuwa mara mbili au tatu ili kuinua pato la taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la zaidi sana tuweze ku-*exploit maximum profit* kutokana na zao hili, kwa sababu mwanzoni mimi nilidhani faida kubwa ya mifugo inatokana na nyama. Kumbe sasa hivi mambo yamegeuka ninaelezwa, sina hakika kama ni kweli kwamba, sasa hivi pato kubwa zaidi ni la ngozi kuliko hata nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Sheria hii pia ingekuwa suala la busara kuwaelimisha wafugaji. Wafugaji wakipewa elimu ya kutosha, kama ambavyo sasa hivi ngozi bado haijaboreka, wakipata elimu ya kutochoma ngozi na nyinginezo, lakini vilevile wakielimishwa manufaa ya ngozi na zaidi sana wakipatiwa soko watahakikisha kwamba, wageni wanaokuja kuiba rasilimali hii hawataweza kuwaibia tena kwa sababu watakuwa na soko la uhakika.

Serikali pia ihakikishe kuwa, tufike mahali kuimalishe viwanda vyetu kwa maana ya kwamba, tuitengeneze ngozi hii hapa hapa Tanzania ili tuweze kupata bidhaa ambazo zitaweza kuuzwa hapa hapa au hata kuuzwa nje na kuongeza pato la taifa. Mimi nashauri kwamba, sambamba na kutunga Sheria hizi na kurekebisha mikataba hii kuhusu rasilimali zetu zinazonufaisha nchi yetu, vilevile taratibu hizi ziwekewe Sheria ziweze kulenga kuwanufaisha wale watu ambao wanashughulika na rasilimali hizi moja kwa moja.

Kwa mfano, juzi tumesikia kila mmoja kutoka maeneo ya madini wanasema wale walioko pale wananufaika na nini. Basi nadhani ni wakati muafaka pia na wafugaji nao wawe wanalengwa ili hali yao iweze kuboreka kwa haraka, kwa sababu wafugaji wapo nyuma sana kielimu, kiafya na mambo mengine. Kumbe wanazo rasilimali ambazo taifa linaweza likawasaidia kwa kuwaboreshea maisha yao ili na wao wapate maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la MKUKUTA ambao unasuasua kwa miaka mingi na ambao hadi leo hakuna taarifa sahihi ya kusema umefanikiwa kwa asilimia ngapi. Kumbe katika kuibua kufikiria na kuweza kuboresha mikataba na Sheria kwa rasilimali zetu, kutahakikisha kwamba, suala la kupambana na umaskini Tanzania, linaweza kufanikiwa kwa asilimia mia moja kwa kuboresha namna ya kuzilinda rasilimali zetu hizi ikiwepo rasilimali ya ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikuwa na mambo mengi ya kuchangia na baada ya kusema haya machache, nimalizie tu kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jina langu ni John Paul Lwanji.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa John Paul Lwanji, kwa kuweka rekodi vizuri.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia naunga mkono Muswada huu na mawazo yangu hayatofautiani na wenzangu waliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo Afrika, ukiacha Ethiopia na Sudan. Tumearifiwa kwamba, tuna viwanda vyetu sita vya ngozi hapa nchini na ukiangalia sana viwanda hivyo vipo hoi. Hatuko makini kwenye biashara hii na hilo ndilo tatizo tulilonalo na hatukuchukua hatua makini za kuweza kudhibiti magendo ya biashara hii. Kama tulivyosikia wenzetu hapa kwamba, ngozi nyingi, lakini hata mifugo yetu inaibiwa na kupelekwa nchi jirani na nchi hizi ndizo zinazonufaika zaidi kuliko hata sisi wenyewe. Hilo mimi ninashauri kwamba, Serikali ichukue hatua za makusudi kabisa za kudhibiti magendo au matatizo ya hii biashara ya ngozi ili tuweze kunufaika na hii biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningesisitiza pia kwamba, haya matatizo ya athari za ngozi zinazotokana na chapa inayowekwa kwa moto, kupiga fimbo mifugo kwa mfano wakati wa kuwafundisha kulima ng'ombe wanapigwa sana, kutothamini mifugo kwa ujumla na tumesikia pia wengine wanatumia ncha kali. Kwa kweli wanyama wanayapata mateso makubwa. Sasa huwezi kupata ngozi bora kwa vitendo hivi na Muswada huu hauzungumzii vitendo hivi vinadhibitiwa vipi. Inazungumzwa habari ya uchunaji ngozi wakati ngozi hiyo haijaondolewa kutoka kwa mnyama; ni hatua gani zinachukuliwa ili kuweza kudhibiti vitendo hivi? Sasa matokeo yake ni kwamba, tunakuja kupata ngozi ambayo si bora. Hii ni kutokana na mila au makabila fulani, ukikuta ng'ombe anapowekwa alama kwa kweli inatia huruma.

Huyu ng'ombe anapokwenda sokoni mkazo wake ni nini hasa? Mkazo wake ni nyama tu basi. Sisi tumeona mara nyingi watu tunakimbilia kuchinja ng'ombe, mbuzi au kondoo; *we are interested with meat* lakini ngozi mara nyingine utakuta hata mbwa anaweza akawa anaiburuza tu na watu hawajaona umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naona mbali ya kuwa na huruma juu ya hao wanyama, ili tuweze kupata bidhaa bora nadhani Serikali ingejaribu kuangalia pia kwamba; je, kuna faini yoyote inayoweza kutozwa kwa hawa watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomchoma ng'ombe kutoka miguuni mpaka kwenye nundu, maana yapo makabila yanafanya hivyo; nadhani ingekuwa ni vizuri kwamba, waweze kuelimishwa na pale ambapo hawawezi kuelimika, basi zichukuliwe hatua za makusudi ili kuweza kurekebisha hii hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeomba wafugaji wafundishwe ni sehemu gani za kupiga chapa, kuweka alama kama ni kwenye masikio kidogo basi. Sasa hawajui na wanafuata *traditions* zao za zamani, zaidi wao wapo *interested* na hiyo nyama, pamoja na usalama wa huyo mnyama, anadhani akimuweka alama nyingi ndiyo hawezi kuibwa. Zipo alama ambazo kitaalam kama zitawekwa, basi wanaweza waka…

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wafundishwe hiyo kwamba, ngozi ni *source of income*. Hawana habari hiyo, hivyo wafundishwe kabisa. Mimi naunga mkono kwamba, usindikaji wa ngozi utiliwe umuhimu badala ya kukimbilia kuuza *raw*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumesema ni nchi ya tatu, lakini hatuna viatu vya kutosha, hatuna mikanda, hatuna makoti ya ngozi kama wenzetu wanavyofanya. *Ironically* ni bidhaa hii hii inayotoka hapa nchini ndio inakwenda kutengenezwa huko vitu na tunarudishiwa tena sisi wenyewe kuweza kuvinunua. Sasa ningeomba hatua za makusudi zichukuliwe ili wananchi au watu walio katika sekta hiyo, waweze kufundishwa mambo yote hayo na tuweke viwanda vya kutosha ili tuweze kusindika. Tutapata bei kubwa na nzuri zaidi kama tutasindika hapa nchini, badala ya kuuza ngozi tu nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na mengi, lakini nasisitiza tena kwamba, bado biashara hii tunaidharau, hatuitilii mkazo. Watu wetu hawajafundishwa vizuri kwamba hizo ngozi ni *source of income*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kuna mtu mmoja aliuliza swali hapa juu ya ukatili wa wanyama. Mimi nasisitiza kwamba, vitendo hivyo vidhibitiwe, tuvikemee na tuviwekee sheria au adhabu ambazo zinaweza zikadhibiti vitendo hivyo ili tuweze kupata bidhaa ambazo ni bora. Kwa hiyo, si vyema kuendesha vitendo kama hivyo tulivyosikia juzi kwamba, kuna watu wananing’iniza kuku. Mifugo ndio kabisa, hata inapobebwa kupelekwa sokoni au inaposafirishwa kutoka Mikoani kupelekwa Dar es Salaam kwa ajili ya masoko kule, utakuta mifugo hiyo inawekwa katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaposafirisha mifugo katika usafiri ambao ni finyu, ngozi mle zinakwaruzwa, zinatoboka, unapofika kule hupati kinachotakiwa na si vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusimuliwa juu ya imani moja hapa nchini na nchi nyingine kwamba, maisha hapa Duniani wanaamini kwamba ni ya mzunguko kwamba, ukifa basi roho yako inahamia kwa binadamu mwingine unazaliwa mnyama. Sasa wewe kama ni katili sana, unapiga ng’ombe, unachinja na hivi, basi ukifa na wewe utakapokuja kuzaliwa unazaliwa ng’ombe ili na wewe uwe *subjected* katika hali hiyo. Kama wewe ni mchinjaji wa kuku sana, unatesa, basi na wewe utakuja kuzaliwa kuku. *It is a circle!* Sasa ukiwa mstaarabu, unawatunza vizuri na nini, basi ukija kufa unazaliwa nchi nyingine, lakini unazaliwa binadamu. Wewe kama matatizo yako ni kutesa, kukanyaga wadudu, panzi; basi na wewe utakuja kuwa *subjected* katika hali hiyo hiyo.

Hiyo dini nadhani ingefundishwa vizuri watu waweze kuelewa hivyo kwa sababu si vitendo vizuri. Kitu chochote utakachokitunza ni lazima kitakuzalishia; kama hukitunzi unaki-*neglect, definitely* utapata hasara na matatizo nayo yatakukumba kama wenzetu ambavyo wanaamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninasisitiza kwamba, Muswada huu umekuja wakati muafaka na kwa kweli umechelewa. Tunaomba upitishwe ili tuweze kunufaika na biashara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Paul Lwanji, nakushukuru sana na hiyo falsafa yako mpya ya leo; ukimtesa mdudu ukifa utazaliwa mdudu. Sasa sijui Mabwana Afya wanaoua inzi kwa wingi wakifa itakuwaje, naona wote watakuwa mainzi!

Tunakushukuru leo umetupa changamoto ya kuwatunza wanyama na kutunza ngozi za wanyama wetu kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Muhammad Sanya, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa.

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa asubuhi hii kupata nafasi ya kuchangia huu Muswada ambao umechelewa, lakini umefika. Inabidi tuuchangie kiasi ambacho siyo tu kuhifadhi na utengenezaji wa ngozi kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunaambiwa kwamba ni ya tatu, lakini mimi siamini hivyo, kwa sababu hata hiyo sensa yenyewe hatuambiwi imefanyika mwaka gani. Kuna watu wana mifugo wengi tu hapa, lakini hawajafika maofisa angalau kuhesabu mifugo yao ni mingapi. Tatizo kubwa tulilonalo ni ukiritimba tu, siyo kuhofia gharama kwa sababu kuna mambo mengine yanakuwa na gharama kubwa kwa Serikali na yanafanyika, lakini haya muhimu ya kulipatia tija Taifa letu, hayafanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano mmoja mdogo tu mzuri; hivi karibuni ilitokea *volcano eruption* kule sehemu za Arusha. Kuna kijiji kinaitwa Naiyopi, hebu tujiulize; ng’ombe wangapi walikufa pale kwa kukosa malisho? Bahati nzuri hakuna athari iliyompata binadamu na kufa, lakini wanyama walipoondoshwa katika eneo lile kutokana na chumvi chumvi zilizoingia katika majani ambayo ni malisho ya wanyama wale, ikabidi wahamishwe. Katika uhamishaji ule, walikufa ng’ombe wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe makini katika suala zima la ufugaji. Wafugaji wanapata *priorities* gani kutoka Serikalini? Wametengewa maeneo gani? Leo wafugaji wanapigana na wakulima mpaka baadhi ya Watanzania kupoteza maisha yao, kwa sababu tu ya kukosa hifadhi bora na maeneo bora ya malisho ya wanyama tuowafuga na maeneo ya wakulima. Tukiwa makini kwenye suala hilo, ndio hapo tutaanza kuhifadhi ngozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Botswana inachangia zaidi ya asilimia 30 kwa uzalishaji wa nyama tu. Sisi tunaambiwa ni wa tatu, tunachukulia Ethiopia ni *number one,* lakini Ethiopia imegawanyika, kuna Ethiopia na Eritrea. Inawezekana wao tunawapita kwa idadi ya wanyama wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitakwenda zaidi ya hapa ambapo tunazalisha. Tunazalisha ngozi, wasimamizi wa ngozi wako wapi? Maofisa kutoka Wizara hii wanafanya kazi gani ya kuwahimizza wafugaji ili waelemike na utunzaji bora wa ngozi ya wanyama ambayo tunaweza tukasafirisha. Mimi naitaka hii Wizara, pamoja

na Serikali twende mbele zaidi. Tanzania leo sisi sio wa kuagizia viatu kutoka nchi za nje, tena viatu dhaifu kabisa kabisa. Unakinunua Kariakoo, mpaka ukifika Ilala kama unakivaa soli unaiacha njiani. *Yes*, ni maplastiki tu, lakini sisi kama tungekuwa tumejikita katika uzalishaji bora wa ngozi na baadae tukafufua viwanda vyetu ili tukazalisha viatu, tukazalisha mikanda, mabegi ya akina mama, tukaweza kutumia humu ndani ya nchi na vingine kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano bora katika Bara la Afrika ni Egypt. Egypt hawana uzalishaji mkubwa wa wanyama, lakini leo wanasafirisha viatu tena *one of the best shoes.* Nenda Italy, viatu vyao vimejaa Dunia nzima. Nenda Vietnam wanatengeneza viatu mpaka vya Clarks leo. Zimbabwe kwa bahati mbaya tu ya kiuchumi na matatizo ya kisiasa, lakini ilikuwa ikisafirisha viatu. Walikuwa wakitengeneza *Clarks, Hushpuppies*. Twende Kenya, nchi jirani ambayo haina ng'ombe kama Tanzania, wanatengeneza *Safari Boots* ambazo ni ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda Uingereza, unataka kununua kiatu cha *Clarks* ambacho ni *genuine leather* ni zaidi ya Paundi 75. Nigeria wamepiga marufuku kuagizia viatu kutoka Thailand, wanatengeneza viatu vyao wenyewe. Sasa na sisi tufufue viwanda vya kuweka hadhi ya ngozi yetu, lakini na wakati huo huo na si mara moja, mara mbili/tatu nalizungumzia suala hili; mabenki yetu yawakopeshe watu au vikundi vya watu walio na mwamko wa kibiashara wa kufungua viwanda vidogo vidogo vya kusindika, kuanzia matunda na ngozi. Tunaweza kufanya hivyo, tukawa na *Farmers Bank*.

Jana Mheshimiwa Waziri wakati tunapitisha Muswada wa *Mortgage Finance* alisema kutakuwa na *Land Bank*. Sasa tukiwahamasisha wananchi wetu wakawa na mtaji mzuri, tukaagizia *designers* kutoka nchi kama Thailand, Vietnam, Egypt, India, wakaja hapa tuka-*process* ngozi, halafu tukaongeza thamani zaidi ya kutengeneza viatu, tunaweza tukauza viatu ndani ya nchi na vingine tukasafirisha nje ya nchi. Hili linawezekana kabisa kabisa; kwa nini lisiwezekane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo magari yanatumia *genuine leather* katika *seat covers* zao, masofa haya *genuine leathers* yanatengenezwa Duniani, sisi tunatengeneza ngozi tunawapelekea wao. Kwa nini sisi tusiingine ubia na watu kama hawa, tukahamasisha wakaja wakafungua viwanda katika nchi yetu na tukaweza na sisi kuitangaza Tanzania kwamba ni kweli nchi ya tatu ambayo ina wanyama wengi kuanzia ng'ombe, mbuzi na kondoo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda China; China wanasafirisha viatu vingi sana. Mimi kuna wakati mmoja kuna mfanyabiashara pale Zanzibar aliagizia viatu kutoka China, akaulizwa na Wachina unataka viatu vya ngozi ya Mbuzi au ya Nguruwe? *Yes*, yule Bwana kwa maadili yetu ya Kiislamu, akawaambia tunataka vya ngozi ya mbuzi na akaleta viatu vya ngozi ya mbuzi ambavyo huwezi ukavipata mahali pengine popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda Canada, Uingereza, unakuta viatu vinatoka India. India wao wana ng'ombe lakini kutokana na itikadi zao za kidini,

hawaruhusu ng'ombe kuchinjwa, lakini wanasafirisha ngozi, sijui ngozi ya kitu gani na wanaipata wapi? Wanatengeneza viatu. Kwa hiyo, sisi tutakapokuwa *serious*, tukitaka kuinua uchumi wa nchi hii, kuna mambo madogo madogo yana tija zaidi hata kuliko kuvamia maeneo tukaenda kuchimba madini, tukasafirisha mbao zetu bila ya kutengeneza *furniture, why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, meza hii hapo mbele yako imetengenezwa kwa mbao ya Tanzania. Hii hapa na ni mbao safi kabisa na ni meza nzuri tu, lakini maofisi ya Serikali yote, kuanzia Bunge mpaka Mawaziri; yamejaa *furniture* kutoka Malaysia. Ajabu kubwa sana, tusafirishe magogo, halafu tuletewe viti; umeona wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeutwanga mwenyewe mpunga ukatoka mchele, halafu unakushinda kuupika unaupeleka ukapikwe Jamatini uletewe nyumbani! Umefika wakati tuamkeni vichwa, tusiamke miguu! Ukiamka miguu utatoka tu utembee, urudi, hakuna tija yoyote. Amka kichwa, ufungue kichwa chako. Tuwaite watu wenye mitaji, watakuja na *capital*, watakuja na viwanda, watatoa ajira. Wao watakuwa ni wasimamizi kutokana na *capital* yao, lakini ajira itatoka kwetu, viwanda vitakuwa katika nchi yetu, tutaitangaza nchi yetu kusafirisha bidhaa hizo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningesisitiza Tanzania sasa tusiwe mahodari wa kutunga Miswada tukaipeleka Bungeni, ikaletwa hapa tukaipitisha, halafu haifanyiwi kazi. Njia ya kuihifadhi ngozi ya wanyama wetu tuliyokuwa nayo ni nzito, lakini ni rahisi. Tuchukulie mfano mmoja mdogo tu; hawa wafugaji wetu wanaweka alama za moto katika miili ya ng'ombe; kwa nini tusiweke utaratibu wa ku-*stitch* kwenye masikio kama wanavyofanya nchi nyingine kunakuwa na *lebel* tu kwenye sikio, ana-*stitch* akishamwona kwamba huyu ni ng'ombe wangu na sikio halitoi chochote katika bidhaa ya ngozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kibegi kidogo cha akina mama ambacho wanabeba mkononi kinafika mpaka *300 Dollars, genuine leather. Yes!* Angalia kile kibegi kinachukua mita ngapi ya ngozi ambayo imetokana na mnyama? Kwa hiyo, mimi nasisitiza tu kwamba, Tanzania tusiwe mahodari wa kuleta Miswada hapa halafu tusiifanyie kazi, lazima sisi tuamke kibiashara. Tumeingia katika soko huria, tusijaze viatu vibovu katika nchi yetu, tukaacha ngozi yetu isafirishwe ikatengenezwe viatu, halafu viatu virejeshwe hapa. Tuchukue mfano tu, tutoe watu waende kuona na ziundwe Kamati za Bunge zifanye hizi kazi. Kwa kila maeneo ambayo kuna wafugaji, watafutwe wafugaji, wasafirishwe waende wakaone kuna soko gani, wanaweza wakaingia ubia na kampuni gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Vietnam wanatengeneza viatu vya Clarks, vipo Tanzania. Kuna Viatu kutoka Egypt, kutoka Kenya, Italy, Uingereza, Marekani na kiatu kimoja kinakwenda mpaka *200/300 Dollars* na sisi ndivyo tunavyovaa humu Bungeni na wananchi ndivyo wanavyovaa. Walalahoi wananunua kiatu kwa shilingi 30,000/40,000, baada ya mwezi mmoja hakionekani; soli iko mbali, nyuzi mbali na kiatu mbali. Si kiatu ni *fake* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuamke kibiashara, tukishaandaa huu Muswada ukishapita, iandaliwe na mikakati bora ya kuwaelimisha wafugaji na wafugaji wapewe *privileges* fulani kwa ajili ya kuhifadhi ngozi ili tusafirishe kwa ajili ya kupata ngozi ya kutengenezea bidhaa katika nchi yetu ya Tanzania. La sivyo, tutakwenda na kuvaa bidhaa za nje na kusafirisha bidhaa ambazo sisi wenyewe tunaweza tukazitengeneza. Kuna ubaya gani kuagizia *designers* wawili au watatu kutoka Thailand, ukawa-*provide facilities*, ukawapa nyumba, ukawapa mishahara mizuri, ukawaambia haya vijana wangu 300 hawa wapo Dodoma, tengeneza viatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa nacho kiwanda cha Bora hapa, kimekwenda wapi? Kwa nini kimekufa? Hatuwezi kuvaa viatu vyetu mpaka tuvae viatu vya nchi za nje? Hapana! Tujenge imani kwamba na sisi tuna uwezo wa kutengeneza bidhaa tukazitumia wenyewe na nyingine tukasafirisha nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nimesikia suala kuhusu usindikaji wa matunda kwamba, kuna viwanda viwili/vitatu vinasindika matunda. Je, kuna udhibiti gani wa kutokuagizia bidhaa ambazo zinaagizwa katika nchi? Kwa sababu ni soko huria, juisi za maboksi zinatoka Afrika Kusini, zitoke Kenya? Kama ni bidhaa huria unaruhusu viingine ndani, punguza kodi ya viwanda vyako vya ndani iwe na *competition* nzuri ili bidhaa ya ndani iweze kupata soko, bidhaa ya nje isije ndani. Umeme bei kubwa, kodi zimepanda, wanaotaka kufungua viwanda wanashindwa. Lazima tuandae mikakati sasa ya kupunguza kodi na kupunguza gharama za umeme ili viwanda vizalishe, viwe *competitive* na bidhaa zinazotoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yalikuwa ni mafupi tu yangu hayo, lakini nasisitiza tena na tena kwamba, tusiishie kuhifadhi ngozi, twende zaidi ili tuweze kutengeneza bidhaa zinazotokana na ngozi kwa manufaa ya Watanzania na kwa ajili ya kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Sanya, kwa mchango wako mzuri. Ninaamini mpaka kule Comoro leo wamekusikia kwa huo mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa na Mheshimiwa Kaika Telele ajiandae.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niseme machache tu. Kwa ujumla, Muswada huu naukubali na nauunga mkono hata kama umechelewa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kila aliyesimama na kuzungumza, tunazungumzia hii ngozi, wengine wametaja idadi ya ng’ombe waliopo, mbuzi, kondoo na thamani ya ngozi na namna tunavyopoteza. Msemaji wa mwisho Mheshimiwa Sanya, ameweza kutoa namna gani tunavyopoteza na tunavyotumia vifaa vya ngozi hasa viatu, mikoba ya akina mama, majaketi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama kuna kasoro fulani katika Muswada huu. Sasa katika kasoro hizi, nitalazimika kwanza niende niitizame Wizara yenyewe; hii ni Wizara ya Ufugaji na Uvuvi. Katika kubaini, nikatafuta *definition* ya hii *skin* inayokusudiwa hapa, nikaangalia *skin means the raw skin of mature or fully grown animal of the smaller kinds including sheeps, goats, pigs, reptiles, birds and fishes or the immature animals of larger species including cows*. Kwa hiyo, nikakuta kumbe huu Muswada haujakosea, samaki wamo, ngozi ya samaki imo, lakini kila anayesimama anazungumzia ngozi kwa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi yetu ya Tanzania, tuna wavuvi kuanzia Ukanda wa Mtwara mpaka Tanga na Visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia huko wapo wavuvi si chini ya milioni nne na nusu au milioni tano, achilia wavuvi wa kwenye Maziwa huko, wa Ukanda huu wa Pwani tu. Mheshimiwa Rais, alipounda Wizara hii akasema iwe Wizara ya Ufugaji na Uvuvi, alikuwa na maana kamili kwamba, muda mrefu Tanzania imekuwa ikijali ufugaji wa sehemu ya juu au wanyama wa juu juu, lakini samaki na wanyama wa baharini ilikuwa haujafikiriwa. Kwa hiyo, huu Muswada ukiuangalia kumbe umefikiria na samaki wamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baharini kuna ngozi ya samaki na hawa samaki wapo wa aina nyingi, ambao wanatoa ngozi na ngozi za samaki nazo zina thamani. Kuna samaki Nduwaro anatoa ngozi nzuri, lakini inatupwa. Ukienda *Ferry* hapo, inachunwa ngozi inatupwa. Kuna Chewa, ngozi yake ni ya thamani kubwa sana Duniani na mpaka hivi karibuni Mashirika ya Kimataifa yalipiga marufuku kuchuna ngozi ya Chewa. Kuna Taa, kuna Songoro, ni samaki mtamu sana, zamani alikuwa analiwa na Mfalme tu. Songoro ana ngozi nzuri sana. Kuna Papa, anatoa ngozi na mapezi, hayo mapezi huyanunui, kilo moja sasa hivi inakwenda kwa shilingi 120,000; mapezi ya Papa, kitu kidogo. Yanaitwa mapezi ya Papa, hamyajui, bahati mbaya! Mapezi ya Papa, Mwenyekiti yanauzwa …

**MWENYEKITI:** Labda Mheshimiwa ungetoa ufafanuzi, maana huo ni msamiati mpya. Tusaidie kwa kuutolea maana kuliko kwenda hivi hivi.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitafafanua, pezi la Papa; kasikia mapenzi yule? Pezi siyo mapenzi! Papa ana vitu vimekaa kama mbawa za ndege hivi mgongoni. Sasa vile vilivyochomoza mgongoni, vikikatwa vina thamani kubwa sana Duniani, ndiyo pezi lile, siyo mapenzi. Kwa maana hiyo, Muswada huu umefikiria pia, lakini je, Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, imehamasisha vipi mambo kama haya?

Ukienda *Ferry* pana ngozi tele zilizochunwa zinatupwa pale na ni kitu ambacho leo Wizara haijafanya juhudi za kutosha za kutoa elimu na matumizi halisi ya ngozi hizi za samaki niliowataja ambazo zina thamani kubwa Duniani. Leo tunapoteza, zinatupwa bure. Ukanda wote wa Pwani ngozi hizi zinatupwa bure.

Kwa maana hiyo, wakati leo tunalalamika ngozi za ng'ombe, mbuzi na nyingine hatuzitumii vizuri, basi angalau huko tuna afadhali kuliko tukienda Ukanda wa Pwani, tunazitupa ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Wizara hii sasa kuielimisha jamii na kama kutafuta masoko, basi yatafutwe masoko ya ngozi za samaki mbali na wale wanyama wa baharini. Kwa hiyo, upungufu huo, nafikiri Waziri autilie maanani na uangaliwe kwa jicho la huruma, kwa sababu wakati tutakapohimiza ndugu zetu Wamasai wafugaji na ndugu zetu wa Ukanda wa Pwani huu wapo wengi mno na wao ni Watanzania na wangehitaji kupata kipato au vipato ya hali ya juu.

Kwa maana hiyo, kama leo tunafikiria kufufua viwanda vya ngozi hizo za wanyama, basi tutafute na uanzishaji wa ngozi hizo za samaki ili zisipotee bure na wavuvi wetu waweze kufaidika, siyo kitoweo tu bali na ngozi ziweze kuwafaidisha. Kwa hiyo, hiyo ndiyo ilikuwa mada yangu ya kwanza ambayo ina umuhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ngozi ambazo sijui kama zinatajwa humu au zinahusika na Muswada huu. Kwa mfano, ngozi za Chatu, tunategemea hii ni mali asili, ngozi za Mamba. Sasa ikiwa hazitajwi, nazo tukazihusisha, basi kidogo kuna makosa kwa sababu sasa hivi kuna ufugaji mkubwa wa Mamba, nyote mnafahamu. Wakati kuna wenzetu wanafuga Mamba na Mamba yule ngozi yake ina thamani sana Duniani na inahitajika sana, lakini ikiwa hatukuitilia maanani, je, wale wanaofuga Mamba ambao ni matajiri wakubwa au wafanyabiashara wakubwa wanatoka Kenya Canirval kule wanakuja kununua hawa Mamba, zile ngozi wakichuna wapeleke wapi, tuwafaidishe nchi jirani tu?

Tunaweza tukauza kitoweo cha Mamba kutoka Tanzania, ngozi zile tukachuna, tukazihifadhi sisi. Kwa hiyo, Ngozi za Mamba, ngozi za Chatu na ngozi za nyoka wa kawaida zote ni vitu ambavyo vina umuhimu, vitiliwe maanani. Pamoja na kwamba, hivi vitu vingine vipo katika Wizara ya Maliasili, lakini vinahusika huku pia. Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na la mwisho, nilikusudia kuuliza kuhusu Kiwanda cha *Tanneries* kilichobinafsishwa cha Mwanza. Tuna malengo gani ikiwa mwekezaji hivi sasa amefanya kama stoo tu? Ile faida ya madhumuni na malengo ipo vipi? Vipo vingi si cha Mwanza tu; je, Mheshimiwa Waziri, baada ya kupitishwa Muswada huu leo, atatuahidi vipi kwa vile viwanda vyote na wakati huo sasa thamani itakuwa ipo juu na Watanzania watakuwa wameshapata njia nzuri, wameshaboreshewa faida ya ngozi; je, viwanda vile vilivyobinafsishwa na havifanyi kazi ile tutafanya vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema machache kuhusiana na Muswada huu wa Ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Wataalam na Kamati ya Bunge inayohusika, wamefanya kazi nzuri. Nataka tu nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Magufuli kwamba, wanavyomwita kwamba ni Waziri wa Kitoweo wala asikasirike, angalau ni kati ya Mawaziri wenye chakula cha kutosha. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa ngozi, sisi huko masaini na wafugaji wengine wengi wakiwemo Wasukuma, tuna ile hali ya jadi ya kuibiana mifugo na alama ambayo tunaweka kwenye ngozi ni kwa sababu tunataka itusaidie kutambua mifugo inayoibiwa. Kitengo cha Serikali cha miaka mingi cha *Stock Safety Prevention Unity (STPU)* kimekufa, mimi sijui kiko wapi na kwa hiyo, wafugaji wenyewe ndiyo wanachukua jukumu la kufuatilia mifugo yao inapoibiwa wala siyo Serikali. Labda Waziri atueleze baadaye, lakini mimi naona kama hakipo. Kwa hiyo, hii habari ya kuweka alama kwa kweli ni namna tu ya kuweza kutambua, ukifuatilia mwenyewe kama mfugaji wa kawaida, mfugaji mdogo, unaweza ukafuatilia kwa kufuatilia nyayo, unatumia pia alama unayoweka kwenye ngozi ya mifugo au hata kwenye masikio ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lawama ikitupwa moja kwa moja kwa wafugaji siyo kuwatendea haki; kwa sababu hata hizo ngozi kuna utaratibu gani, nani hasa ananunua katika mfumo na utaratibu mzuri uliowekwa na Serikali, kama siyo walanguzi na watu wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya mifugo hakuna miundombinu ikiwa ni pamoja na machinjio, viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na hasa zao la ngozi. Tunaambiwa kuna viwanda karibu sita ndiyo vinafanya kazi, lakini katika kiwango cha chini sana; asilimia 30 hadi 50, ndiyo maana watu wanapouza mifugo yao, kama mfugaji wa kawaida, ukishauza madume yako kumi, basi ndiyo hivyo umepata hela yako unaachana na kila kitu, huna habari tena na ngozi. Walanguzi wakishanunua wanapeleka Kenya kuliko na bei kubwa zaidi na kuliko na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku za karibuni ngozi imepata soko sana. Inaonekana vitu ambavyo kama alivyosema ndugu yangu, Mheshimiwa Laizer, Mbunge wa Longido kwamba, bidhaa za ngozi ambazo zina bei kubwa sana sasa hivi ni vitu ambavyo vinatokana na ngozi. Kwa maana ya wafugaji wadogo, wenye mifugo yao huko nyumbani, soko lao ni ndani wanajitosheleza kwa soko hilo. Ukichinja ngombe unatumia ile ngozi kuwa godoro, kitanda ni kila kitu. Kwa hiyo, tunajitosheleza kwa matumizi ya ngozi, lakini kitaifa kwa kweli hatujafikia mahali ambapo tunauza hizo ngozi tunapeleka nje zinasindikwa vizuri na baadaye kuuza hata kwa fedha za kigeni. Kwa wenzetu ambao wana viwanda vya kutengeneza hivyo vitu vya bei ya juu, basi hizo ngozi zikishakamilika zinarudi tena huku kwetu tunauziwa kwa bei ambayo ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ugonjwa unaitwa *lampskin disease;* ugonjwa huu unaharibu sana ngozi za mifugo na ni ugonjwa ambao wenyeji wana tiba yao wenyewe na hasa Wamasai; kama Wasukuma hawajui basi wafike kwetu tutawaambia tutawapa hiyo dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dawa ambazo zinatengenezwa na viwanda, lakini hazifiki kule kwa wafugaji. Lazima uwekwe utaratibu tuweze kupata hizi dawa, zinaweza kusaidia kutunza ngozi ya mifugo yetu, pamoja na hiyo *local knowledge* ya kuzuia ugonjwa wa ngozi tupate na hizi dawa ambazo ni za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma wafugaji wa jamii ya kimasai, katika mambo ambayo yaliwafanya watengeneze urafiki na wasomali ingawa walikuja kutugeuka baadaye ikawa balaa. Ilikuwa ni kwamba; wanatuletea dawa ya mifugo katika maboma yetu ya ng'ombe na wanatuuzia kwa bei ambayo ni ndogo sana. Tunaweza kutumia ile *barter system*, tukabadilisha bidhaa kwa bidhaa. Hiyo ilitusaidia sana wakati huo, lakini pia walikuwa wanakuja kuchukua ngozi nyumbani. Wanakuja na punda wengi wanapakia ngozi wanapeleka wanakokujua wao na wamasai wao, hawaulizwi kwamba unapeleka wapi, ilimradi tu wanawapa ngozi wanaondoka. Baadaye mambo yalipoharibika walipoanza kuchukua mbuzi wetu wazuri na kuchinja kwa lazima na pengine kuchukua na wake zetu, ikawa ni balaa, ikawa ni mgogoro moja kwa moja. Tunaishukuru Serikali wametusaidia, maana walikuja na silaha kali, tungeweza kukabiliana nao lakini walikuwa na silaha basi Serikali ikatusaidia. Nafikiri sasa wakija, watakuja kwa utaratibu mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine kwa kweli tukiona mifugo imefungiwa yale majembe ya kulima, tunaona kama huu ni ukatili kwa wanyama. Lakini inasaidia kwa wale waliobuni hiyo badala ya kulima kwa jembe la mkono hufiki mbali sana, lakini kwa jembe la kukokotwa na ng'ombe, unalima eneo kubwa. Sawa na hii Sheria ya Wanyamapori, ambayo tunaambiwa sisi wafugaji tusitembee na sime kwenye game *control areas*, haiwezekani; sime kwa mmasai au kwa mfugaji ni kama nguo tu uliyovaa. Unapomwambia kwamba, asitembee nayo, haitawezekana, lakini basi hiyo sheria tutaijadili katika Bunge lijalo la Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Sanya, alizungumzia juu ya volkano iliyotokea Mlima Lengai huko, ni kweli ilileta madhara makubwa sana kwa mifugo, wanyapori na hata watu. Kwa sababu binadamu wana uwezo wa kuondoka haraka, basi hakuna madhara yaliyotokea kwa watu, lakini kwa maana ya mifugo na wanyamapori, ile volkano kwa sababu ilikuwa inachukuliwa na upepo kwa hiyo inapotua kwenye ardhi au inapotua kwenye mgongo wa mnyama awe mfugo au mnyama wa porini, ile ngozi inanyonyoka, nywele zake zinanyonyoka na hazitaota tena.

Tuliieleza Serikali juu ya suala hili; Serikali inasema kaeni mbali na Mlima. Volkano ile pia imeleta neema kubwa sana; inaonekana kwamba ile volkano baada ya kutulia juu ya ardhi na mvua ikanyesha, basi imekuwa kama ni *urea* kwenye shamba lililolimwa vizuri. Majani na uoto wa asili umeota vizuri sana na kwa hiyo, mifugo yetu sasa hivi yote imehamia tena Nayobi. Namshukuru Mungu kwamba, ule Mlima sasa

umeacha na ndivyo inavyokuwa kwamba baada ya muda fulani ule mlima unatoa volkano na watu wanakwenda mbali, lakini ikishaacha wanarudi kuendelea na shughuli zao. Kwa hiyo, tunataka kuwaambia Serikali, suala la wananchi kuwahamisha pale wala siyo hoja ya msingi kwa sababu ni tangu miaka nenda, miaka rudi wapo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la wafugaji kwamba, kama alivyosema ndugu yangu Sanya pale, tungelitazama wafugaji katika ujumla wake na mifugo yao na kuona kwamba, wanaendesha uchumi ambao ni mkubwa kama tungeliboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya wafugaji kutoka Ihefu na kuzunguka nchi nzima hii ya Tanzania, kuna mikoa ambayo haiwataki hawa watu, lakini wanataka nyama ya mifugo yao. Kwa hiyo, nataka niwaombe ndugu zangu wa mikoa ambayo hawa wameenda, labda muweke tu idadi ya mifugo mnayoihitaji huko, lakini wapokeeni kwa sababu wanasaidia katika zao hili la mifugo na hasa katika zao la ngozi, ambalo likiboreshwa linaweza kusaidia uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na hayo machache na baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Telele, kwa mchango wako na nafikiri wale ndugu zetu wanaozunguka ule mlima wamekusikia pia.

Waheshimiwa Wabunge, nimwite Mheshimiwa Pindi Chana, msemaji wa mwisho kwa asubuhi hii ya leo, tutakaporejea baadaye tutaanza na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya na yeye ndiye atakuwa msemaji wa mwisho kabisa kwenye Muswada wetu. Kwa hiyo, naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Pindi Chana na jioni tutamalizia na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kama wachangiaji wa mwanzo walivyochangia, mimi nasikitika sitokei maeneo ya wafugaji, natokea maeneo ya wakulima lakini nitashauri tu kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuupongeza Muswada huu muhimu sana katika nchi yetu na umekuja wakati muafaka. Kimsingi, masuala haya ya ngozi ni moja kati ya mambo ambayo yatasaidia kuboresha uchumi na kupunguza umaskini. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni muhimu sana na litafanyiwa kazi kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na sehemu ya pili ya Muswada huu, kifungu cha saba kinaelezea *Establishment in every authority in a council*, sasa ushauri wangu ni kwamba, hii *council* ambayo itakuwa *established* ni muhimu sana Wajumbe wake wazingatie *gender*. Wamesema kutakuwepo na Wajumbe, Wajumbe hao hawajaelezewa vigezo. Vivyo hivyo kutakuwepo na Kamati katika kila kijiji, Kamati itakuwa inashughulikia masuala haya ya ngozi. Kwa hiyo, zile kamati za kijiji zitakuwa na Wajumbe watano katika kila kijiji; vivyo hivyo naomba masuala ya *gender* yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kifungu cha 9(2), kinaelezea majukumu ya ile Kamati ya Kijiji itakayoshughulikia masuala ya ngozi na kwa mujibu wa Muswada huu, inaonekana kwamba, majukumu yake yatakuwa ni kushauri *(advise)*. Ukienda (a) inasema; *advise the village council*. Mimi ningeshauri ili waweze ku-*advise* vizuri; ni muhimu sana wangekuwa wanasaidia kufanya kazi ya *inspection* kwa sababu kwa mujibu wa Muswada huu, kutakuwa kuna inspekta, ambaye atakuwa anazunguka yale maeneo ya *premises*. Neno *premises* limekuwa *defined* katika yale maeneo ambayo yatafanya zile shughuli za ngozi. Wasiwasi wangu ni kwamba, inspekta ambao watakuwa wanazunguka yamkini wakawa wachache; ni muhimu hawa wakaguzi wa masuala haya ya ngozi katika kila eneo, iwe ni kijiji iwe ni wilaya, iwe ni mkoa, wakasaidiwa na zile Kamati za Vijiji zitakazokuwa zinashughulikia ngozi.

Baada ya ile Kamati kukagua katika shughuli zao za kila siku, wao wanaweza kushirikiana na yule *inspector*, kwa sababu mwenye haki ya kuandika *document* yoyote atakuwa ni *inspector*, kwa mujibu wa sheria kwamba eneo hili linafaa kuendelea na shughuli hii na eneo hili halifai. Kwa hiyo, ile Kamati itakapokuwa inashirikiana na huyu *inspector*, ndipo kazi hiyo itafanyika kwa ufasaha zaidi. Kwa hiyo, ni ombi langu kwamba, kifungu cha 9(2) kingeongezeka baada ya (d) kwamba, watafanya shughuli za ku-*inspect premises* wakishirikiana na *inspector* kwa sababu wasiwasi wangu ni kwamba, *Inspector* atakuwa peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimemgusia huyu *Inspector*, basi ninashauri majukumu ya huyu *Inspector* yangeorodheshwa vizuri, kwa sababu wakati mwingine katika utekelezaji wa mambo mbalimbali, utakuta hawa wakaguzi wanakuwa ni chanzo cha shughuli kwenda pole pole; chanzo cha urasimu. Yeye anakuwa na vigezo vyake mwenyewe, sasa ningeomba sana hawa *Inspectors* ambao watakuwa wanasaidia kuboresha na kusaidia kurahisisha shughuli hizi za ngozi, wafanye kazi kwa maadili. Kuwepo na *code of conduct*, kuonyesha *ethics* za *inspectors* katika kila eneo. Isiwe chanzo cha kikwazo kwamba, mkaguzi amefika ame-*council* leseni yangu sasa inabidi tukaonane kidogo. Kwa hiyo, ningeomba sana *code of conduct* ya *inspectors* iwe *very clear*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Muswada huu umesema kwamba, leseni zitakapokuwa zinatolewa kwa ajili ya masuala haya ya ngozi, zitakuwepo leseni za miaka mitatu na za miezi 12. Leseni hizi za miezi 12, ninaungana kabisa, lakini wamesema kutakuwepo na ada; sasa hii ada tuiangalie iwe ni ada ambayo itakidhi uwezo wa wafugaji wetu kulipa, isiwe ada ambayo ni kubwa sana ikashindikana. Maeneo mengi tumeboresha, kwa mfano; zamani leseni za biashara, wafanyabiashara walikuwa wanapaswa kukata kila mwaka na baadaye Serikali baada ya kutafakari ikaonekana kwamba, mtu umeenda kuomba leseni ya duka na mwakani unaenda tena, wakasema mtu ukishakata mara moja basi kunakuwa na *income tax* lakini ile leseni inakuwa *valid* kwa kile kipindi ambacho una-*operate* biashara yako. Endapo unabadilisha biashara *then*, inabidi ubadilishe leseni. Kwa mfano, leseni za mashine za kusaga, leseni za hoteli, zinakuwa *valid* kwa kipindi chote lakini zile ada ndiyo zinaendelea.

Kwa mujibu wa Muswada huu, kila mwaka ukakate leseni, ikifika mwezi kwa kumi na mbili hapo hapo atafute soko, hapo hapo afikirie nikakate leseni, kuna kujaza *form* na kadhalika. Kwa hiyo, kwa sababu tunaanza si jambo baya, ili kuweza ku-*monitor* biashara kwa ufasaha. Tuweke utaratibu mzuri kwamba, ada ya kulipia kwa ajili ya ku-*renew registration* iwe ni ada ambayo inawezekana ikalipwa na mtu yeyote, isiwe ni kikwazo mtu anafanya biashara mwaka mmoja anasema ada yenyewe ni kubwa sana nashindwa kulipa inakuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia juu ya *quality* ya ngozi; ni lazima iwe nzuri. Je, ni jukumu la nani; la Wizara, mfugaji au mfanyabiashara na ni jinsi gani tunaweza kuboresha *quality* ya ngozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine wamekuwa wakifanya *zero grazing* na sisi kwetu tumekuwa tukiomba sana; pale tunapoweza badala ya mkulima au mfugaji au mfanyakazi kuzunguka na mifugo yake kila mahali kutafuta chakula, wakiweza ku-*operate zero grazing* chakula kinapatikana pale pale; ng'ombe wananenepa na ngozi inakuwa safi. Wengine wamezungumzia juu ya kuweka alama za ngozi kwa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya nchi kwa mfano Ufaransa (Paris), ufugaji wao wanaweka *tag* na ile *tag* akienda sehemu inakuwa na *alarm.* Wana-*monitor* kupitia *tag, of course* wao nchi zao wameendelea sana, lakini hata sisi tunaweza kupunguza kidogo alama tukaangalia ni jinsi gani ya kuboresha alama ili ngozi iwe nzuri. Kwa hiyo, tunapokuwa tunaboresha, tuna-*monitor* ngombe au mnyama yeyote, anakuwa na hali nzuri na itasaidia kuboresha viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia yapo masuala mengine kama matibabu; ni jukumu la Serikali ku-*provide* dawa za kutosha; *verterinaries* ambao wanaangalia wanyama. Je, tunao wataalam wa kutosha, tuna-*co-operate* namna gani na nchi jirani kwenye *bilateral cooperation* ili tuweze kushirikiana tupate *donor funded project,* tuone jinsi ya kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine la *training*, *education* na *awereness creation*, kwa wafugaji, wachunaji ngozi za wanyama na vilevile *extension officers* wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeomba sana Serikali ilitafakari na ilizingatie katika bajeti ijayo ni suala la ruzuku. Tumesema tunahitaji kuboresha masuala haya ya ngozi, ni muhimu ikapatikana ruzuku angalau hizi *premises* ambazo tumezitaja katika Muswada huu kwamba kutakuwa na *premises*, maeneo ambayo wata-*operate* biashara ya ngozi, tuwe na *pilot*. Tunaweza kuchagua Wilaya tano au mikoa kadhaa tukajenga *premises,* Serikali iwajengee na inapowajengea si kwamba Serikali inapeleka pesa kwa yule mfugaji, inaingia mkataba. *Procurement* zinafanyika, wanakuja *contractors*, Serikali inamlipa *contractor* tunasema utajenga kwa muda gani, kama utasema utajenga kwa miezi sita, tunakuwa na maeneo ya ku-*open* shughuli hizi. Haya maeneo ni lazima yawe na *quality* ya juu, unahitaji masuala ya *temperature*, *fridge*, kusiwe na joto ngozi itaharibika, unahitaji huduma safi, maji safi yanatoka, vinginevyo huyu mfugaji itakuwa ngumu sana.

Katika *premises* tuwe na *pilot*, tunaweza kukosea, tuanze na *pilot* maeneo kadhaa halafu baadaye wawekezaji watakapokuja, tunaendelea na *Private Public Partnership*. Kwa sasa ningeomba sana Serikali ifikirie ruzuku, jambo hilo lizingatiwe na nadhani Waziri ataweza kusema neno juu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, kuna eneo dogo sana linalohusiana na masuala ya kesi. Katika kifungu cha 25(2) kuna faini mbalimbali, wamesema *fine not exceeding two hundred thousand shillings*. Maeneo mengine kama kifungu cha 32 wamesema *not exceeding one million shillings*. Ningeomba tubadilishe, badala ya kusema 200,000/= tuseme *one million*, kwa sababu 200,000 inaingia ndani yake ili isipelekee Muswada huu kuuboresha mara kwa mara. Leo tunaweza tukadhani zinatosha, kesho zitakuwa hazitoshi; kwa hiyo na eneo hilo lingezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo na nina imani utazingatiwa, naomba kuunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia kwa kipindi hiki cha asubuhi, hauwezi kututosha kwa mchangiaji mwingine yeyote. Naomba tu niseme kwamba, tutakaporudi jioni, msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Dr. Christant Majiyatanga Mzindakaya. Yeye atatumia dakika kumi na tano za kuchangia Muswada huu, halafu tutampa Mheshimiwa Naibu Waziri, naye atatumia dakika kumi na tano za kuchangia na baadaye mtoa hoja Mheshimiwa Waziri mwenyewe, tutampa dakika 45. Baada ya hapo, tutaingia kwenye taratibu zetu za kawaida za kikanuni na za kikatiba za kupitisha Muswada wetu. Baada ya hapo, tutakuwa tumemaliza shughuli ambazo zitakuwa mbele yetu kwa mujibu wa ratiba ya siku hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli yetu ya leo. Naomba niwakaribishe kwa jioni hii, kama nilivyosema wakati nikisitisha shughuli za Bunge; mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na baadaye tutaanza kuwasikiliza Waheshimiwa Mawaziri. Basi namwomba Mheshimiwa Dr. Mzindakaya aendelee na kabla hajaendelea namwomba Katibu aweze kutuongoza.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vile vile nakushukuru zaidi kwa kutamka jina langu vizuri sana. *(Makofi)*

Kwanza, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kusema kwamba, naunga mkono Muswada uliopo mbele yetu kuhusu sheria hii ya ngozi. Pia

naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Magufuli, Naibu Waziri, pamoja na wataalam wa Wizara yao, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Nataka pia niseme kwamba, Mheshimiwa Magufuli, ana haja ya kuona raha kufanyakazi kwa sababu Wabunge wengi tunaamini kuwa ni mchapakazi. Kwa hiyo, tunakupongeza na uendelee hivyo. *(Makofi)*

Kabla sijasema yale machache niliyonayo, nilikuwa nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wengi waliotangulia kusema na hasa Mheshimiwa Ibrahim Sanya na mfugaji mwenzangu, Mheshimiwa Laizer, kwa mambo mawili. La kwanza, ni lile linalohusu pembejeo kwa mifugo. Kama miaka miwili/mitatu iliyopita, Serikali ilikubali kwamba wafugaji wapewe pembejeo. Sisi tukatoa ushauri kwamba, wanunuzi au watakaoingia kwenye tenda wawe ni wale wanaotoka katika Mikoa hiyo husika. Tunashangaa, tabia hii imeendelea kuwepo kwa muda mrefu na mimi ningekuomba Mheshimiwa Waziri uisahihishe hii tabia; kwa nini mtafute watu kutoka Dar es Salaam kwenda kuuza pembejeo au dawa za mifugo Rukwa; hivi kweli kule Rukwa hakuna watu wa kuweza kununua wenyewe wakauziana?

Sisi kule Mkoa wa Rukwa na Mbeya, kapewa mfanyabiashara Mu-Asia hata Kiswahili hajui, anaishi kwa *permit,* ndiyo kapewa tenda ya kutuuzia sisi dawa za mifugo wakati mwenyewe hana hata mbuzi! Sasa hili ni tatizo. Lazima mtazame; sekta ambayo ina watu wanaoelewa wafikirieni na muwape hapa wahudumiane, kuliko kuwaweka watu ambao hawana maslahi na jambo lenyewe. Hilo nilitaka niunge mkono ile hoja ya Mheshimiwa Laizer. *(Makofi)*

Pili, maelezo na ushauri alioutoa Mheshimiwa Sanya, mimi nadhani ungezingatiwa. Ameeleza vizuri, labda mimi nianzie hapo; lakini kabla sijasema hapa nataka nieleze matatizo ambayo tungeji-*address* changamoto zilizoko mbele yetu katika jambo hili.

La kwanza, kama walivyosema Wabunge wenzangu, Tanzania itakuwa ni ya pili au ya tatu kwa kuwa na ng’ombe wengi, lakini pia ndiyo nchi inayotoa ngozi ovyo kuliko nchi yoyote. Sababu ni mbili; ya kwanza hatuna machinjio yanayojulikana. Ng’ombe wanaangushwa huko porini hata katika miji yetu, kwa mfano, sina hakika lakini watu wengi wangefika Vingunguti na kuona machinjioni yake, hakuna mtu ambaye angekula nyama Dar es Salaam.

Sasa nchi kubwa kama Tanzania, mimi natoa ushauri kwamba, tuweke mpango katika kipindi cha miaka mitano na kumi ijayo, angalau kila Wilaya iwe na machinjio ya kisasa ndogo tu, inayotosheleza mahitaji ya wananchi wa eneo hili; watapata nyama nzuri na ngozi nzuri zitapatikana. Vilevile jambo moja ambalo ningependa kulisema na Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwa sababu ni mfugaji; Tanzania yenye ng’ombe ndiyo haikufundisha watu wanaojua kuchuna ngozi. Hatujui kuchuna ngozi. Ngozi nayo ina utalaam wa namna ya kuichuna. Sisi hatujui kuchuna ngozi, maana hatuna vyuo vya kufundisha watu kuchuna ngozi. Hiyo yenyewe ni kasoro *number one*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, malizia kuchuna ngozi za wanyama.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Kuchuna ngozi za ng'ombe na mbuzi. Sawa ni sahihi kabisa. *(Kicheko)*

La pili, ningeomba kama hatuwezi kuanzisha vyuo, vyuo vilivyopo vinavyofundisha wataalam wa mifugo waongeze somo la kumjua mnyama, kumjua ng'ombe na mbuzi, aina za nyama, kwa sababu ndiyo nchi kwenye kanda yetu ambayo haina wataalam waliosomea kukata nyama. Kuna watu wanapata shahada za namna ya kukata nyama ya ng'ombe, ana vitu vingi sana; ana nyama nyingi sana na zina majina, lakini sisi hatuna hao. Kama wapo hawawezi kufika hata wanne au watano. Sasa kwa sababu sekta hii baadaye itakuwa muhimu, tujitahidi kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kusindika nyama, tutaona kama tunahitaji watu hawa tutalazimika kwenda kuwaomba kutoka nje.

Mimi meneja anayefanya kazi kwangu ni Mzimbabwe, kwa sababu tulitafuta hapa Tanzania hatukupata mtu ikabidi tukatafute Mzimbabwe. Mtu anayefundisha kukata nyama nimemtoa Zimbabwe pia. Hapa yuko mmoja tu hapa *VETA,* ningemchukua Serikali ingekosa mtu wa kufundisha. Kwa hiyo, ni mambo ambayo lazima tuanze kuona kama ni changamoto zilizo mbele na tujitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine mimi nilikuwa nataka Waziri atusaidie pia, naomba Serikali ijiingize na kufikiri ubora wa vyakula wanavyokula watu wetu. Mimi nilikwenda sokoni Kariakoo na rafiki yangu mmoja mtu wa nje, nikanunua samaki pale, tuliporudi wakapika yule samaki hakula kwa sababu ya soko lilivyo. Ukienda katika mabucha yetu hapa Dodoma, unaweza usile ile nyama kwa sababu unakwenda unakuta nyama imewekwa kuna nzi hapo na kila kitu hapo hapo. *(Makofi)*

Sasa kazi ya kwanza ya Serikali ingekuwa ni afya ya watu wetu. Watu wanakula aina gani ya vyakula. Tanzania ndiyo tunaongoza kwa wananchi kuuza nyanya sokoni zikiwa chini ya udongo. Hivi hatuoni? Kwa hiyo kwetu kitu kinachoitwa usafi na afya tumeweka pembeni. Kwa hiyo, naomba hili niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada hayo, nilikuwa nataka kushauri kuwa hili zao la ngozi kwa kuwa tumeamua kulitungia sheria, naomba Wizara kwa kuwa Muswada huu utapita, basi watusaidie namna ya kuitekeleza sheria, kwa sababu sheria yenyewe haina maana kama haikutekelezwa. Ikitekelezwa ni wazo zuri sana na nakupongeza Waziri kwa kuona umuhimu wa jambo hili. Utekelezaji ndiyo jambo muhimu sana, likitekelezwa tunaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Mheshimiwa Sanya, alipokuwa anazungumza alizungumzia kuhusu matumizi. *Brother* Waziri wewe unatoka Kanda ya Nyanza, tangu tupate uhuru na kila siku jambo hili mimi nalisema na nitaendelea kusema mpaka nitakapomaliza muda wa Ubunge; hakuna kitu kinachonikera rohoni mwangu

kama sisi kuendelea kuuza *raw material* ya bidhaa zetu. Pamba tunauza nzima nzima, kahawa, kila kitu; nani katuzuia kuanzisha viwanda vya ku-*process*?

Misri kama alivyosema Mheshimiwa Sanya, hawana ng'ombe wengi kama sisi, lakini wanafanya *export* ya viatu na bidhaa za ngozi, sasa sisi wenye ngozi ndiyo tunaagiza kila kitu kutoka nje. Sasa hili jambo ni kichekesho, haliingii akilini kwa mtu anayejua maendeleo. Vitu hivi haviwezi kuja vyenyewe, lazima sera zetu zitufikishe mahali pa kusema ninyi wawekezaji sekta hii lazima muitekeleze.

Viwanda ambavyo vilikuwa vya ngozi, kimoja Mheshimiwa Mwenyekiti hapa nikujulishe, mimi nilipokuwa Wizara ya Viwanda, ndiyo nilianzisha chuo cha kufundisha wataalam mambo ya *leather boot* kule, sijui kama kinaendelea au hakiendelei.

Kwa hiyo, mimi nashauri tuweke mpango kabisa kwamba, ikifika baada ya miaka mitano, kumi, Tanzania inavaa viatu vyake yenyewe kutoka kwenye ngozi inazozalisha. Tanzania tusiuze ngozi nzima nzima, tuuze ngozi iliyosindikwa ndiyo itatupa fedha zaidi. Sasa mambo haya hayawezi kufanywa na watu wanaokuja kesho, tuanze sisi tuliopo. Huo ndiyo wito wangu. *(Makofi)*

La mwisho, ningependa niliseme lakini hili naomba ku-*declare interest;* mimi nina kiwanda kinachochinja nyama na kusindika. Kenya wanatuuzia nyama na bidhaa za nyama, lakini sisi hatuwezi kuuza nyama Kenya ingawa tupo kwenye jumuiya moja ya Afrika Mashariki. Mimi mwenyewe nimezungumza na wafanyabiashara wa Kenya, nikawaambia jamani mimi nataka kuwauzia nyama wakaniambia Bwana Mzindakaya tumeiambia Serikali hapa, Sheria ya Kenya inazuia hakuna kuleta nyama kutoka mahali popote.

Sisi Watanzania tunanunua nyama kutoka Kenya; hivi tatizo letu ni nini? Ng'ombe wanaochinjwa na nyama kuletwa hapa wanatoka Mara na kwa rafiki yangu Mheshimiwa Laizer. Mwenzetu Dr. Mazala, ana kiwanda cha maziwa pale Musoma, ameshindwa kuuza maziwa kule, ameuza kwa shida wanakwenda ku-*process* mafuta na siagi wanatuletea Tanzania. Sasa jumuiya gani hii?

Kwa hiyo, naiomba Serikali itoe tamko; kwa nini tunaendelea kukataliwa kuuza nyama Kenya wakati wao wanatuuzia? Mimi kiwanda changu kinaweza kutoa tani 500 kwa mwezi za nyama, tena *cuts* siyo *carcasses*, *cuts* tani 500 kwa mwezi. Mimi ningeweza kuuzia hoteli zote nyama na tukaacha kununua nyama kutoka Kenya. Siwezi kuuza kwa sababu nyama ya Kenya inaingia hapa, sisi tutakuwa watumwa mpaka lini katika mambo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, kwa mchango wako. Mchango wako ni mahiri na tunakupongeza ume-*declare interest* na ni mdau mkubwa sana katika sekta hii ya ufugaji.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ambao wote wanatoka katika jamii ya wafugaji na tuna imani nao. Nawapongeza pia Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, kwa kutayarisha kisayansi na kitaalamu, muswada wa Biashara ya Ngozi. Mategemeo yetu ni kuwa, Muswada huu ukipitishwa na Bunge utatekelezwa na kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Muswada utekelezeke na uwe endelevu nashauri yafuatayo:-

(i) Katika Jimbo la Kondoa Kaskazini, pamoja na kuwa tuna mifugo mingi, lakini kuna upungufu mkubwa sana na maafisa ugani katika sekta ya mifugo. Hii inasababisha wafugaji kukosa utaalamu na matokeo yake ni ufugaji duni na usio na tija.

(ii) Serikali iongeze ruzuku kama ilivyo katika sekta ya kilimo.

(iii) Wafugaji watengewe maeneo ya malisho na wamilikishwe. Hivyo, Serikali Kuu ishirikiane na Halmashauri. Aidha, maeneo hayo yawe na huduma zote muhimu kwa mfano, maji, majosho na kadhalika.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ndogo ni muhimu sana kwa kumuwezesha mfugaji kujiendeleza kimaendeleo, hasa kwa kuwa na uhakika wa bidhaa ya ngozi kuwa na soko la uhakika kujiongezea mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mapendekezo yafuatayo ili kuiboresha sekta hii:-

(i) Maafisa Ugani wote waliopo ngazi ya wilaya, kata na vijiji kuendesha kampeni kwa wafugaji ili kuwaeleza faida ya ngozi na hasara au athari zinazoweza kuathiri bidhaa hii katika soko na hivyo kujipunguzia mapato.

(ii) Soko la ngozi za mifugo kama ng’ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika, liwe la wazi ili wafugaji waweze kufahamu hilo kwa dhana ya kuondokana na kwamba baada ya mnyama kuchinjwa hiyo ngozi inakosa thamani tena.

(iii) Kwa kuwa matumizi ya ngozi ni muhimu sana kwa mahitaji ya binadamu kama vile utengenezaji wa viatu, mabegi, sofa za viti na kadhalika, ambavyo vyote ukihitaji *pure leather* gharama zake ni kubwa sana, basi serikali itilie umuhimu wa kuhakikisha viwanda vya ngozi vinakuwepo nchini na vinafanya kazi ili zao hili la ngozi liingie katika ushindani wa soko sawa na mazao mengine.

(iv) Malisho, majosho, maji na matibabu kwa mifugo vitiliwe mkazo kwa wafugaji hasa kufuata sera ya mifugo ili kutoa kipaumbele katika kuboresha zao hili la ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kuletwa kwa Muswada huu.

Nashauri Kamati ya Ngozi ya Kijiji wale Wajumbe watano wazingatie gender, angalau wawili kati yao wawe ni wanawake.

*Functions of advisory committee iongezwe (e) "To Inspect the premises situated in respective village where Village Advisory Committee is situated."*

Establishment of Council izingatie Gender.

*Nashauri Registration Certificate* ambayo itakuwa *renewed* baada ya miezi kumi na mbili, kusiwepo na ada au kama ipo iwe ndogo sana ili kupunguza mlolongo.

*Functions of the village Hides, Skins Advisolry Committee,* tuongeze 9(2)(e); wawe wanafanya *inspection* maana inawezekana Inspectors wakawa wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngozi iwe nzuri na ufugaji unapaswa kuwa mzuri, tukiweza kushauri *Over Grazing* itasaidia sana. Kwa mfano, Ng'ombe awe *monitored* anatoa maziwa kiasi gani, anaumwa, matibabu na kadhalika.

Pia alama za ng'ombe, anaweza akavalishwa tag yenye namba na kadhalika. Suala la *training (education/awareness),* halijawa *covered* kwenye Muswada huu. Kamati za ushauri ya kijiji/na halmashauri sijui wanapata wapi *training?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Subsides*, kwa mujibu wa muswada huu kutakuwa na jengo la kuchunia ngozi na biashara ya ngozi. Naomba ujenzi wa maeneo haya upewe ruzuku (subsides), kwa kuanzia wafugaji wetu wengi wangetamani kuwa na *premises, building or place where curing, grading, storage and trade are being carried* lakini hawana uwezo.

Naomba kushauri *method;* hii *premises* wasipewe hela Wizara, i-*advertise tender (procurement)*, wawe na ramani alipwe *contractor*, tuingie mkataba baada ya miezi kadhaa *premises* ipo. Aidha, tuwe na *pilot areas*. Ada ya kulipia leseni iwe ndogo.

Je, hawa inspector wapo wakutosha? Maadili ya *Inspector* hayamo kwenye muswaada huu, wamekuwa ni chanzo cha ucheleweshaji au urasimu. Nashauri wawe na *code of conduct* (maadili).

Naushauri faini iwe *not exceeding one million shillings*, badala ya *two hundred thousand* ili isipelekee kurekebishwa mara kwa mara kwa mfano, kifungu cha 32(1).

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wote wa Wizara, kwa kuleta Muswada wa Sheria mpya ya ngozi.

Sheria mpya ya Ngozi naamini itachangia uwepo wa maboresho katika sekta ndogo ya ngozi, kwa maana ya mapato kuongezeka kwa mfugaji, mfanyabiashara ya ngozi, viwanda vya ngozi na mapato ya serikali. Hata hivyo, ubora wa ngozi, ambalo ndilo zao la kwanza, utategemea uwepo wa wanyama/mifugo bora, yaani yenye maumbo makubwa na yenye afya bora.

Hivyo, mipango ya kuiboresha Sekta ya Mifugo iendelezwe. Bado ruzuku ya serikali kwa dawa za kuogesha na kutibu magonjwa haitoshi sana ukilinganisha na ruzuku inayotolewa katika kilimo cha mazao. Naomba muendelee kupigania ongezeko la Bajeti ya Serikali kwa suala hili na mengine ya kuboresha Sekta ya Mifugo. Nawatakia kila la heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakupongeza sana kwa kuleta Muswada huu muhimu.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

- Serikali imeweka mikakati gani ya kuzuia/kudhiti magonjwa yaenezwayo na kupe kwa kuwa yanaharibu sana ubora wa ngozi?

- Je, serikali itakubaliana nami kwamba ifanyike sensa upya ya mifugo; ng’ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika?

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri zinazofanywa na Wizara yake. Nami nasema naunga mkono hoja na kuchangia kwa ufupi, atusaidie kufahamu ni kwa nini sasa bei ya ngozi ipo chini na inashuka siku hadi siku?

Je, Wizara yake imejipanga vipi kuwasaidia wananchi wake kumaliza tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Wizara yake na serikali kwa ujumla, kwa kuleta katika Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria hii ambao umelenga kuboresha uchumi wa wafugaji na wachungaji kupitia biashara ya ngozi.

Kwa kipindi kirefu sana, ngozi imepoteza thamani yake katika soko. Bado ninakumbuka sana, idadi kubwa ya ulanguzi wa ngozi vijijini ambayo imekuwa ikizidi kupungua kwa kasi kuanzia miaka ya 1960. Kwamba, leo tunajadili njia na utaratibu wa kuboresha zao hili kwa manufaa ya wadau wa zao hili ni jambo la kutia moyo sana.

Binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Kwimba, ninaunga mkono hoja hii.

Baada ya kuupitia Muswada kwa kadiri nilivyouelewa, nimejiridhisha kuwa lengo lake lilikuwa wazi; ni kuboresha zao hili ili liweze kupata pato zuri zaidi katika soko. Nimegundua uandaaji wa ngozi hadi kufikia ubora unaokusudiwa, umewekewa utaratibu mzuri sana na inatarajiwa kufuatiliwa kwa msimamizi na weledi kwa kutosha kila hatua.

Ni imani yangu kuwa, utaratibu huo ukifuatwa kwa karibu, ngozi itafika kwenye soko ikiwa na sifa na ubora unaotarajiwa na hivyo, kulinufaisha taifa kimapato ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara wa ngozi. Kwa maoni yangu, utaratibu huu unalenga kulinufaisha taifa zaidi, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi na wafanyabiashara wa ngozi.

Naomba kufahamishwa wazi ni kwa namna gani mfugaji/mchungaji atanufaika na utaratibu huu; faida itakayokuwa dhahiri na hali ilivyo sasa?

Naomba nifahamishwe bei ya ngozi kwa mfugaji itapangwa vipi na kwa utaratibu gani? Je, mfugaji atashirikishwa katika upangaji wa madaraja na bei? Haki za mfugaji katika utaratibu huu zitalindwa na kipengele kipi cha Muswada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli biashara hii itaongeza ajira. Je, waajiriwa hawa wanapokuwa wezi, hawataathiri moja kwa moja faida kwa mfugaji?

Aidha, nimeshindwa kuona waziwazi katika Muswada huu jinsi sheria hii itakavyoazimia na mchungaji kupata fursa zifuatazo: Haki ya kupata fursa ya kupata semina elekezi kujipatia ufahamu wa weledi wa uchungaji, uanikaji, upangaji wa madaraja na kadhalika kwa kuwawezesha wanachi hawa kufanya shughuli hizi bila kulazimika kulipia tozo kwa ajili ya shughuli hizo.

Hivyo, Sheria kwa kiwango fulani ingelionesha shauku ya kuwaona wananchi; wafugaji na wachungaji wanaunda ushirika wao angalau hadi ngazi za kata na wilaya ili

mara kwa mara wakumbushane haki zao, wajibu wao na vikwazo na jinsi ya kuvitatua. Ushirika kama huo, ungelekeza hatimaye ngozi zisitoke wilayani au mikoani kabla hazijasindikwa. Hivyo, ushauri wangu ni ufuatao:-

(i) Kupunguzwa hatua zitakazomtaka mchungaji/ mfugaji kulipia huduma moja kwa moja.
(ii) Elimu ya kutosha kutolewa kwa wafugaji na wachungaji juu ya umuhimu wa upatikanaji wa ngozi bora na jinsi ubora wa ngozi unaotakiwa unavyoweza kuufikia.

(iii) Serikali kwa kiwango cha juu iwasaidie wafugaji na wachungaji katika hatua za mwanzo za utekelezaji wa sheria hii ili kuwezesha wananchi kwa kadiri itakavyowezekana, wananchi wenyewe waweze kutekeleza hatua za msingi wenyewe bila kutegemea waajiriwa ili kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara hii ili bei ya ngozi kwa mfugaji na mchungaji isipungue sana. Lengo kuu liwe kumsaidia mwananchi kupata faida kubwa kutokana na zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka, ukizingatia ya kwamba, Sheria hii ya Mwaka 1963 imepitwa na muda na umuhimu wa zao la ngozi kwa uchumi wa taifa letu.

Hata hivyo, inasikitisha kuona viwanda vilivyobinafsishwa havifanyi kazi kama ilivyotarajiwa; badala yake ngozi ghafi inauzwa nje kwa njia ya magendo. Iwapo waliopewa viwanda hivyo hawawezi kuviendeleza; basi wavirudishe serikalini ili wawekezaji wengine wapatikane ili kuviendeleza viwanda hivi.

Aidha, ili kuondoa kero za harufu mbaya maeneo ya viwanda hivi, kama ilivyokuwa kwenye kiwanda cha Kibaha, uwepo utaratibu wa kuhakikisha kila kiwanda cha ngozi kinakuwa na *oxidation ponds* kuzuia hewa mbaya na hususan *ammonia.*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na viwanda vichache, ukilinganisha na idadi ya mifugo iliyomo nchini, serikali ichukue hatua za makusudi kufungua viwanda vilivyosimama kufanya kazi, kikiwemo kiwanda kikubwa na cha uhakika cha Mwanza Ilemela. Kusimama kufanya kazi kiwanda hicho, kimesabibisha vijana wetu kukosa ajira na vyombo mbalimbali kuibiwa kwa kukosa udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pendekezo la kuwamilikisha maeneo wafugaji wa mifugo, itakuwa ni bure kama serikali itatoa eneo bila kuzingatia kutoa maeneo mengine ya huduma kama vile malambo ya maji, kurudisha heshima ya vituo vya matibabu ya mifugo *(veterinary centre),* pamoja na wataalam wa kutosha katika maeneo ya wafuaji hawa na *veterinary officers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kuongoza kikao cha Bunge Tukufu, pamoja na Naibu Spika na Mwenyekiti. Nawapongeza kwa hilo. Pia nawapongeza Waziri na Wizara yake yote, kwa kazi nzuri na mashirikiano na watendaji wake wa serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ya Biashara ya Ngozi kwa kwetu Tanzania ni nzuri kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, naiomba serikali kusimamia vyema ili tupate tija zaidi na pia tufaidike kwa mambo yote kwa serikali na wananchi wenyewe kifedha na ukuaji uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itoe elimu kwa makusudi kwa wananchi; wafanyakazi na wafugaji na kupewa uwezo wa kifedha ili wawe na mifugo mingi na kuitunza, wapatiwe dawa na kuwekwa kwenye mazingira mazuri ili inapofikia kuchinjwa, zipatikane ngozi nzuri zenye uimara na *grade* safi sana kwa kuuza ndani na nje ya nchi yetu kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri na yeye nitampa dakika 15 za kuchangia hoja hii, kabla sijamwomba Mheshimiwa Waziri mtoa hoja aweze kuchangia hoja yake kwa dakika 45.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Nianze mchango wangu kwa kutamka kwamba, naunga mkono hii hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia kwenye majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Charles Mwera, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Tarime. Nampongeza sana. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa John P. Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa maelezo aliyotoa asubuhi hapa Bungeni. Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, pamoja na Kambi ya Upinzani, kwa maoni yao ya kuunga mkono hoja. Napenda kuwapongeza sana. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kusisitiza umuhimu wa zao la ngozi, maana Mheshimiwa Waziri wetu na wachangiaji mbalimbali wamelielezea suala hili kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitoe maelezo ya hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, zilizojitokeza katika kuchangia Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi *(The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008)*. Nitasema baadhi, kwani Mheshimiwa Waziri atawatambua Wabunge wote waliochangia muda mfupi ujao atakapoanza kuhitimisha hoja hii. Naomba niwashukuru waliochangia na kuwahakikishia kwamba, tutathamini michango yao na tunawaahidi kuwa itazingatiwa katika kuikamilisha sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia hoja za Wabunge waliochangia. Kwanza, naanza hoja ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Charles Keenja, ambaye alitoa mchango wake hapa kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Alitaka kujua kama wafugaji wanamilikishwa maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo. Ukweli bila maeneo ya kulisha mifugo, hata hiyo ngozi tunayoisema hatutakuwa nayo kwa sababu hatutakuwa na mifugo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutamka kwamba, hadi sasa Serikali imechukua na itaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kwamba, wafugaji wanapata maeneo ya kufugia. Hadi sasa jumla ya hekta 930,276 katika vijiji 155 vya Halmashauri 24 zimeshatengwa na kupimwa kwa ajili ya ufugaji. Zoezi hili litaendelea hata mwaka huo na litaendelea miaka ijayo, wakati tunashirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Halmashauri. Serikali kazi yake ni kuhakikisha kwamba, wafugaji hawafukuzwi ovyo ovyo, wanakwenda na kuepuka matatizo kama haya ambayo yametokea Kilosa. Kwa hiyo, tutaendelea kupima hayo maeneo.

Hoja nyingine iliyotokea ni kwamba, zipatikane huduma za ugani, maji na malisho. Kuhusu huduma za ugani ni kwamba, mkulima hawezi kuboresha ng’ombe wake, hata akiugua hawezi kujua jinsi ya kumtibu. Vilevile huwezi kufuga bila maji na malisho, lakini Serikali imeanza kutoa huduma hizi. Utoaji wa huduma umezingatiwa katika Bajeti ya Wizara. Aidha, wananchi wanahamasishwa kuibua miradi hii kupitia *DADPs* ili kujipatia huduma hizi. Nimetembelea sehemu nyingi, nikifika wanasema Wizara haitupatii majosho. Ndugu zangu hizi hela zinapitia katika mpango wa *DADPs,* tunasisitiza sana tuhakikishe kwamba, Halmashauri zinahamasisha. Wakati mwingine Mkurugenzi ndiyo anakuuliza ziko wapi hela za malambo, wengi hawajui.

Tunasema hela hizi zipo na tunatakiwa tuwahamasishe wananchi kupitia Mipango ya *DADPs,* kuweza kuwapatia wananchi malambo, majosho na mambo yote ya ugani.

Hoja nyingine ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Keenja ni kwamba, wafugaji wapewe ruzuku kwa pembejeo. Ndugu zangu Wizara imeshaliona hili na katika mwaka 2008/2009, Serikali imeongeza ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo kutoka shilingi bilioni 1.2 mwaka 2007/2008 na kufikia shilingi bilioni 1.4. Serikali itaendelea kuongeza hii ruzuku.

Napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, hela za *EPA* zimesharudishwa. Tumeshaitwa Hazina na tumetayarisha bajeti ya kuomba tena

tuongezewe.  Kwa hiyo, naamini kwamba, hela za ruzuku za pembejeo zitapatikana na huo uhakika tunao tumeshapendekeza na zikipatikana tu tutaongeza ruzuku.

Hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba, iwepo mipango ya uhakika ya masoko ya mifugo na bidhaa zitokanazo na mifugo, yaani viwanda, minada na machinjio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa machinjio, minada na viwanda, kuongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba, tutafsiri sheria na kanuni kwa Lugha ya Kiswahili na kutoa elimu ya Sheria ya Ngozi. Ukweli panaweza kuwepo na sheria, lakini kama wananchi hawajui lugha ile iliyotumika, hawawezi wakaifahamu vizuri. Kwa hiyo, ushauri huu umezingatiwa na utatekelezwa kama Waraka wa Baraza la Mawaziri unavyoagiza. Tutahakikisha kwamba, hii sheria imetafsiriwa vizuri na kuweza kuwapa wafugaji na wananchi wote wa Tanzania ili waweze kuitumia kwa manufaa na maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mengine ni kwamba, ziwepo sheria za kudhibiti ushindani wa haki kulinda soko la ndani.  Ipo Sheria ya Ushindani wa Biashara *(The Fair Competition Act)* na ndiyo itakayosimamia eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mengine yaliyotolewa ni kwamba, taratibu za ununuzi na uuzaji wa mifugo ziwe wazi.  Napenda kutamka kwamba, taratibu zipo wazi ila kuna watu ambao hawazifuati na wanafanya haya makosa kwa makusudi tu. Hivyo, tunaomba ambao hawazifuati waripotiwe na sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi iliyotolewa na Mheshimiwa Keenja ni kwamba, mipango ya elimu kwa wadau wa ngozi itolewe.  Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imeshaling’amua hili na inazingatia elimu kwa wafugaji.  Ndio maana kuna mpango wa kufundisha maafisa ugani katika vyuo vyetu vya Tengeru, Morogoro, Mpwapwa, Buhuri, Temeke, Madaba.  Aidha, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo, elimu juu ya ufugaji bora, uchunaji, ukaushaji na uchambuzi wa ngozi, inatolewa katika Halmashauri 55.  Tumeshapitia Halmashauri 55 kwa kutumia *Livestock Development Fund* na hiyo elimu itaendelea kutolewa.  Kuhusu maafisa ugani ni kwamba, mwaka jana tulipeleka maafisa ugani kama 1,006 na tunatarajia kwamba, wakitoka wataajiriwa wote.  Mwaka huu tunapeleka 1,185, nia ni kupata maafisa ugani 15,000 ambao watapelekwa kila kijiji ili waweze kutoa huduma za ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa kutuunga mkono.  Alitoa ushauri mzuri na sisi tumeupokea na hoja zake zote ambazo alizitoa tutazizingatia.  Hoja aliyoitoa kwanza ya pato la taifa litokanalo na ngozi ni dogo ni hoja ya kweli.  Sisi tumesema tuna ng’ombe wengi na mwaka jana tumeuza ngozi karibu milioni 2.5 na tulichopata ni bilioni 21. Hiyo hela kama ni ya Wanyancha ni nyingi, lakini ukisema Tanzania yenye watu milioni 40 ni kwamba, kila mtu amepata shilingi hamsini tu. Kwa hiyo, jitihada zinaendelea kuboresha zao la ngozi ili kuongeza ushindani hapa nchini, kama njia mojawapo ya kuongeza pato la taifa.

Tutaendelea kuendeleza jitihada hizi, hasa kwa kupitia, hatutaandika na utaratibu wa sheria utaanza.

Serikali itatue matatizo yanayokabili zao la ngozi. Serikali inatekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Viwanda, unaolenga kutatua matatizo haya. Maoni mengine ilikuwa sifa za *registration authority* ziainishwe wazi kwenye kanuni. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, ushauri utazingatiwa wakati wa kuandaa kanuni. Lazima hizi ziwepo ili iweze kujulikana kwamba ni sifa gani mtu anatakiwa kuwa nazo. Sifa za *premises* ziwekwe bayana. Sifa na ubora wa *premises* zitawekwa kwenye kanuni zitakazoandaliwa. Kwa hiyo, huu ushauri utazingatiwa.

Hoja nyingine iliyotolewa ilikuwa kwamba, kipindi cha leseni kiwe miaka miwili hadi mitatu badala ya mwaka mmoja. Kweli ni usumbufu kumpatia mtu leseni, baada ya mwaka anakuja, anaweza asipate halafu akafunga biashara yake. Katika kipindi cha mwanzo hiki ndiyo tunafanya hivyo, lakini baadaye mambo yakishaenda vizuri, tutatoa leseni hizi kwa kipindi kirefu.

Uchafuzi wa hewa *(Air Pollution)*, kutoka katika viwanda vya ngozi uzingatiwe. Ni kweli kama mliona juzi katika taarifa ya habari, watu kule Mbagala uliona yale maji yalivyokuwa yanatiririka na wananchi wakiwa na hali ile. Hii hali haiwezi kuvumilika. Kwa hiyo, uharibifu wa mazingira bado tutatumia Sheria ya Mazingira. *Environmental Management Act*, itaendelea kusimamia shughuli za uchafuzi.

Kwa hiyo, hiyo sheria ipo kupitia *NEMC* tutaidhibiti. Adhabu zitaje viwango vya chini na vya juu. Ni kweli, kama ukiachia kiwango cha juu milioni moja, watu wataendelea kupigwa faini ya shilingi 5,000, 10,000, kwa hiyo, sheria itakuwa haina maana. Adhabu za chini zitawekwa katika kanuni hizi na zitakuwa juu isiwe tu ni kufanya mzaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mengine ya mwisho ambayo Msemaji wa Upinzani aliyatoa alisema uamuzi wa Mheshimiwa Waziri na Mkuu wa Mkoa, usiwe wa mwisho unaokiuka Katiba ya Nchi. Mambo yote yanapoenea hapa Tanzania, mwisho wake inatakiwa iwe mahakama. Sasa hivi siyo kwamba, mwananchi hataruhusiwa kwenda mahakamani, lakini uamuzi wa Waziri na Mkuu wa Mkoa ni wa mwisho kiutawala; hauzuii mwananchi asiyeridhika kukata rufaa katika mahakama. Kwa hiyo, pale bado sheria itaendelea kuzingatia utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hujaunga mkono hoja. Naomba useme ili iingie kwenye rekodi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sawa sawa, maana wewe usipoanza kuunga mkono hoja yako, haitakuwa vizuri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA MAENDELEO YA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimechagiwa vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dr. James Wanyacha, kwa jinsi alivyojitahidi na kujibu vizuri sana baadhi ya hoja na amenisaidia sana na kwa maana nyingine amenipunguzia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, ningependa nitambue WaheshimiwaWabunge waliochangia hoja hii na Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Vuai Khamis, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Charles Mlingwa, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Salim Mohamed, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa James Wanyancha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamechangia na kutoa mchango mzuri sana kuhusu Muswada huu wa Sheria ambao tumeuwasilisha mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, Wabunge wote wa pande zote wameunga mkono na wengi wamezungumza kwamba, Muswada huu ulitakiwa uwe umekuja mapema sana. Kwa hiyo, kila mmoja amefurahi kwamba, Muswada huu umeungwa mkono. Kwa kuwa tumefanya *amendment* nyingi na kutoa masahihisho ambayo yamejitokeza katika Muswada huu, nina uhakika tutakapoingia kwenye Kamati, wote watasema umepita halafu tutaendelea na mambo mengine kwa ajili ya kesho, kwa sababu kila mmoja ameunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ambavyo wengi wamezungumza; ni kweli kabisa katika nchi yetu tuna mifugo mingi sana; tuna ng'ombe zaidi ya milioni 18.8, mbuzi zaidi ya milioni 13.5, kondoo milioni 3.6, nguruwe zaidi ya milioni 1.4, tunaambiwa hata mbwa ni zaidi ya milioni 4 na Iringa inaongoza kwa kuwa na mbwa nyingi. *(Makofi)*

Lakini tuna kuku zaidi ya milioni 53 …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hapo ni mbwa nyingi ama mbwa wengi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Naona Wahehe watanisaidia zaidi namna ya kuweka vizuri, kwa sababu tunazungumzia mifugo nafikiri ni nyingi.

**WABUNGE FULANI:** Hapana ni wengi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Haya ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sensa ya mifugo hii ambayo tunaizungumzia na ambayo nimeitaja hapa ni kweli kabisa sensa ya mwisho ilifanyika mwaka 1984. Kwa hiyo, idadi hii inayopatikana ni takwimu ambazo zimekuwa zikipatikana kutokana na *explication* ya maofisa mifugo wetu walizokuwa wakifanya. Pia napenda kukubaliana na wale ambao wanasema kweli inawezekana mifugo ikawa ni zaidi ya hiyo, kwa sababu ukiangalia hata takwimu tu za ngozi ambazo ziliuzwa, zilikuwa zaidi ya ngozi za ng'ombe milioni 2.5.

Palikuwa na ngozi za mbuzi zaidi ya milioni 1.9 na kondoo zaidi ya ngozi milioni 1.5, ambapo ni zaidi ya ngozi milioni 5.9 za mifugo. Hata ukipiga hesabu ya kawaida kwamba, Watanzania huwa wanakula kilo 11 kwa kila mmoja kwa mwaka, sasa kama ni kilo 11 ukizidisha kwa Watanzania ambao wapo karibu milioni 40, unaweza ukajua ni kilo ngapi ambazo wamekula na ukigawa angalau kila ng'ombe aliyekufa alikuwa na *average* kilo 200 unaweza ukajua ni ng'ombe wa ngapi waliochinjwa. Mheshimiwa hapa ananisahihisha, najua Wahehe wana mifugo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusisitiza ni kwamba, suala la kufanya sensa ya mifugo yetu ni muhimu na ndiyo maana kwa sasa hivi tunajipanga kuangalia kadiri bajeti itakavyoruhusu siku za usoni, tunaweza kufanya sensa ili tujue tuna idadi kiasi gani ya mifugo tuliyonayo. Kwa sasa hivi kwa takwimu tulizonazo hizi ni kwamba, tuna mifugo mingi na tupo nafasi ya tatu katika Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni ukweli usiopingika pia kwamba, pamoja na kwamba tumekuwa na mifugo mingi, nchi zinazotuzunguka ambazo hazina mifugo mingi ndiyo zimekuwa zikiuza ngozi nyingi kuliko sisi. Hata Kenya ambao wana mifugo michache, huwezi ukalinganisha na sisi Tanzania, wamekuwa wakiuza ngozi nyingi nje ya nchi na sehemu nyingine. Kwa hiyo, lengo kubwa la Muswada huu ni kuhakikisha kwamba, sasa tunaweka utaratibu utakaotusaidia katika kuhakikisha kwamba, zao la gozi linaanza kuleta faida kwa Watanzania.

Katika mazao ya ngozi na mazao ya mifugo ambayo tuliyapata, utaona kwamba, katika bajeti niliyoitaja ya mwaka huu, mazao yaliyoiingizia fedha za kigeni nchi yetu karibu bilioni 23.8; bilioni 21.5 zilitokana na ngozi. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba, ngozi ni zao muhimu, lazima tuliendeleze na ndiyo maana Muswada huu Mheshimiwa Mwenyekiti ulikuwa muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu pia umekuja kulingana na Miswada mingine na sheria nyingine ambazo tunaamini kabisa zimekuwa zikitekelezwa ili tuweze kufanikisha haya mengine yote, ndiyo maana tunaomba sana Bunge lako Tukufu liupitishe Muswada huu. Tunafahamu kuna Sheria ya Veterinary Namba 16 ya Mwaka 2003, kuna Sheria ya Nyama Namba 10 ya Mwaka 2006, tuna Sheria ya Maziwa Namba 8 ya Mwaka 2004 na tuna Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Namba 17 ya Mwaka 2003. Ndiyo maana tumeona hii sheria ikipitishwa ambayo imekuwa ni ya muda mrefu, inaweza ikaendana na hali halisi ya mabadiliko ya kiuchumi ambayo tunayahitaji.

Waheshimiwa Wabunge, wamechangia michango mizuri sana na mimi naweza nikasema, asilimia mia tunaikubali sana. Nikianza michango ya Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja, Mheshimiwa Charles Keenja, ambaye amezungumza kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwanza ameunga mkono lakini amezungumzia kuhusu uchungu wa kwamba, Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi lakini haitusaidii sana. Napenda niseme tu kwamba, mifugo ya Tanzania inatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano; kama kila Mtanzania anakula kilo 11 na tupo karibu Watanzania milioni 40, ukizidisha mara 40 na hizo kilo tungekuwa tunazinunua, tungejua kwamba zingehitajika trioni ngapi kwa ajili ya kuagiza zao hilo. Watanzania kwa mfano, wanakula zaidi ya mayai 64 kwa kila Mtanzania kwa mwaka sasa ungezidisha mayai 64, kwa watu milioni 40 na ukajumlisha tu kwamba kila yai unalinunua shilingi mia mbili, ungejua unahitaji trioni kiasi gani. Tunajua kabisa kwamba, Watanzania wanakunywa lita 41 ukitoa labda sehemu za Rukwa ambao wanakunywa lita 8.1, ambayo ni sawa kijiko. Kama tunakunywa lita 41 za maziwa kwa kila Mtanzania, uzidishe mara Watanzania milioni 40 na uhesabu kwamba kila lita ya maziwa unainunua kiasi gani kwenye maduka ya vyakula, unajua ni zaidi ya trioni ngapi zingehitajika.

Kwa hiyo, mazao na mali zake na matokeo yake, yanatumia fedha nyingi kama tungekuwa tunaagiza nje. Ukitoa *estimate* ya kawaida ni zaidi ya trioni 25 zingehitajika kila mwaka, kwa ajili ya kununulia hivi vitu ambavyo vinahitajika, ambavyo vinatokana na mazao ya mifugo. Ndiyo maana siku moja nimekuwa nikisisitiza kwamba, jamani wafugaji ni watu muhimu sana katika nchi hii na hivyo wasihesabike kama wakimbizi, kwa sababu wanachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi hii. Bahati mbaya tu mazao yao hatuyanunui, tungekuwa tunayaagiza nje ndipo tungejua umuhimu wa wafugaji katika nchi yetu. Kwa hiyo, tuwalinde lakini pia tuwaeleweshe ili wafuge kisasa zaidi kwa ajili ya kuendeleza na kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, wamechangia kwa uzuri tu na ushauri wao karibu wote tumeukubali. Wameelezea changamoto na kwa vile siku zote wamekuwa wakitueleza ushauri wao na kwa vile pia walitueleza wakati tukiwasilisha bajeti, tumeyazingatia na napenda kusema tu kwamba, tunawashukuru kwa ushauri wao mzuri wote na hasa kwa sababu pia wameunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naye ameunga mkono na ni kwa mara ya kwanza. Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Jecha, naona sasa Kambi ya Upinzani imeanza kutekeleza vizuri Sera ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu wanaona mambo yanavyoenda vizuri. Kwa hiyo, nawapongeza sana Kambi ya Upinzani, kwa kutambua hili na ninaamini tukienda hivi, tutakuwa tunatekeleza malengo mazuri ya wananchi ya kuujenga uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakupongeza Mheshimiwa Jecha, kwa michango yako mizuri, lakini lile suala la kwamba, uamuzi utakuwa unaishia kwa Waziri au kwa Mkuu Mkoa, Mheshimiwa Naibu Waziri amefafanua vizuri kwamba, mahakama bado ina jukumu lake kwa mtu ambaye hataridhika na ushauri ambao utakuwa umetolewa.

Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, anaunga mkono hoja. Ngozi zinazokusanywa zinaandaliwa na viwanda vya ngozi vinavyofanya kazi mafunzo ya watu wanaofanya kazi na kila kitu ameelezea. Kwa bahati nzuri, Serikali imetambua hili na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka jana na mwaka huu, ku-*train* maofisa ugani zaidi ya 1,006 katika vyuo sita vya mifugo. Mwaka huu tumetenga pia shilingi milioni 720 kwa ajili ya ku-*train* maofisa ugani 1,085. Tunaamini kabisa kwamba, upungufu wa maofisa ugani katika Sekta ya Mifugo utaendela kupungua na hadi ikifika hali halisi tuweze kuwa na maofisa ugani wa kutosha katika nchi nzima.

Kwa sasa hivi maofisa ugani wapo karibu 3,000 tu katika nchi nzima, wakati wanaotakiwa ni karibu 16,000. Kwa hiyo, tuna upungufu mkubwa lakini mwanzo ni mgumu na ndiyo maana tunapitisha hizi sheria ili ziweze kutusaidia. Ndiyo maana nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge katika bajeti zinazokuja zinazohusu Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo, basi ziboreshwe na ziwe nyingi zaidi ili tuweze ku-*cover* matatizo mengi ambayo tumekuwa tukiyakabili.

Amezungumzia pia kuhusu Bajeti ya Wizara hii ndogo na kweli ni ndogo, lakini ninachotaka tu kukuahidi ni kwamba, pamoja na kuwa ndogo, tutakitumia hiki kidogo katika kuzalisha na kuleta *productivity*. Tunaamini unaweza ukapata kidogo lakini ukikitumia vizuri, kinaweza kikaleta matunda mazuri, badala ya kuwa na kingi halafu ukakitumia ovyo ovyo. Kwa hiyo, tunaamini hiki kidogo tutaendelea kukitumia vizuri, lakini tukipata kingi napo tutaendelea kukishukuru ili tuweze kuzalisha vizuri. Anasema suala la adhabu liangaliwe, nafikiri kama tunataka kujenga uchumi wa kweli katika sekta hii, suala la adhabu tuliache hivi hivi, kwa sababu tukianza tena huruma huruma hatutaweza kuendeleza hili suala. *(Makofi)*

Ninafahamu kuna Muswada mwingine ambao tutauleta kama tutapata nafasi; Muswada wa Ustawi wa Jamii. Unaendana na adhabu na namna gani tunaweza tuka-*treat* mifugo yetu.

Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, naunga naye mkono na mengine mengi ameyazungumzia. Amesema bajeti ni ndogo na kadhalika. Mheshimiwa Lekule Laizer, anaunga mkono hoja na mimi namshukuru sana; Muswada huu ulichelewa kuletwa lakini sasa tumeuleta Mheshimiwa Laizer akiwepo. Fedha nyingi zinapotea na mimi

nakubaliana naye, kwa sababu kwa mfano Wamasai kule aliko, watu wengi huwa wanauza ngozi Kenya.

Sasa ndiyo maana tumeleta Muswada huu uweze kudhibiti, lakini pia kuwasaidia wakulima na wafugaji wakiwemo akina Laizer katika kuboresha lakini na pia kuboresha ukuaji *value* kwenye ngozi zetu. Anaishukuru sana Wizara kwa kuandaa Muswada huu.

Sensa ya mifugo; na mimi ninakubaliana naye kwamba, inawezekana tukawa na mifugo mingi zaidi kuliko hii tunayoizungumza na ndiyo maana watu wamekuwa wakitoka sehemu moja hadi nyingine. Kwa hiyo, suala la kufanya sensa ya mifugo ni muhimu lakini kitu kikubwa kinachohitajika ni fedha. Mwaka huu mfanye sensa ya mifugo; mbona mnahesabu sensa ya wanyama porini! Sasa ndiyo maana nasema haya yote yanaendana na uwezo wa bajeti, kwa sababu tulifanya sensa ya watu lakini sensa ya mifugo ya ukweli kabisa ilifanyika kwenye miaka ya 1984.

Pamekuwepo na udanganyifu hasa wakati ule palipokuwa na kodi ya mifugo, mtu anaenda anaulizwa; hasa ndugu zangu hawa akina Laizer Wamasai, ukienda kuwauliza una ng’ombe wangapi; mfugaji akiwa na ng’ombe 200 atasema yeba nina ng’ombe 20 tu au 30, kwa sababu palikuwa na kodi ya mifugo. Bahati nzuri suala la kodi sasa hivi limefutwa, kwa hiyo, nina uhakika kuwa sensa tutakayoifanya italeta matokeo halisi katika mifugo tuliyonayo katika nchi yetu.

Mazao ya mifugo ni muhimu, ametoa ufafanuzi wa mazao ya mifugo mengi tu, pamoja na vitanda vya ngozi ambavyo tunalalia, makochi na kadhalika. Nakubaliana naye kabisa, lakini tunauza mifugo baadaye tunaletewa mazao ya mifugo. Hili ni suala la aibu na ndiyo maana tumeleta Muswada huu ili ukishakubalika, tuanze kuweka utaratibu mpya na wale watu wenye uwezo wa kuanza kujenga viwanda waanze sasa kujenga viwanda.

Ningependa kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, wale ambao wana marafiki zao ambao wanaweza wakawaleta huku kwa ajili ya kuanza kujenga viwanda vya ngozi akiwemo Mheshimiwa Sanya, basi uwalete ili wajenge na watu wapate *employment. Grade* za ngozi zetu zitakuwa nzuri, badala ya kuuza asilimia 80 kama *raw material*, lakini pia itaongeza Pato la Taifa.

Kwa hiyo, ningependa kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge walio na marafiki zao, wawalete kwa ajili ya kuanza kuingia kwenye biashara hapa inayohusiana na mifugo. Ndiyo maana tunampongeza sana Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, ameanza hili kwa kuanza na biashara ya nyama, lakini namshauri pia aingie sasa na kwenye biashara ya ngozi. Pale anapochinja wale ng’ombe wake 500, basi pawepo na kiwanda pia cha ku-*process* ngozi badala ya kuchinja, halafu ngozi anawauzia watu wengi kwa kupunjwa.

Mmezungumzia pia kuhusu masuala ya dawa za mifugo; ni kweli kabisa magonjwa ya mifugo kwa mfano, kupe nayo ni chanzo cha kuharibu ngozi. Bahati nzuri katika bajeti ya mwaka huu, tulipewa bilioni 1.4 kwa ajili ya ruzuku ya dawa ambayo

yanatosha kuogesha ng’ombe milioni 2.3 tu, hatutaogesha mbuzi wala kondoo wote; na wale ng’ombe milioni 18.8 tutaogesha milioni 2.3 tu wengine hawataogeshwa na huu ndiyo ukweli na hii ndiyo *challenge* tuliyonayo katika Wizara hii. Kwa hiyo, ninaamini kwamba, kadiri mambo yanavyokwenda, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna hatua zinaangaliwa ni kwa namna gani tunaweza tukaongezewa hela ambazo zinaweza zikasaidia katika dawa ambazo zitasaidia katika kuogesha. Mimi ninaamini hizi tunazichukua kama changamoto ambazo zitaweza kusaidia katika kuongeza na kuhamasisha suala hili la ngozi katika nchi nzima.

Katika suala la elimu kwa wafugaji, tunaendelea kutoa elimu kupitia vyuo vyetu sita vya mifugo, lakini pia Wabunge kupitia Miswada kama hii, nayo ni elimu. Tunaamini pia tunatoa vipindi katika redio na *television*, vinavyohamasisha ufugaji bora. Muswada huu utakapopita, tutatoa vipeperushi na kutoa maelezo *especially* kwa Wakurugenzi wetu ni kwa namna gani sasa wanaweza kutafsiri kwa lugha iliyo rahisi ili elimu hii ya kutengeneza ngozi iweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Martha Umbulla amesema Muswada huu umekuja kwa kuchelewa sana; hivyo, hatukutakiwa Watanzania kuwa maskini. Ni kweli kabisa, lakini Sheria hizi zisaidie Watanzania badala ya kuwanufaisha wageni. Tumekuwa tukiwanufaisha wageni na ndiyo maana tumeleta Muswada huu, tunapokuwa na sheria inasaidia sasa ni kwa namna gani sheria inaweza ikadhibiti masuala haya. Amezungumzia pia Muswada huu ni mzuri sana, elimu kwa wafugaji, soko lipatikane na kadhalika na anaunga mkono kwa asilimia 100.

Kila mmoja alikuwa anatoa ushauri na kuunga mkono na sisi tumeupokea ushauri wote. Tunawashukuru kwa kuunga mkono na nina uhakika Muswada huu, kwa sababu tumeuleta kwa wakati unaotakiwa, basi Watanzania watautumia kwa ajili ya manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa John Lwanji, anaunga mkono hoja na anasema Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kwa kuwa na mifugo lakini viwanda havipo, vipo sita tu vinavyofanya kazi, navyo vinafanya kwa asilimia kati ya 30 na 50. Hii ndiyo hali halisi na ndiyo tulitaka Waheshimiwa Wabunge, wajue hali halisi ya suala hili kwamba, tulikuwa na viwanda sita vinavyofanya navyo vinafanya kwa asilimia kati ya 30 na 50 na vile vingine hata vilivyokuwa wameuziwa kupitia ubinafsishaji navyo vimekaa tu kama magodauni havifanyi kazi. Sasa hatuwezi kuendelea kwa njia hii, ndiyo maana tumeleta Miswada hii ili tuweze kuwa na utaratibu mzuri wa kuendeleza zao la ngozi.

Vilevile amesema hatuko-*serious* kwenye biashara hii, hivyo Serikali ichukue hatua madhubuti. Ndugu yangu, hatua madhubuti ni pamoja na kuleta sheria, kwa hiyo, huu ni mwanzo wa sheria madhubuti ya Serikali, ndiyo maana tumeleta Muswada huu. Tunaomba upitishwe ili muanze kuona matokeo, namna gani tutaweza kuitumia hii Sheria katika kuboresha na kuinua biashara ya ngozi.

Wanyama wasiteswe ili kupata ngozi iliyo nzuri, ni kweli ndiyo maana kuna Muswada wa Ustawi wa Wanyama, ambao tutauleta hapa. Sasa sifahamu kama katika Bunge hili utapata nafasi. Muswada huu unazungumzia ni kwa namna gani wanyama wanatakiwa wawe *treate* kwa kuzingatia ushauri huu ambao umetolewa na Mheshimiwa Lwanji. Amezungumzia pia elimu itolewe kwa wafugaji, viwanda vya kutosha vinahitajika na mimi nasisitiza kweli viwanda vinahitajika, wale wenye uwezo wa kujenga viwanda, waanze kujenga hata kwa kuanzisha viwanda vya pamoja kwa kutumia *SACCOS* na kadhalika.

Mheshimiwa Sanya amesema, Muswada huu umechelewa lakini umefika na umemfikia Mheshimiwa Sanya. Tanzania tunaambiwa ni watatu, lakini tunaambiwa sensa hiyo ilifanyika mwaka 1984, kwa nyakati hizi zote tumekuwa tunapata takwimu kupitia *explication* kwa kutumia maofisa wetu wa mifugo walioko katika Halmashauri. Tupo makini katika kuwalinda wafugaji na ndiyo maana tunatengeneza sheria. Nimetaja kwamba, kuna Sheria ya Nyama Namba 10 ya Mwaka 2004, tuna Sheria ya *Veterinary* Namba 16 ya Mwaka 2003, tuna Sheria ya Maziwa Namba 8 ya Mwaka 2004 na kuna Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, lakini tuna Bodi ya Nyama na Bodi ya Maziwa ambayo tayari nayo tumesha. Katika kuboresha haya, ndiyo maana tumeleta Muswada wa Ngozi, lakini tutaleta pia Muswada wa Ustawi wa Wanyama. Katika hilo, tumeanza kushirikiana na wenzetu Wizara ya Ardhi kwa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji. Hadi hivi sasa zaidi ya hekta milioni moja zimeshatengwa kwa ajili ya wafugaji wa vijiji 155 katika wilaya 24.

Hii ni katika kuhakikisha kwamba, tunaendelea kuwasaidia wafugaji nao waweze kufuga kisasa, kwa kushirikiana vizuri na wenzao wakulima kwa sababu Tanzania tunawafugaji milioni 24. Kwa hiyo, karibu nusu ya Watanzani ni wafugaji. Hata yule anayekaa Dar es Salaam, kuna akina mama wengi wanafuga kuku, wale ni wafugaji. Hata wale wakulima wanaolima sana, lazima wanalima kwa kutumia ng’ombe, kwa hiyo wanakuwa ni wakulima lakini pia ni wafugaji.

Wengine wanafuga, nimetaja Iringa zaidi ya mbwa milioni nne, kwa hiyo, nao hata kama ana mbwa mmoja anamfuga ni mfugaji. Unaweza ukakuta Watanzania ambao ni wafugaji ni wengi kweli. Kwa hiyo, saa nyingine ni vigumu kutofautisha kati ya mfugaji na mkulima. Ninakubaliana na Mheshimiwa Sanya kwamba, tutaendelea kuwalinda wafugaji kwa kuboresha sheria zetu ili mambo haya yaweze kwenda sawa sawa kwa maendeleo ya Watanzania wote.

Umezungumza pia kwamba, Tanzania hivi leo si ya kuagiza viatu kutoka nje; ni kweli kabisa haya yote yanamuumiza Mtanzania yeyote ambaye anaipenda nchi yake, huwezi ukauza ngozi zaidi ya milioni tano za wanyama waliokufa, waliochinjwa au kuuawa katika eneo hili kama *raw material* asilimia 80. Unapowauzia wale wanakwenda ku-*process* halafu wanakuletea kiatu ambacho utakinunua kwa shilingi 500,000 wakati wewe ng’ombe umemuuza kwa shilingi 10,000, kwa hiyo ni kama ng’ombe 100 unanunua kiatu kimoja, hii ni aibu.

Hii ndio sababu tunaleta Miswada hii tuweze kuanza kubadilika. Inawezekana tumechelewa, lakini inawezekana wa mwisho akawa wa kwanza ilimradi tutatekeleza haya ambayo tutakuwa tumeyatekeleza kwa juhudi zetu zote, kwa nguvu na kwa ushirikiano wa pamoja kama ushirikiano ambao umeonyeshwa leo na wenzetu wa Upinzani na wa CCM, kwa kukubali Muswada huu kwa asilimia 100. Kwa hiyo, haya ni mambo mazuri na nina uhakika mengine yote yatakuja kama yatakavyokuwa yanaendelea.

Mabenki yetu yaanze kuwakopesha wafugaji, hili nalo ni tatizo moja kubwa; tuna mabenki zaidi ya 33 na mengi sasa yanaendelea kufanya biashara kwa *Treasury Bills* na Serikali na kadhalika. Hayakopeshi wafugaji, hata *NARCO* ambacho ni chombo cha Serikali ambacho kina hekta zaidi ya 230,000 na ng'ombe zaidi ya 41,000, hawajapata mkopo kutoka kwenye mabenki yetu. Kwa hiyo, ni kitu cha kusikitisha. Sifahamu tutafanyaje; mimi nafikiri pangekuja Muswada hapa wa kulazimishwa mabenki yawakopeshe wakulima na wafugaji ili benki itakayoshindwa kukopesha hata mfugaji ifukuzwe iondoke, hakuna sababu ya kuwa na mabenki ambayo hayawaimarishi wananchi hawa. *(Makofi)*

Nina uhakika wafugaji makubwa wakikopeshwa, uchumi wetu utakua, hata mchango wa sekta ya mifugo ambao ni asilimia 2.4 utaongezeka na wananchi watafaidika. Kwa hiyo, nafikiri nakubaliana na wewe kabisa kwamba, mabenki yaanze kujifunza na kuweka utaratibu wa kuanza kuwakopesha wafugaji na wakulima, badala ya kuendelea tu kufanya utaratibu unaofanywa sasa hivi na kubaki na mapesa mengi kwenye mabenki ambayo hayawezi kukopesha. Hii ni *challenge* kwa mabenki na nafikiri wahusika watazidi kuwaeleza na kuwaomba, haya mabenki yaanze kujifunza kukopesha wakulima na wafugaji. *We need to be serious, we are serious Mr. Sanya.*

Tuamke vichwa badala ya kuamka miguu, tunatumia vyote vichwa, miguu, viuno na vyote ndiyo maana masuala haya yanaenda vizuri. Tanzania tusiwe mahodari wa kuleta Miswada tutafute masoko, lakini kabla ya kutafuta soko lazima uwe na Muswada ambao utasaidia katika kutafuta soko na ndiyo maana tumeona tuulete kwanza huu Muswada ili masoko yaje. Bila kuwa na Muswada, hata huyu anayekuja kuwekeza hawezi akaja akawekeza kwa sababu hatakuwa anajua taratibu na sera zinazotakiwa kutekelezwa.

Elimu kwa wafugaji; nakubaliana naye, tutangaze bidhaa zinazotokana na ngozi; huu ni ushauri mzuri, kwa hiyo, mchango wote ni mzuri, hakuna mtu ambaye anaweza akapinga mchango mzuri ambao umeutoa. Kwa hiyo, tunakubaliana na wewe na hii ni changamoto. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sanya pitisha huu Muswada tukaanze kazi bila kuchelewa.

Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, anaunga mkono Muswada huu hata kama umechelewa, anazungumzia suala la ngozi ya samaki; *actually,* kwa sasa hivi kuna kiwanda kule Mwanza kinatengeneza ngozi zinazotokana na bidhaa ya samaki na mabegi mazuri sana, siku utakapotembelea Mwanza utaanza kuona. Kwa hiyo, kwa sababu pia upande wa bahari tuna samaki wengi, mimi nafikiri Mheshimiwa Mnyaa, tuanze

kuwahamasisha watu waanzishe viwanda vya kutengeneza bidhaa za ngozi zinazotokana na samaki. Inawezekana pia tunaweza kutumia hata mradi wa *MANCEP* katika kuwahamasisha watu kujiunga pamoja na kuanzisha viwanda vidogo vidogo, vitakavyoweza kuanza kutengeneza bidhaa za samaki na kadhalika.

Mwanza kuna kiwanda ambacho kimeanza kutengeneza bidhaa za ngozi za samaki, zinazotokana na Sangara. Kwa hiyo, ninaamini hii wana *add value* na bidhaa zile, mabegi yale yanapendwa kweli na watu na wanasafirisha mpaka nje. Kwa hiyo, watu kama hawa ni lazima tuwahamasishe na mabenki yetu basi yaanze kuwakopesha watu kama hawa ili viwanda vyao vikue na kutoa *employment* kwa Watanzania zaidi.

Ametoa mfano wa samaki Chewa, Tao, Songoro, Papa na kadhalika; mimi nafikiri hizi ni changamoto ambazo tunatakiwa tuzichukue katika kuhakikisha kwamba tunafanya haya. Amezungumzia mengi, ngozi za chatu na kadhalika, viwanda vya *tanneries* vya Mwanza vimekaa tu; ndiyo maana tumeleta Miswada hii ili sisi pamoja na wenzetu wa Wizara ya biashara, tushirikiane katika kuhakikisha kwamba, tunaboresha hata vile viwanda ambavyo vilikuwa vimechukuliwa kwa ajili ya bidhaa za ngozi.

Mheshimiwa Telele, ameunga mkono hoja, amezungumzia juu ya Wamasai na Wasukuma walivyo na tabia ya kugonga mihuri kwenye mifugo yao ili isiibiwe na kadhalika. Hii itaendana na Muswada utakaokuja wa Ustawi wa Wanyama. Pia amesema, Serikali iweke utaratibu wa ununuzi wa mifugo; haya yote nakubaliana nayo, ngozi itumike pamoja na kwamba inatumika kama vitanda na magondoro sehemu nyingine lakini tukiweka utaratibu mzuri itaweza kuboresha maisha ya Watanzania. Mimi nakubaliana naye kabisa na ndiyo maana Muswada huu utakapopitishwa, tunaweza tukaanzisha minada ya ngozi katika kila Halmashauri na kuuza ngozi inayokusanywa na baadaye zikauzwe katika masoko mengine ya nje. Kwa hiyo, Mheshimiwa Telele, nakubaliana na ushauri wako, dawa za mifugo pia umezungumza ni muhimu kwa mfano kupe ni moja ya mdudu ambaye anasababisha uharibifu wa ngozi.

Ukatili wa wanyama; yeye anaona kwa mfano, ng’ombe akikokota jembe ule ni ukatili. Katika Muswada utakaokuja, tutazungumza vizuri kuhusu ukatili wa wanyama. Amezungumzia pia mfano wa *volcano* iliyotokea kule na ng’ombe sasa hivi wanavyostawi. Tatizo mikoa haitaji hawa watu lakini wanahitaji nyama ya mifugo hiyo na kadhalika; nakubaliana na wewe kabisa na mimi ningependa nitoe wito kwa viongozi wote, wasiwanyanyase na kuwasumbua sana wafugaji. Wafugaji wanatakiwa kufuga kisasa, kwa kuzingatia sheria zilizopo lakini pia waishi salama na wakulima kwa sababu kila mmoja anamtegemea mwenzake, Wakulima, wafugaji, wafanyabiashara, wavuvi na Watanzania wote, tunategemeana na wote ni muhimu katika kuleta maendeleo ya kweli na kujenga uchumi wa nchi yetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Telele, nakubaliana na ushauri wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pinda Chana yeye amesema anatokea … *(Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi Chana; unajua majina ya watani zangu haya ni magumu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema yeye anatokea kwenye eneo la wakulima badala ya wafugaji, lakini mimi nataka kumhakikishia kwamba, yeye pia ametokea kwenye eneo la wafugaji, kwa sababu kufuga si ng'ombe tu, hata mbuzi na kondoo. Hata ukifuga kuku ni mfugaji, ukifuga kondoo ni mfugaji, ukifuga nguruwe ni mfugaji, ukifuga mbwa ni mfugaji, kwa hiyo, nina uhakika asijitoe na yeye pia ni mfugaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ametoa maelezo kuhusu sehemu ya pili ya kifungu cha saba, Wajumbe wazingatiwe *professions* zao na kadhalika na ushauri mwingi ameutoa, nimeuchukua. Yapo mengine ambayo hatukutaka kuyaandika kwenye sheria, tukaona tuyaweke kwa ajili ya *regulations* ili yasiwe kila mara panapotokea mabadiliko tuje humu kubadilisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Pindi Chana, nakubaliana na ushauri wako mzuri.

Amezungumzia pia kuhusu ruzuku ya mifugo, *zero grazing* na kuhusu leseni za miezi 12; anaunga mkono lakini baadaye tuangalie kama zinaweza zikawa *extended*. Amezungumzia pia katika kifungu cha 25 sura ya pili kinachohusu faini, pawepo na marekebisho kidogo kulingana na hali halisi ya hizo faini. Kwa ujumla, ushauri wa Mheshimiwa Pindi Chana tunaukubali, mchango wake ni mzuri tu na ameunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, naye ameunga mkono hoja na ametoa pongezi kwa Wizara. Suala la pembejeo kwa mifugo anasema ni lazima liwekewe mkazo na mimi nina uhakika Serikali kwa ujumla, tutakuwa tunasikia na inawezekana katika mwaka unaokuja masuala haya yatakuwa yameongezwa. Watu wanaopewa *tender* ya kuuza dawa za mifugo wapewe watu wanaotoka kwenye maeneo yanayohusika. Nimelichukua hili na tutalifanyia kazi ili tuone hawa wanaopewa *tender* kwa ajili ya ku-*supply* dawa za mifugo wahakikishe kweli wana-*supply* dawa badala ya kuwa wanafanya utapeli. Kwa hiyo, ninakubaliana na hii changamoto tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngozi zetu ni mbaya lakini hatuna machinjio ya kisasa na mimi ninakubaliana nayo kabisa, kwa sababu mifugo karibu asilimia 60 inachinjwa Dar es Salaam, lakini ukienda Vingunguti ni kazi, hata wanaojenga viwanda vya nyama, hawajengi maeneo kwa ajili ya kutengenezea ngozi. Hii ni changamoto, lakini ninaamini kadiri muda unavyokwenda na Muswada huu ukishapitishwa, nina uhakika tutaendelea kuboresha. Hizi changamoto ambazo zimetolewa, tutaendelea kuzifanyia kazi ili mambo haya yote mliyotushauri Waheshimiwa Wabunge, tuweze kuyafanyia kazi kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujafundisha watu kuhusu masuala ya ngozi, hii ni changamoto na ndio maana tumeeleza kwamba, tutajitahidi na tutaweka baadhi ya kozi za maafisa ugani, zitakazokuwa zinafundisha masuala ya ngozi hasa hawa *dressers* na

wale wengine katika kuhakikisha kwamba, Muswada huu usije ukabaki hewani na ukawa hauna wataalamu wa kuweza kuutekeleza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Mzindakaya kwa ujumla tunakubaliana wewe.

Ubora wa vyakula na afya za watu, halafu amezungumzia *challenge* ya kwamba, Kenya wanaingiza nyama huku kwetu lakini sisi haturuhusiwi kupeleka kwao. Ametoa mfano pia wa suala la Kiwanda cha Maziwa cha Mara, suala hili bahati nzuri tulilipata na tumeshampatia Waziri wa Afrika Mashariki linashughulikiwa, kwa sababu kuna sheria ambazo zinahusiana na masuala ya Afrika Mashariki. Nina uhakika, baadaye masuala haya yanaweza kutafutiwa ufumbuzi, kwa hiyon hata hilo suala la nyama nafikiri tumelichukua na tutaangalia ni namna gani tunaweza kuliboresha na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kuna michango mingi ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge na kwa ujumla ni mizuri na tumeshaiandika hapa kwa ajili ya kutoa ufafanuzi mkubwa zaidi. Ninaamini kabisa kwamba, baada ya Bunge hili, tunaweza tukatoa huo ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao iliyokuwa imetolewa. Kwa hivi sasa ninajua zimebakia dakika tano tu, inakuwa ni vigumu kuchangia.

Wale wote waliochangia kwa maandishi, pamoja na kwamba walikuwa saba, wamezungumzia juu ya Maafisa Ugani. Kwa mfano, Mheshimiwa Juma Killimbah, amezungumzia soko la ngozi na malisho. Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa yeye amechangia hapa. Mheshimiwa Peter Msolwa amezungumzia kuhusu viwanda. Mheshimiwa Bujiku Sakila, anaunga mkono na anaomba semina elekezi. Mheshimiwa Maria Hewa, amezungumzia kuhusu kufufua viwanda. Mheshimiwa Vuai Abdallah naye amezungumzia masuala mengine yanayohusu ngozi. Mheshimiwa Zabein Mhita amezungumzia kuhusu Maafisa Ugani, upungufu wa ruzuku na maeneo ya wafugaji ambayo kwa ujumla nimejaribu kuyafafanua, lakini kwa sababu muda ni mfupi, siwezi nikayaeleza yote, tutawajibu Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu, mimi napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao mizuri sana. Imetusaidia sana sisi, nilipokuwa nikikutana na wataalam wangu; Makatibu Wakuu, Naibu Waziri na Watendaji wengine wote katika Wizara tumesema, michango ya leo itatusaidia sana katika kuhakikisha sasa sekta hii ya mifugo tunaiweka kwenye *direction* iliyo nzuri. Ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, Muswada huu tuupitishe ili tukaanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninawashukuru wote, ninaomba kutoa hoja. Ahsanteni. (*Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi wa Mwaka 2008 *(The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii ya 15(2), ukurasa ule wa 10 kwenye zile *marginal notes* pale …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William Shellukindo ukurasa wa ngapi?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Ukurasa wa 10, *sorry* ukurasa wa 16.

**MWENYEKITI:** Hatujafika.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 16

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ibara hii, ibara ndogo ya pili kwenye *marginal notes* zile kuna kitu kimoja ambacho ningeomba tukubali kisahihishwe, kwa sababu kimeendelea kwenye maeneo mengine. Lile neno *lisense* pale ni c, hii iliyopo hapa ni kile kitendo cha kutoa leseni, sasa imeendelea katika maeneo mengine inafuata huko hii *license* ya namna hii ambayo inatakiwa iwe *noun* kwa maana ya "c" bado ilichukuliwa sehemu yoyote ilipoonekana hapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hili nadhani halina tatizo. Waheshimiwa Wabunge, nadhani halina tatizo tunaweza kusema ni *typing error;* nadhani wote mmeona pale.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo *typing error*, inaweza kuwa huyu pengine amesomea Marekani; Wamarekani wanatumia "se" na Waingereza wanatumia "ce" kwa *license*, ile ni *document.* Kwa hiyo, siyo *typing error* kwa sababu imeendelea na kwenye ibara nyingine zinazofuata huko, nilitaka tu isionekane hivyo kuwa ni *typing error*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William Shellukindo, hakuna tatizo tumekubaliana kwamba, nadhani *concept* yako unataka iwe c badala ya s na Mheshimiwa Waziri hapo amekubali, nadhani halina tatizo. Ndio maana tumelihoji Bunge, pamoja na rekebisho hilo la kuondoa s na kuweka c na haibadili maana ya kifungu chenyewe na hivyo Wabunge wameafiki.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 32(4), ile sentensi ya pili ukiisoma pale ambapo inasema *which the offence has committed*, pana *omission* pale *has been committed*, nimeangalia jedwali la marekesho hawakuirekebisha hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, una tatizo na hilo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala hamna tatizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William Shellukindo, nafikiri halina tatizo, hana tatizo na marekebisho ambayo unayapendekeza.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 34

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hiyo ya 34(n), ukurasa wa 20, hapa ilikuwa tukubaliane kwamba …

**MWENYEKITI:** Ibara ndogo?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Ya (n) ukurasa wa 20, inaanza na *imposition of cess or tax on hides,* nilikuwa ninapenda kupendekeza kwa Wabunge kwamba, tusiishie hapo; kule mwisho tungeweka *in consultation with the minister for finance,* kwa sababu inataja *cess and tax.*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo mtaalamu sana wa sheria, lakini ninafikiri tuiache hivi hivi; huwa wanakutana tu Waziri wa Mifugo wa nini, wote wapo pamoja. Kwa hiyo, kama kuna suala litajitokeza huko wataulizana tu. Mimi nafikiri tuliache hivi hivi ili tusiharibu kazi nzuri iliyofanywa na wanasheria.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Sheria ya Bunge, tusiache tu kitu kikawa wazi. Nakumbuka wakati tunatunga sheria hapa, nadhani ya *Rural Energy Agency,* nadhani Waziri ambaye sasa hivi anakaimu U-*Chief Whip* pale anakumbuka kwamba, tulizingatia hivyo kwamba hizo *consultation* siyo za hiari siyo za kukaa, hapana ni za kisheria *cess and tax.* Mwenye kazi hiyo ni Waziri wa Fedha isiachwe wazi tu kwenye sheria hii, mimi naomba twende na taratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William Shellukindo, mawazo ni mazuri sana, sasa ili tuweze kwenda vizuri na kuliamua hili, ungetusaidia kutuletea *schedule of amendment* mapema. Nadhani tungetakiwa kuliomba Bunge hili, liweze kuona tunafanya nini katika hili na hasa tunapofikia *contradiction* kati ya wewe mtoa hoja na Mheshimiwa Waziri, ila kama Waziri angekuwa anakubaliana na hilo. Kwa maana hiyo sasa, kwa hatua tuliyonayo, itabidi tuikubali kama ilivyo na labda Mheshimiwa Waziri, sasa kwenye Kanuni zenu mnaweza kuona mnalifanya vipi, labda Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa tutaliangalia namna ya kuliweka katika Kanuni ili kusudi tuzingatie hoja ya Mheshimiwa William Shellukindo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba ni dakika za mwisho, kwa uzoefu tulioupata na malalamiko ya maeneo mbalimbali, kwa kweli hizi nafasi zinapojitokeza kwamba tumeona kuna utata ni vyema tuka-*include* kuliko kuweka tu Kanuni. Mimi nadhani haitakuwa na ubaya, naungana na Mheshimiwa William Shellukindo iwekwe wazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eng. Manyanya ni kweli kabisa tunakubaliana na hivyo, lakini ni lazima tuendelee kufuata Kanuni na taratibu ndani ya Bunge. Mara nyingi mmeona tunapofikia hatua ya namna hii, kama hatutakuwa tukifuata utaratibu, basi hatua hizi zitamfanya kila Mbunge ainuke na kutoa pendezo la kitu anachoona kinafaa na ndio maana sasa tunawajibika kumwomba Mheshimiwa Waziri, suala hili lizingatiwe kwenye Kanuni kulingana na utaratibu wa Kanuni za shughuli zetu za Bunge.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nadhani hutakubali twende kwenye Kanuni, kwa sababu limeletwa mchana huu. Nilikuwa napenda kushauri kwamba, pale kile kifungu cha kwanza pameandikwa yule *Chairman, who shall be a qualified person in high skin and leather matters*, nadhani tunaifunga sana hapa kwamba, unaweza kuweka huyu *technician* wa *high skin*.

Tungeangalia fani yote hiyo, mimi nadhani tungeweza kuweka kwenye *shall be a professional in the livestock development and management* ili upate mtu mwenye upana zaidi, siyo yule kwa sababu hawa wataalamu nadhani wanajifunza fani ya mifugo kwa jumla, halafu kunakuwa na *specialization* kwenye *hides* na vitu kama hivyo. Sasa tusije tukaifunga tukapata watu walio-*specialize* kwenye *hides* lakini *management* ya hiyo *sector* hawana, ilikuwa ni ushauri wangu tu huo ambao nilitaka kuutoa katika hilo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilizungumzwa pia hata kwenye Kamati, lakini lengo kubwa lilikuwa ni kuiendeleza *sector* ya ngozi. Hatutaki mtu mwenye utaalamu wa nyama ukampeleka kwenye ngozi, mwenye utaalamu wa pembe ukampeleka kwenye ngozi, mwenye utaalamu wa utumbo unampeleka kwenye ngozi, kwa sababu kuna sheria nyingi; kuna Sheria Namba 16 ya Mwaka 2003 inayohusika na *Veterinaries*, kuna Sheria Namba 8 ya Mwaka 2004 inayohusika na maziwa, kuna Sheria Namba 10 ya Mwaka 2006 inayohusika na nyama na kadhalika.

Sasa hii ni Sheria ya 2008, inayohusika na ngozi. Kwa hiyo, tu-*concentrate* na watu wa ngozi, tusije tukamweka mtu pale ambaye hana *qualification* ya ngozi halafu akaharibu nia nzuri ya Waheshimiwa Wabunge, mnayotaka kuifanya.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea hiyo lakini tunazungumza *Chairman, broad enough,* hiyo naishia hapo. Ninaendelea kwenye kifungu cha kwanza pale ©, ningependa ufafanuzi pameandikwa *director* lakini haijulikani *director* kutoka wapi, imekuwa *lifted* hii kutoka kwenye ule Muswada wenyewe, nadhani hapo tungeweka ufafanuzi, hiyo ni moja.

Pia kwenye kifungu cha pili, kwenye jedwali pale inaposema *a member of the council appointed under paragraph one shall hold office for three years and shall be eligible for the appointment*. Hapa tungeiweka wazi, kwa sababu kuna wanaoingia kwa nyadhifa zao. Sasa mimi nilitaka kusaidia hapo kuifafanua kwamba, ile *paragraph one* ambao watakuwa *eligible for the appointment* iwe ni *(a) Chairman,* halafu kuanzia (e) mpaka (i) hao ndio ambao wana-*serve* kwa miaka mitatu, wale wengine ni *professionals* kama yupo, yaani ni Idara kwa mfano *director* wa *veterinary services* siyo miaka mitatu ni kwamba yupo huyo wakati wote. Halafu upande wa kusema *shall be eligible for the appointment*, nadhani tungetumia *may be eligible* badala ya kusema *shall be eligible, shall* maana yake ni lazima.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi ninashindwa nijibu nini, kwa sababu sheria zinaandikwa na wanasheria na mimi siyo mtaalamu wa sheria, ndio maana ninazungumza tu katika yale ya jumla. Kwa sababu katika *experience* ambayo huwa ninaona, hizi *first schedule* huwa zinaandikwa hivi. Sasa labda kwa sababu kuna wataalamu wa sheria hapa, watusaidie kujibu lakini katika *profession* pia ya huyu *Chairman*, *Chairman* ni mtu mmoja tu, kweli Tanzania akosekane mtu aliye na utaalam wa ngozi na kadhalika?

Kwa hiyo, mimi nashindwa kuchelea kubadilisha hapa kwa sababu sina *detail* sana za wanasheria, inawezekana wanasheria ambao wapo humu watatusaidia kwa haya anayoyazungumza Mheshimiwa William Shellukindo. Kwa sababu tunaweza kubadilisha halafu tukawa tumeharibu sheria kabisa na mimi sitaki kuingilia *profession* ambayo siijui.

**MWENYEKITI:** Lakini kwanza kwa mfano kile kifungu kidogo cha (c) *director*, sasa hata hiyo Mheshimiwa Waziri huwezi ukatuambia ni *director of what?* Tunasema pale kwenye kile kifungu kidogo cha pili ile *may* na *shall* kweli inaweza ikahitaji utaalamu, lakini tunapotaja wale *committee members*?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *director* kwa mfano kwenye *definition* kwenye ukurasa wa nne imefafanuliwa vizuri, *means the Director responsible for Hides, Skins and Leather Development in the Ministry responsible for livestock development* na ndio imetajwa huko. Kwa hiyo, angeangalia huku inajionyesha vizuri. *(Makofi/Kicheko*)

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi wa Mwaka 2008,**
***(The Hides, Skins and Leather Trade Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi wa Mwaka 2008, ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo kama ulivyorekebishwa na Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Shughuli za kupitisha Muswada huu zimekamilika na sasa Muswada huu utaingia katika hatua ambayo inamuhitaji Mheshimiwa Rais, aweze kumalizia kazi yake. Ukishatangazwa kwenye gazeti letu, utakuwa ni sheria ambayo itaanza kutumika katika nchi yetu. Sisi kama Wabunge tumeshamaliza kazi yetu ya awali katika kutunga sheria hii mpya na tumehitimisha mfupi uliopita.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kazi hiyo, shughuli ambazo zimekuwa hapa mezani kwa siku hii ya leo tumeweza kuzikamilisha zote na kabla sijaahirisha shughuli hizi, nitatoa matangazo machache.

Nimeombwa na Kaimu Katibu wa Bunge, niendelee kuwakumbusha tangazo la semina ya Jumamosi na semina ya Jumapili. Kama tulivyoambiwa, semina ya Jumamosi itahusu ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuanzia saa tatu asubuhi Ukumbi wa Pius Msekwa. Labda niwafahamishe Mwenyekiti wa semina hiyo, Mheshimiwa Wilson Masilingi, ndio atakayeongoza semina hiyo kesho; basi tumtakie tu kila la kheri aamke salama ili kesho aweze kuifanya kazi hiyo vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, Jumapili tutakuwa na semina kuhusu mapendekezo ya Muswada mpya wa Sheria inayohusu Wanyamapori. Sheria hiyo ambayo itakuwa ni ya mwaka 2008, lakini ukiingia mwakani nadhani tunaweza kuiita vinginevyo, semina hiyo nayo itaanza saa nne nusu asubuhi. Ninaamini baada ya shughuli za ibada ya asubuhi na itafanyika pia Ukumbi wa Pius Msekwa.

Vilevile kuna kamati nyingine tatu ambazo zimeshapata barua ya mwaliko, pamoja na Kamati ya uongozi ya Bunge, nayo itakuwa na semina baada ya semina hii ya wanyapori asubuhi. Kwa hiyo, semina nyingine itaanza baada ya semina hiyo ya asubuhi.

Baada ya tangazo hilo, nimeombwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wa CCM, niwaarifu Wabunge wote wa CCM kwamba, Jumatatu kutakuwa na Kikao cha Caucus ya Chama. Kwa hiyo, wale watakaosafiri *weekend* basi wakumbuke tu Jumatatu kutakuwa na kikao hicho waweze kurejea tena Bungeni kwa ajili ya kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii, niwashukuru na niwapongeze kwa kazi ya leo. Kwa kuwa shughuli zetu zimeisha, basi ninaomba sasa niahirishe shughuli hizi za Bunge na tutakutana tena ndani ya Ukumbi huu Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.29 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 03 Novemba, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*